# CONSTITUTION OF KENYA REVIEW COMMISSION

# (CKRC)

## VERBATIM REPORT OF

## CONSTITUENCY PUBLIC HEARINGS, VOI CONSTITUENCY, HELD AT VOI MUNICIPAL HALL

ON

29TH APRIL 2002

**CONSTITUTITITUENCY PUBLIC HEARINGS, VOI CONSTITUENCY HELD AT VOI MUNICIPAL HALL ON MONDAY 29TH APRIL 2002**

**Present:**

Com. Zein Abubakar
Com. Keriako Tobiko
Com. Prof. Wanjiku Kabira

**Secretariat in Attendance**:

Fatumma Jama - Program Officer
Onesmus Kipchumba - Asst. Program Officer
Alice Thuo - Verbatim Recorder
Nancy Odipo - Sign Language Interpreter

**Meeting was called to order at 8.45. a.m.**

**Com. Abubarkar:** Ma-commissioners wetu ambao wamefika na wananchi nawasalimia, hamjambo? Mimi niko na furaha leo kwa siku hii ambayo haijawahi kuonekana katika maisha. Ni fursa ambayo imetolewa ili tuweze kuwasilisha maoni yetu kwa ajili ya Katiba yetu ya Kenya. Na ninafikiri ya kwamba kila mmoja aliyekuja ako tayari kabisa kutoa yale ambayo yako moyoni

kwa kuandika ama kwa kunena. Kwa hivyo kabla hatujaanza kufanya hivyo nitamuita Rev. Mcharo anje atufungulie kwa maombi. Karibu.

**Rev. Mcharo:** Naomba tusimame tafadhali. Basi tuombe. Mungu baba wetu wa mbinguni, uliye muumba wetu unayetuhifadhi mwili na roho na pia unayetujali unayekutana na mahitaji yetu kwa kila upande. Tunakushukuru Mungu wetu kwa sababu ya kutujalia tukaweze na kufikisha siku hii salama. Siku ambayo ilikuwa inaonekana kuwa mbali sana lakini Mungu kwa upendo wako umewahi kutusaidia kutufikisha siku hii. Tunakushukuru kwa ajili ya wageni wetu ambao wamesafiri mwendo mbali ili kuweza kukutana na wananchi wa Voi ili Bwana tukaweza kutumia fursa hii kutoa maoni yetu, kuchangia katika marekebisho ya Katiba ambayo ni chombo muhimu sana kwa kila taifa.

Naomba kwamba tunapoenda kufanya hayo uweze kutupa hekima, uweze kutuhakikishia pia uhuru wa kutoa maoni haya na yale ambayo tutachanga, na yale yatachangwa na wengine katika taifa hili hatimaye tuweze kuwa na Katiba ambayo inatokana na maoni ya wananchi, na iweze kukaa na kumlinda kila mwana Kenya popote alipo bila kujali ni wa kike, niwa kiume, ni wa rangi gani na umri gani. Hivyo basi tunapoanza kikao hiki Mungu uishiye milele uweze kukibaliki. Tusaidie, asante kwa ajili ya maisha ya kila mmoja. Asante kwa ajili ya maoni ya kila mmoja yanaoenda kutolewa leo. Naomba kwamba utusaidie kutumia fursa hii vizuri kwa ajili ya utukufu wako na kwa ajili ya manufaa ya nchi yetu ya Kenya. Kwa jina la Jesu Kristo Bwana wetu. Amen.

**Com. Abubakar:** Basi nashukuru kwa ajili ya maombi hayo ni kwamba kabla hatujaanza pale tuko na mwenye kiti wa hii kamati ya Voi kwa hivyo tunaomba akaribie ili aweze kuwakaribisha Macommissioners. Na kabla hajafanya hivyo ningaliomba wale wanakamati wa 3C's wainue mkono wajulikane kwamba wako hapa. Mimi ninayesimama naitwa John Maranda ambaye ni katibu wa kamati hii. Kwa hivyo karibu mwenye kiti. Commissioners wetu wametutembelea kutoka Nairobi mpaka hapa namuomba mjisikie mko nyumbani na wengine mliokuja hapa muwe huru katika kutoa maoni yenu.. Karibuni mmekaribishwa. Asante sana.

**Com. Tobiko:** Asante sana mzee Mwasi mwalimu wangu. Kwa heshima kubwa ningependa kutangaza kikao hiki kuwa kikao lazmi cha Tume ya kurekebisha Katiba ya Kenya kwa ajili ya kukusanya maoni ya wakenya ili kurekebisha Katiba yetu. I would like to formally declare this gathering as a formal sitting of the Constitution Review of Kenya Commission for the purpose of collection of views from Kenyans for amending our Constitution.

Jambo la pili ningependa kujijulisha. Mimi ni kujijulisha kwangu ni kwamba sisi ni kutoka Tume la kulekebisha Katiba. Nitaanza na mkono wangu wa kushoto kumuomba commissioner mwenzangu ajitabulishe kwenu halafu ninje mkono wangu wa kuume kuomba commissioner mwenzangu ajitabulishe kwenu halafu mimi nitajitabulisha kwenu.

**Com. Kabira:** Hamjamboni? Mimi naitwa Wanjiku Mukabi Kabira, ninafundisha University ya Nairobi lakini kwa leo

ninafanya kazi na hii Tume yetu. Asanteni.

**Com.Tobiko:** Hamjamboni ndugu? Kwa jina naitwa Keriako Tobiko na mimi ni commissioner.

**Com. Abubakar:** Na mimi naitwa Abubakar Zein baadhi yenu mtakubuka nilikuwa nanyi hapa tukiwambia kwamba tutarudi ili kukusanya maoni ya wakenya. Hivi sasa tumerudi mara ya pili kufanya hivyo. Tutatumia utaratibu niliowaeleza wakati ule kwamba. Ili kukubushana tu, ukiingia pale utakuta mtu anandika register, kwa hivyo kuna majina tushapewa ukisha pewa form namba one majina ya kwenda mpaka kumi na saba. Baada ya hapo tutaita majina kufuatana na orodha hii na ukiitwa jina lako ukija kutoa maoni yako, ukiwa umeandika mswanda wako, if you have a memorandum, tutakupa sisi dakika tano. Ukiwa huna memorandum unataka kuja kuzungumza peke yako, kutoa maoni yako kwa kauli yako kwa mazungumzo, tutakupa ndakika kumi. Lakini ukiwa pia unataka kutoa memorandum yako bila kuzungumza unaruhusiwa kufanya hivyo. Ikiwa unataka kutoa memorandum yako bila mazungumzo, utaikabidhi pale kwa staff members wetu ambao nikimaliza kuwapa mwelekeo wa kutoa maoni nitaomba fursa nijitabulishe kwenu.

Jambo lingine: Unaruhusiwa kutumia Kiswahili, Kiingereza au lugha ingine yoyote ya Kenya. Ikiwa utatumia lugha ingine yoyote ya Kenya ikiwa si Kiswahili au Kiingereza, tumefanya matayarisho kutakuwa kuna mtu ambaye atakuja kutafsiri lugha hio kwa Kiswahili au kwa Kingereza.

Jambo lingine: Tungewaomba sana ikiwa tutaanza kazi hii ya kutoa maoni, ukiwa una jambo ambalo limezungumziwa na mwingine sio uliwache unaweza kulizungumzia lakini si kwa ulevu kama aliezungumzia mwenzake. Useme tu mimi maoni yangu kuhusu jambo hii na hii kwa ufupi. Halafu sisi tutakaa hapa mpaka saa kumi na mbili jioni. Na hilo ni onyo nzuri kwamba ukiwa una simu ya mkono unatakiwa uizime. Yangu nisaizima. Ukiwa una simu ya mkono uizime kwa sababu inahitirafiana na kurekodi kwetu kwa mazungumzo haya.

Tutakaa hapa mpaka saa kumi na mbili jioni. Ikifika saa kumi na mbili jioni bado kutakuwa na Wakenya ambao wangetaka kutoa maoni yao, tutaendelea na kazi hio mpaka tutakapomaliza.

Mnajua kwamba Voi pia tutakaa kikao kingine kesho. (Katika Voi constituency,) Kwa hivyo ikiwa leo tutaongea kesho iko fursa.

Jambo lingine ni kwamba sisi tunarekondi kila maneno yanayozungumzwa. Tutakuwa tukichukua maandizi lakini tunarekondi kila neno ili neno lolote lizipotee. Utaona mmoja wetu akirekondi na mwingine anaandika kwa mkono.

Jambo lingine, tumekuja na mtu ambaye atatafsiri kwa ishara – sign language interpreter. Kwa wale ndugu zetu mlemavu ambao pengine hawasikii, kutakuwa kuna mtu wa kutafsiri. Sijui kama tunaelewana? Sasa mimi ningeomba niombe fursa watu

tuliokuja nao kutoka katika Tume wajitabulishe kwenu halafu tuanze mazungumzo yetu kupokea maoni yenu.

(Introduction inaundible)

Kwa hivyo ningependa kumuomba Bwana Christopher Ayanda, Lamu organising secretary awe mtu wa kwanza kutoa maoni yake na kama aliavyoandika hapa kwamba ana a written memorandum, Mr. Ayanda una ndakika tano. Fursa Umepewa ndakika tano. Asante.

**Christopher:** Macommissioner wetu, wananchi wa Voi, kwanza ningesema hatuji kurekebisha Katiba ila tumekuja kuvunja Katiba. Kwa sababu uhuru wa Katiba iliokuwako haukuwako. Na kama tunakumbuka alipozungumzia Shikuku Bungeni juu ya vile mambo yanaviotendeka Kenya na Seroney akiwa speaker wa mda alipouliza Seroney kusubstantiate aliposema "why substantiate the obvious", wote waliwekwa Manyaani. Kwa hivyo tunakuja kutunga Katiba ya kutuweka huru. Ijapo nimeandika nikijumlisha na vipengere vingine vya Katiba ilipokwisha lakini hapa sidhani kuna zaidi ya kumi wanaoiujua Katiba ilioko. Kwa sababu tulikuwa na uoga wa kuitafsiri, au kuambia wananchi.

Jambo lingine ambalo ni muhimu na hii macommissioners mtanisamehe, nitalisema. Ni kwamba sisi Wakenya tumewekwa watumwa kiakili. Kila Commission inapokuja hapa inakuja kutuchunguza tuko vipi watummalize. Ilikuja Commission ya Njonjo hapa, kuja kuzungumza juu ya ardhi. Badala yakutuokoa imetuweka katika zogo ambalo hivi sasa wenzetu wafanya kuletewa karatasi katika plot inayoishi. Kwa kuwa wewe ni temporary sijui ni nani permanent duniani. Jambo hili tunasema mambo ya ardhi ni Katiba ichunguze yachukuliwe yawe yanaendeshwa na wazee wa pahali pale wala si ardhi na council na nini, maana italeta zogo kama yale yaliotokea Molo, Burnt Forest na huku Likoni. Sisi hatuwezi kuficha hayawezi kutokea, yaweza kutokea na yameanza kuonyesha ncha. Kwa hivyo kwa sababu tunaelewa ardhi ni mwanadamu na katika memorandum hii nimewakubusha muangalie kitabu cha Mungu kilichompa kila mtu pahali pake asiguzwe na mtu kwa nguvu.

Jambo lingine ni kwamba sisi sasa hatutakubali uchaguzi ufanywe kabla Katiba haijamalizika. Kwa sababu pendekezo letu kwa sasa wengi wetu ni majimbo, sio serikari ya umoja, serikari ya majimbo. Kwa hivyo ikiwa utachaguliwa sasa, serikari moja wakati itakapokuwa Katiba imekubali kuwa ni majimbo, je tutarudia uchaguzi tena? Kwa hivyo ni kwamba Bunge liongezwe mda mpaka Katiba iishe. Sisi tunasitikika kwamba wabunge wakifika huko huwa ni maBwana wakubwa. Wananchi ndio maBwana wakubwa ndio wanawachagua na hawana ruhusa kwenda kuamlisha tajiri wao. Kwa hivyo wabunge wahakikishe wananchi wanataka nini. Kwa sababu sitaki kupoteza mda kwa point zangu, ningependa kwamba pia kuongeza Katiba hio iongeze kwamba ma Chairmen na ma Mayor watakuwa wakichaguliwa na wananchi sawa na wabunge na madiwani. Kwa sababu hii mambo ya kuchagua madiwani nao wachague chairman mwenye pesa atakuwa anatutawala akitumia nguvu zake za pesa na mambo mengine na atatuongoza katika njia isiofaa. Haya, nafikiri ili naona wenzangu wanazidi kuongezeka hata mbunge wetu ameingia nafikiri ni lazima tuelewe tumekuja kuunda Katiba kwa sababu Katiba ile ilioko ni wangapi wanaijua? Ukiuliza hapa utapata 3 kati ya wote walioko hapa. Kwa hayo ninapeana memorandum yangu ili muende muifafanue. Asante.

**Com. Abubakar:** Asante sana mzee Kayanda. Jisajiri pale na u-sign register, utakuwa umefanya jambo lasmi sasa. Wa pili ni Rev. Mcharo na ningependa kutambua rasmi kuasiri kwa mheshimiwa Mwakilingo. Karibu sana.

**Rev. Mcharo:** Macommissioners nina mambo yafuatayo ambayo naona kwamba Katiba yetu pengine hatuelewi hii ilioko sasa kwamba mambo haya yanahakikishwa kwamba yanafanyika vilivyo au vipi. Kwa hivyo la kwanza ningeliomba ni kwamba our Constitution to allow free primary and secondary school education in the government schools. Kwa sababu jambo hilo limerudisha elimu nyumma maana tunao wengi ambao hawawezi kujimudu kifedha. Kwa hivyo tunaona kwamba kuna matatizo mengi juu ya hiyo. Kwa hivyo ningeomba kwamba elimu ya msingi na ile ya secondary tuhakikishiwe kwamba katika Katiba hii ya sasa hakika kwamba ni bure ili wananchi waweze kusoma.

Ya pili, the Constitution to allow for free medical services in the government hospitals. Huu mpango wa kusema kwamba kugawana ghalama na kadhalika, ni mpango ambao umeleta matatizo. Wengi wamepoteza maisha, watu wengi wameishia kudawia maelfu na maelfu ya pesa kwa sababu ya ukosefu wa pesa. Kwa hivyo tunaomba Katiba ya sasa ihakikishe jambo hilo kwamba hakika tutapata hudumma za hospitali na matibabu bure.

And then thirdly, the Constitution should limit or even stop the registration of churches because at present they are becoming a menace. Kwa hivyo kama Katiba inaweza kusema ifunge mlango kabisa kwamba kusiwe na registration ya makanisa tena, maana yamekuwa ni kama maduka na mahali ambapo tunaelekea mahali ambapo hatuelewi tunaelekea wapi kama wakenya. Ingawa ninasema kwamba kuwe na uhuru wa kuabudu lakini uhuru wa kuendelea kuregister makanisa na makanisa it is confusing Kenyans.

Halafu ya nne bila kupotesa wakati, the Constitution should prevent devil worship and even go to an extent of exposing those who practise the same. Kwa sababu tumekuwa na shida na tunaambiwa kwamba kulikuwa na Tume ilikuwa inachunguza devil worship. I don't know whether the report has ever been made public. Na basi kama kuna watu na serikari inajua basi Katiba ikaweze kupata kuzuia jambo hilo isiendelee na wale wanaofanya hio pia wafichuliwe ili wajulikane kwamba hawa ni waabudu ibilisi.

And fifthly, the Constitution is strictly and only allow secret balloting during elections. Hii mambo ya mlorongo ni mambo ambayo inaletea watu shida. Kwa hivyo the Constitution is strictly and only allowed for secret ballot during elections. Asanteni.

**Com. Abubakar:** Rev. Mcharo, asante sana. Sign hio register. Ningependa kuomba Otieno.

**Otieno:** Asante sana kikao hiki cha commissioners ambayo imekuja kutoa maoni, nimefurahia sana mambo haya. Mimi sina mengi na mimi kama disabled Taita Taveta district, mimi ni chairman. Nagusia kidogo tu. Sisi tunapendelea tutabulike kikazi ila sisi tuwalemavu mguu ama mkono si ubongo. Ubongo ni timamu maana kuna mambo mengine tunatumia kiguru itupiliwe mbali

maana inalete taabu kwetu. Ukisikia mtu ametukana kiguru uko tayari kupigana naye maana hukupenda upate kilema kama hiyo na katika Kenya nzima tutabulike vile tumetabulika President wetu ametupenda sana na kupendwe na everybody, Kenya nzima kuhusu matatizo tuliyonayo kikamilike. Sina mengi nataka raia wa Kenya watambue wasiojiweza kama watu wengine. Sina mengi ni hiyo tu.

**Com. Abubakar:** Asante sana Bwana Otieno, tafadhali andika jina lako kwenye register. Anayefuatia ni Oliver Mwatei. Asante.

**Oliver Mwatei:** Honourable commissioners, mimi ni one of the 3C's members nawakilisia Bororo location ambapo mtakuwa kesho. Kwa hivyo nilikuwa nimetayarisha maoni yangu mengi ambayo nitatoa kesho lakini sasa hapa siwezi kosa moja ama mbili ambalo nitakalotoa. Mimi nilikuwa nataka nizungumzie juu ya uraia kwanza. Kwa mfano mimi kwa maoni yangu nilikuwa ninapendekeza kwamba mtoto ambaye amezaliwa na mzazi mmoja ambaye ni raia wa Kenya bila kujali jinzia mzazi, huyo mtoto apewe uraia bila swali. Huyo mtoto pia apewe jukumu na kupewa uridhi na kuajiliwa hapa Kenya bila kujali rangi yake. Katiba ambayo itakayoandikwa sasa isiruhusu mtu ambaye atakuwa na uraia wa nchi mbili. Kitambulisho cha kuonyesha kwamba huyu ni raia wa Kenya, kiwe nikitambulisho cha taifa na stakabadhi ya kuzaliwa.

Pia ningetaka kuzungumzia juu ya haki za watoto wa kike. Honourable commissioners, wazazi wengi sana wameadhiriwa kwa sababu wanapata extended families ambazo huwa hawatarajii. Kama kwa mfano, utakuta kwamba msichana amepata mimba ya mvulana. Zamani vile ilikuwa ni kwamba wazee huketi wakazumgumzia juu ya hiyo na kama wakigundua kwamba huyo mvulana ambaye ametajwa na huyo msichana ndiye alimweka msichana huyo mimba aidha hutozwa kiwango fulani kama hatamuoa huyo msichana ama kama akikataa kabisa tunaomba Katiba ambayo itandikwa sasa, huyo mvulana ambaye atakuwa ameharibu msichana kama huyo alee huyo mtoto mpaka yule mtoto atakapofika miaka kumi na nane. Kwa sababu wazazi wengi wanapata hasara sana wanalea watoto, wanafundisha halafu tena badaye unapata kwamba huyo mtoto anakimbia anapata babake. Hayo ndiyo machache ambayo ningetoa leo, lakini kesho huko Tausha nitakuwa na maoni mengi ambayo nitawakilisha mbele yenu. Asanteni sana.

**Com. Abubakar:** Asante Bwana Oliver. Tafadhali sign register huko. Tungeomba Bwana David Mwabunge. Basi imeandikwa vibaya hii. Imeandikwa Mwakibuge. Sorry Mwakirenge.

**David Mwakirenge:** Asante sana macommissioner na ma officer wote ambao mmefika hapa, ni shukurani nawasalimia nyote. Kwa kweli leo pia tunaona mabadiliko maanake mimi nimekuja kama mlemavu hapa na ni kitu kingine kimezungumzwa hapa. Nasikia kwamba ukiita mtu mlemavu ana uchungu mkali sana, naningependa kuwapa maneno yale ambayo kama mlemavu anaweza akatambulikana maana anaweza kuwa he is already educated man hata pengine ni wa form six. Lakini utakuta akizungumza na officer kwenye ofisi unakuta kwamba yeye anaangaliwa kama mtu ambaye hana maana yeyote. Lakini miaka hiyo ndiyo tumesikia kwamba tumekuwa considered na serikali tunaona kweli tutaweza kufanya kazi na ndugu zetu. Sasa basi

tumekaa na serikali muda mrefu lakini hatuoni lolote mbele likitokea kwa sababu sijui mtu anadharauliwa kama nimlemavu, maanake, kama for example, nakupa mfano, mimi ni mlemavu lakini hauwezi kujua kama mimi ni mlemavu. Nimeambiwa na daktari nitaishi kwa madawa tangu nimemaliza shule kulingana na mishipa vile ilikutwa wakati, wowote unakuta mtu anazimia. Lakini sasa unakuta kwamba every time I'm working with the government, lakini sasa ukikaa na ma officer wale unadharaurliwa. Hiyo ndiyo kitu tulikuwa tunauliza sasa zamani sisi walemavu tutakuja kutambulikana lini?

Sasa ni kiguru naye anadhalauriwa atawezaje kusimama. Hata pengine amefanya interview lakini atadhalauriwa kwa sababu kulingana na ile ameonekana somewhere short hawezi kufanya ile kazi. Anawachiwa na utakuta mtu atawekwa ambapo hana education yoyote na yule ambaye amemshinda na yule mtu pengine ni wa form six (6) na anawachwa. Hiyo tungetaka serikali kama kweli ni Katiba iangalie watu kama hao kwani hata ikiwa DO ni mlemavu na anazungumza na yuko sawasawa nafikiri anaongoza watu maanake akiketi kwenye kiti kama hapo juu anaweza akazungumzia tumikutano na akafanya.

Mengine ningesema ni kwa upande huu wa mambo ya matibabu. Mlemavu atapata wapi pesa za kwenda kutibiwa? 1980s mpaka 1992 walemavu walikuwa wanatibiwa bure, lakini since mambo yalianza multipary hii, tayari mambo yalibadilika na ikawa mlemavu lazima atafute pesa ndiyo aweze kutibiwa. Kshs. 1,000 nitaipata wapi na mimi sifanyi na siwezi kazi yeyote? Hiyo nayo tunataka Katiba kama itarundisha hicho kifungu, mlemavu aweze kuaguliwa kwenye hospitali vile vile aandikiwe dawa na awekewe sahihi na apewe dawa. Maana kama tutafanya waachiliwe hivyo hivyo watakwisha wote.

Nilikuwa na watoto wanaosoma shule hata mwingine angekuwa anamaliza form 4 kwa sasa. Lakini nimefika kwa serikali nataka msaada unakuta hujaliwi kama ile msaada tunayeomba. Hata sasa mtoto yuko nje angekuwa anaanza secondary school, sasa unakuta kwamba huyu mlemavu hizi pesa atazipata wapi? Je, kama mlemavu hamuwezi kumsaidia na amefanya bidii mpaka amepata mtu ambaye ataweza serikali mbeleni je itakuwaje? Sasa tulikuwa tunatakikana walemavu kama tutakosekana kuonekana uso wetu na tutambulikane, na hata kama ni kwenye ofisi tufanye kazi nafikiri tungejua kweli tuna serikali Kenya na tungekuwa tunakaa sawa sawa. Na hiyo Katiba tungekuwa tungejua kwamba inabeba watu sawa sawa maana hatuna uwezo wowote. Lakini kuna mtu amesoma na kuna kazi anaweza kufanya kwa masomo yake lakini utadhalauriwa kwa yale maumbile uliyoko naye. Mimi sina mengi ni hayo tu. Ni ule uchungu tu wa walemavu vile tunavyofanywa na ile madharau tunayedharauliwa. Kama watu wataendelea kukaa tutazidi kuzungumza mengine zaidi. Sina mengi.

**Com. Abubakar:** Asante Bwana Mwakirenge. Tungemuomba Joseph Mwawazi. Bwana Mwakirenge sign register. Joseph Mwawazi.

**Joseph:** Commissioners wetu na wananchi wote, jambo ambalo ningeliweza kuzungumza ni mawili ama matatu hivi. Jambo la kwanza ni juu ya majimbo. Nasikia macommissioners walipokuwa huko Central Province majimbo yalikataliwa. Tunaelewa kwa nini yalikataliwa huko. Kwa sababu kule kwao walikuwa wameishi kama jimbo na rasilimali zote walikuwa wanazicontrol

kule. Na ilikuwa ngumu sana watu wa nje ya Kenya kupenetrate kuingia kule ndani. Na kusema hatutaki majimbo ni kusema kwamba hawataki sisi tuwe na majimbo yetu. Kwa hivyo sisi tunataka tuwe na majimbo. Angalieni kwamba kule Central ya Kenya kuna zile tunaita volcanic soil, wana pareto, wana chai, wana kahawa zote ninaingia mfukoni kwao. Sisi hapa rasilimali zetu ni buga za wanyama, beaches zetu hapa coast na ruins za zamani. Hizo ndizo rasilimali zetu. Lakini tunaambiwa rasilimali hizi zote zaenda Central Government. Sasa sisi tutapata nini? Tunataka zile rasilimali zetu hizi zote ziingie mfukoni mwetu kama zinavyoingia kwao zile rasilimali zao zinaingia kwao. Jambo la majimbo si jambo sasa la kuzungumzwa ati argument zozote ni jambo la lazima. Na mimi nafikiri jambo la majimbo liingizwe Katiba hii inandikwa. Iandikwe Katiba ya majimbo. Nafikiri kama si majimbo hakutakuwa na amani katika nchi hii yetu. Sisi tunataka nasi tuenjoy rasilimali zetu hilo ni jambo la majimbo.

Jambo lingine ambalo nataka kuzungumzia limezungumswa sana na watu linaloitwa Presidential powers. Presidential powers zimesemekana kwamba President ana powers mingi na nini na nini. Ni kweli sioni sababu yeyote rais kuwa mkuu wa chuo kikuu na yeye mwenyewe hawezi kufundisha wala haingii kule. Vitu kama hivyo vinaweza kuondolewa, lakini Rais akose kuwa na power ya kumchagua mkuu wa majeshi? Huyo ni Rais wa namna gani? Hapa kwetu Kenya kuna magonjwa mawili, matatu. Ukabila – tribalism, hapa kuna chuki – hatred, kuna madharauliano. Sasa mimi nimemchagua Rais halafu mnaniwekea, makabila yetu hayapendani. Mnaniwekea mtu ati anachaguliwa Vice President wangu. Nikiangalia siwezi kufuatana na yeye kwa kweli mimi nitasuza mkono wa Kenya chagueni Rais mpya. Mchague Rais mwingine kwa sababu huyu sitaweza kukaa naye. Tumeona miaka hii iliopita 83, 84 tulikuwa na problem ya mzee Njonjo. Tukaona madhambi alikuwa anayoplan against the government. Sasa kama ni Rais lazima apewe jukumu la kuchagua makamu wake, jukumu la kuchagua Major General, Police Commissioner na watu kama hao. Otherwise tutakuwa tunachagua, tunaandika Katiba ambayo itafanya Kenya iweze kutawalika. Kwa hivyo powers za President Katiba imake sure kwamba nchi hii itaweza kutawalika. Maana Rais kama hawezi kuchagua watu kama hawa ambao wako karibu karibu naye, cabinet yake, nchi hii inaweza kutumbukia katika janga. Upande mwingine ni nchi ya Kenya hii. Uganda 1966 kulikuwa Rais ni Kabaka, Waziri Mkuu Obote. Makabila haya ya lango na Baganda hawabatani. Kabaka akaanza kumchiba Obote. Obote akagundua. Obote akapeleka majeshi katika palace ya Kabaka bahati Kabaka ananusurika. Kabaka akatoroka akaenda London akafa huko. Katiba Obote alisema, "this is a piece of paper". Akaiweka huko. Kama hapa Kenya, mkiandika Katiba ambaye haiwezekani mimi Rais kuchagua watu wangu, atatokea mtu mmoja atakayesema, "this is a piece of paper throw it let me rule by decree." Hilo ni jambo la presidential powers.

Haya na mengine, other grievances nimesema: Wamasaai walifanya mapatano na Waingereza, Lenana 1904 and 1911. Lenana na British, Wamasaai na British government world power and a village chief. Ni kitu gani hii? Mapatano gani haya? Mapatano haya yafutwe. Hakuna mapatano ya mtu mkubwa na katoto kadogo ka kuzaliwa jana. Lenana hakuwa na powers zozote. Angalikataa aje? Angalifanya nini? Waingereza wangalileta Lenana mwingine, kwa hivyo mapatano kama hayo yatupiliwe mbali.

Lingine ni Mazrui land. Mazrui walipatana na Waingereza kuchukua hilo land Malindi. Waingereza hawako. Mazrui ni wa

Kenya kama sisi. Sasa haya mapatano yatupiliwe mbali. Wangiriama kule ni masqutter. "Squatterism" Kenya should go, "landlordism" in Kenya should go. Wafransa walipopindua serikali ya kwao 200 years ago "landlordism" went and it is never there. Kwa hivyo "landlordism" in Kenya should go. Wamazrui ni wa Kenya kama sisi, wagaawanye ile nchi upande, upande kila mtu Mngiriama, mazrui, nani, apate land. Halafu kuna hii mapatano ya mwambao. The Colonial Secretary arrived in Nairobi and announced that the Coastal Strip will belong to Kenya officially after compensation with the Sultan of Zanzibar. Haya yalikwisha bona tuyajazungumzia? It was in 1963, March 4th ndio alikuja mkubwa wa Uingereza, katika serikali ya Waingereza colonial secretary. Sasa hebu tuyazungumze hayo. Mwambao ulikwenda na ukaenda for ever. Halafu kuna haya mashamba makubwa makubwa ya taifa yetu. Tunasikia yanaanza kuchukuliwa na watu wengine Taita Taveta, sijui nani huko, Mwatate. We were told katika hizi civic education classes by the leaders. Halafu wakatuambia mambo ya kushangaza sana ati kuna Estate moja ati Mwatate inamilikiwa na mama mmoja anaitwa Beth Mugo. Sasa wazungu wanaenda, wengine wazungu weusi wanaingia. Jambo gani hii? Mzungu ataweza kwenda kabisa lakini Muafrika hawezi kwenda. Tutakaa hapa milele. Sasa ndio tutakaa hapa for ever and ever as squartters. Sasa hio ni jambo gani hio? Taveta central sisal, inamilikiwa na Criticosna yeye alikwenda kwenda zake. Iko kampuni naambiwa inamilikiwa na mama Ngina haya ni mambo gani? Kwa hivyo hayo ndio mambo ambayo ningetaka kuyasema Katiba iyafute.

Halafu kuna hizi leases za miaka 99 miaka 999, zote ziende hatutaki kusikia mambo kama hayo. Nani ataweza kungojea miaka 999 utakaa wapi? Hivyo ni vigumu kufuata, hata watakapokuja wataona hawa watu walikuwa wajinga. Kwa nini walikubaliana na watu hawa kuishi kama hivyo? Mapatano hayo yamalizike kupitia Katiba. Halafu kuna watu fulani fulani walichukua plots na ardhi. Mapatano hayo jinsi walivyochukua plot hizo, jinsi walivyochukua ardhi hizo ati wenyenji hawajui, tafadhali Katiba iandikwe ardhi hio kama ni Wataita waulize, "ee Bwana ulipataje hapa? Ulipataje hii? Hii kutoka hapa mpaka huo nikwako, ulipata namna gani hii?" Tunataka mambo kama hayo yafutwe na yachunguzwe watu hawa waulize, ulipata je? Yafutwe kabisa.

Halafu mwisho kabisa nasema all government officials should declare their wealth. Kumma watu ambao wamepata madaraka makubwa makubwa. Mbele hawajapewa madaraka waulizwe Bwana una property gani? Wewe una nyumba kule, mashamba kule iandikwe chini. Maana kuna watu wengine wameingia serikalini, madaraka makubwa makubwa 2 years ago leo ni billionairess, vipi, na msahara wake unanjua shilingi Kshs50,000. Ni Kshs.50,000 x 12 x 2 miaka miwili, haziwezi kufika billion, lakini utamkuta mtu kama huyu ana mabillion angepata aje? Kwa hivyo watu hawa wadeclare their wealth before they get these jobs. Haya tu macommissioners wetu.

**Com. Abubakar:** Asante mzee Mwawasi. Fursa hii tungependa kumpa Joseph Mwagogo.

**Joseph Mwagogo:** Bwana commissioner, wananchi na nyote mlioko, hamjambo? Lengo la kutoa maoni haya ni juu yetu sisi walemavu. Swala la walemavu kumekuwa kama wananchi wengine wamepata uhuru lakini mlemavu bando hajapata uhuru. Jambo la kwanza kijamii tumesahaulika, kidini tumesahaulika na kielimu pia tumesahaulika. Neno la kwanza nasema Mungu

hana upendeleo kwa kila mchae hukubaliwa na yeye. Naongea kwa niamba ya kidini. Kuna baadhi ya walemavu wana vipawa vyao tofauti. Lakini kwa sababu yeye ni mlemavu kinavyoinuka kinakanyangiwa na viongozi wa ndini. Anaambia huyu mlemavu ni punguani, ama huyu ni kiwete. Jambo lingine kuhusu swala la walemavu. Nataka jambo hili lichunguzwe sana linanitia uchungu. Walemavu wengi wamefichwa, hawasomi. Nilikuwa naongea na mbaathi ya mmoja kule Mwatate nikamuonea huruma mpaka nikasikia kulia. Ananiambia anataka kwenda shule lakini mama hataki. Jambo hili tafadhali Katiba hii iangalie uhuru wa walemavu.

Jambo la tatu naongea sisi walemavu juu ya msaada. Hatutaki msaada wa walemavu upitie kwa DC ama kwa DO, direct. Kwa nini? Kwa sababu ukianzia (wacha nimtumie mzee wangu Mwangeka) kwa Mwangeka uje na uje kwa mzee wangu huyu kabla haujafika kwangu, kama ilikuwa ni shilingi 20 mimi nitapata shilingi mbili.

Jambo la nne. Walemavu tuwe na mambo ya kujisimamia sisi wenyewe. Twende Bunge kama wananchi wengine, tuwe na machief walemavu, wanaosimamia kwa mambo ya ulemavu. Tuwe na viongozi wa kidini walemavu. Pia tuajiriwe kazi kama walemavu. Kuna kazi ya walemavu nikasema lakini kwa vile mimi nikipovu sioni. Nikienda kuuliza kazi kwa Bwana Mwageka ataniambia "kwenda huko kipovu". Imagine angeniandika ata kama ni kuokota karatasi ningepata shilingi 20 ningenunulia watoto wangu ungaImebaki sisi kusema saidia maskini na mimi si maskini, mtu aliye na akili si maskini. Kwa hivyo jambo kama hilo walemavu lichunguzwe sana sana. Maana sisi bado hatujapata uhuru. Kwa hivyo mimi nasema mpiganie uhuru kwa walemavu. Kweli tumekuwa kama watumwa kijamii naongea ukweli maImaam wanapokuwa msikitini fundisheni watu, mtu mlemavu achukuliwe sawa na mwingine. Yule aliyeniumba mimi mlemavu ndiye aliumba wewe sawa. Na unapoishi kwako Mungu amekuumba waweza kuwa kama mimi. Jambo lingine ni mahoteli ya ngazi. Sisi walemavu hatuwezi panda kama steps hiyo mambo iangaliwe ya steps. Elimu tuwe tunafundisha watoto wetu free of charge. Kama sina nguvu matibabu yaangaliwe yawe free. Pia kwa usafiri tuangaliwe pia, mlemavu aangaliwe kwa mambo hayo. Asanteni.

**Com. Abubakar:** Asante sana Joseph. Asante sana. Bwana Geoffrey Mwajuru.

**Geoffrey Mwajuru:** Natoa shukrani kwa commissioners kwa kunipatia nafasi hii ya kuweza kutoa maoni yangu. Kwanza nitaanza kutoa maoni kuhusu biashara. Biashara nitasema kwamba ikiwa itakuwa ni sawa kwenye Katiba iorodheshwe ili serikali za wiraya ama councils ziweze kutofautisha mahali ambapo biashara ziko. Kama saa hizi kuna kitu kunaitwa business permit. Business permit iko general haijalishi mtu yuko katika position gani. Watu wengine wanaadhirika kwani maduka yao yako dani dani. Kwa hivyo kwa sababu duka lake haliko katika barabara ambako labda anapata wateja wengi yuko disadvantaged. Kwa hivyo afikiliwe labda Katiba hii kwamba mahali biashara yake ilipo labda hio liceni yake iwe tofauti. Halafu kitu kingine ni kwamba mashirika ambayo hayamsaidii mfanyi biashara kwa lolote ikiwezekana Katiba iyafutilie mbali.

Nitasema kuhusu dairy board. Mimi ni mfanyi kazi wa biashara ya maziwa. Na dairy hoard inatucharge licence kubwa sana kwa mfano utalipa shilingi 2,000 kwa mwaka na charges zingine cess na mambo kama hayo. Na dairy board haikusaidii na

chochote, hata ngunia ya makaa, hata mkebe wa makaa haiwezi kukusaidia nao. Kwa hivyo hatujui hio pesa wakichukua inafanya nini kwa sababu unajua kwamba ikiwa kuna shirika ambazo sitachukua pesa za wafanyi biashara, lazima nipate kitu in return.

Upande wa siasa ni kwamba tunahitaji siasa ya majimbo. Hatuwezi kujidanganya kwamba Kenya hii tuko katika hali sawa. Hio ni kusema uongo. Kenya hii tunahitaji majimbo. Hata kama hatutaanza majimbo vile inatakikana katika boundaries lakini wakati huu tuanze ile tunaita, mimi si msomi sana lakini nisa sikia wakisema, ile tunaita majimbo ya kiuchumi. Zile raslimali sinatoka hapa zianze kutumiwa hapa hapa ili zinufaishe mtu ambao anakaa mahali hapa.

Upande wa afya nitaomba kwamba vile ambavyo uongozi unatambazwa siku hizi tunatambaza uongozi sana. MaDC tunawapeleka karibu, district zinaongezeka, machief location zinapanuliwa lakini utakuta dispensary ni ile ile moja. Kwa mfano mahali hapa nakaa kunaitwa Mzwanini. Watu wa pale inabidi watoke Mzwanini waende mahali panaitwa Mpizini ama Msau ama waje mpaka Voi. Wakati chief amekuja pale karibu na kuna ingine inakuja karibu inakuja pale karibu. Ningomba kwamba hudumma zile za mhimu ambazo zitasaidia wananchi ziletwe karibu na wananchi.

Upande wa ardhi – ningeomba kwamba iingie katika Katiba kwamba wale ambao hawana uwezo wa kwenendeleza ardhi zao lakini wako na ardhi, serikali iwasaidie hata kwa loan. Mahali kama hapa Voi tuko katika position nzuri sana ya watu ambao wanaweza kujiendeleza kupitisha kwa nyumba za kukodisha. Kuna mahirika kama national housing company na HFCK kama yako, badala ya kwamba wanachagua mahali pa kupeana hizi loans hata mahali kama hapa waje waangalie mtu huyu ana ardhi lakini hana uwezo wakuendeleza hii ardhi yake. Basi asaidiwe hata kama apewe loan anjenge nyumba yake halafu ile nyumba kiasi fulani cha nyumba kikatwe kiende kwa kulipa ile loan na kiasi kingine ambaki nacho mwenyewe ili kusudi ile ardhi isipotee.

Kielimu nitaomba kwamba elimu iwe ya bure, tena isiwe ya mzigo kama ya 8-4-4 vile inasubua wakati huu. Twaomba elimu ichunguzwe zaidi na iwe ni ya bure. Nikiendelea kummaliza nitaongea kuhusu wana michezo. Mimi ni mwana mchezo nimekuwa nikipiga mpira kwa miaka mingi. Lakini kuna wachezaji wengine ambao tunawahurumia. Kwa mfano hapa Voi tulikuwa na kijana ambae ni malehemu sasa, alikuwa akiitwa Morris Godwin, amecheza mpaka team ya taifa. Lakini nitasema wanamichezo Kenya hii hawangaliwi. Mchezaji anakwenda anapeperusha bendera ya Kenya, wimbo wa taifa unapigwa, watu wanashangilia lakini mwisho akishaumia akitoka, naye pia ametoka ameenda kabisa. Naomba iwe katika sheria kwamba wana michezo washuhurikiwe hasa ambao wamefika kiwango cha taifa kwa sababu wamebemba nchi hii mahali pakubwa sana.

Kazi za kujitolea – Naomba kwamba kazi za kujitolea wazee wa mitaa ikiwezekana wafikiliwe. Nilisikia Bunge likizungumza kuhuzu haya wakataa kabisa wazee wa mtaa hawatakikani kushuhulikiwa. Lakini nauliza, ikiwa wale ambao wanaonekana kwamba wanastahili kutumia pesa za serikali na wenyewe wanaziharibu ama wanasivuja, misappropriation of funds inafanywa. Kwa nini mzee wa mtaa ambae anajitolea kupiga vilimbi asipewe chochote ili kusudi kumpatia mwingine ile kazi? Hio iingizwe katika Katiba.

Mwisho ama ili kabla sijafika mwisho, mahitaji kama barabara na simu na sitima yasiwe yakujadiliwa. Barabara iangaliwe kwamba barabara haifai itengenezwe. Mahali pengine tunasikia barabara inatengenezwa lakini zinaanikiwa mahindi. Kwa mfano tunasikia mambo kama hayo ingawa mimi sijaona lakini tunasikia hivyo. Na kuna mahali pengine barabara hakuna kabisa. Tunaomba mambo kama haya yaingizwe kwenye Katiba kwamba barabara isiwe jambo la kujadiliwa. Ikiwa inaonekana kwamba barabara insaidia watu na inastahili kutengenezwa, itengenezwe.

Mwisho kabisa ni mambo ya kidini. Mimi ni muhudumu, muinjiristi na ningekua na maoni haya yaingizwe katika Katiba ikiwa itawezekana. Iwe ni hatua ya kisheria ikiwa mtu atasimama anahubiri dini yake na huku anashaburia dini ya mwingine. Nasema hivyo kwa sababu uhuru wa dini tunautaka lakini tunataka huu uhuru usilete mfurugano. Tunataka uhuru ambao utakuwa wa amani. Nigeria watu wanauana. Nigeria ni mbali, hapa Kenya South B juzi juzi tulisikia jambo lilijitokezea pale hata makanisa yakaanza kuchomwa. Nataka kusema kwamba chanzo cha haya mambo yote ni kuingiliana. Imani ni jambo la kiroho zote tunalotarajia ambalo hatulioni. Kwa hivyo sioni kwa nini tuingiliane. Kwa hivyo ningependelea jambo kama hilo liwe katika Katiba kwamba mtu yeyote anapoingilia mwenzake imani yake basi iwe ni hatua ya kisheria. Asanteni sana, Mungu awabariki.

**Com. Abubakar:** Asante Bwana Geoffrey Mwajuru. Sign register tafadhali. Yahya Peter.

**Yahya Peter:** Macommissioners wote na wananchi hamjambo? Kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia kufika mahali kama hapa. Katika maoni yangu, au katika mapendekezo yangu. Hususa ninapenda kuongea kuhusu ardhi. Anayepasa kumiliki ardhi ni jamii ya mahali pale. Hapo tayari ina maana ya majimbo. Anayepasa kumiliki ardhi ni jamii ya mahali pale. Halafu sasa tunataka kuuliza swali, ikiwa sisi tunasemekana tuna uhuru huo uhuru sisi hatuoni kwa sababu mipaka ya ukoroni ni ile ile. Mipaka ilioachwa na mkoroni ni ile ile. Huku tunadai ati sisi wakenya tuna uhuru, uhuru gani? Ndio tunasema, raslimali zetu sisi tusimiliki sisi wenyewe. Tukiangalia wanyama wa buga wanamilikiwa na serikali. Kuna kitu kinaingia kama watalii wakija katika sehemu ya Taita Taveta. Kuna kitu wanatoa? Hakuna. Bona sisi mahindi yakiliwa na ndovu ukipiga report hutaona yeyote. Hutaona hata baiskeli ikija kuangalia haya mahindi lakini sikiza wapate report kuwa ndovu tu ameguzwa. Kwa hivyo tunaona hii serikali yetu masilahi sana inaangalia wanyama haiangali wananchi. Na kama inaangalia wananchi inaangalia upande fulani haingalii upande wote kwa sababu mimi natoka katika Taita natoka mahali panaitwa Kasigala mahali pana ndovu mingi sana.

Kwa hivyo tunaona ndovu kama hawa wakiingia shambani hakuna hatua yoyote itachukuliwa. Lakini ndovu moja tu aguzwe, ndege zitakuja, magari yatajazwa petroli na kuja na viumma. Vipi? Ina maana ndovu na mwanadamu ni nani mkubwa? Ni nani mwenye kupata kulindwa sawa sawa? Kwa hivyo hawa wanyama kwanza Mwenyezi Mungu ametuubia sisi si kwa manufaa ya mtu binafsi. Hizi wanyama wa poli mimi nataka raslimali zetu tusimiliki sisi wenyewe. Nikisema hivyo nakusudia ndovu na wanyama wengine. Kwa nini tusuiliwe kura wanyama wa poli, na hawa Mwenyezi Mungu ametuubia sisi? Tena nyinyi mmechukua jukumu ya kuwalinda bona msiwalide kisawasawa? Na kile kitu kinachoingia katika hawa watalii wanakuja

kuangalia bona kitu kile kikiingia kama mimi shamba yangu imeliwa na ndovu bona msije mkanipiga kitu? Kuwa Bwana umeliwa na hizi ndovu, hizi ndovu sinaingiza kitu. Watalii wanakuja kuziangalia ndio tunasema mzifanye kitu. Bona hizo pesa zitumike katika area hio? Ati mtu wako akauliwa na ndovu unapewa 50,000, inatosha hio ndugu zanguni?

Kwa hivyo tunataka lazirimali zetu sisi kama wana wa Kenya kama kweli tuna uhuru na hii mipaka ya kikoroni ziondolewe. Na ikiwa kama kweli sisi tuna uhuru, basi hizi mipaka za kikoroni ziondolewe na lazirimali zetu tuzimiliki sisi wenyewe kwa sababu tunaona hapo wanashindwa. Kwa sababu kama kweli wanaweza ingalikuwa hakuna kusubuliwa na hawa wanyama. Kwa hivyo wanyama wetu tuwamiliki sisi wenyewe. Tuamue tutawapiga mishare, tutawafanya nini, tujue sisi wenyewe. Tuamue tutakuwa na council yetu wenyewe watalii wakija wanaandikisha kila kitu tunaona sisi wenyewe. Mambo ya kumilikiwa na watu wengine yanakuwa ni manufaa kwa watu wengine na Mwenyezi Mungu ametuubia sisi wenyewe hawa wanyama. Kwa hivyo mimi singekua niende mbali sana na la mwisho nilikuwa nataka kuchangia uhuru wa dini. Tunataka uhuru wa dini sio uhuru wa kuabudu. Uhuru wa kuabudu na uhuru wa kidini. Kwa hayo machache nitakwamia hapo.

**Com. Abubakar:** Asante sana Yahya. Tunamuita Hassan Kassim.

**Hassan Kassim:** Salaam aleykum. Natoa shukrani kwa zote tuliohudhuria hapa na yangu nitakayoyasema au maoni yangu juu ya marekebisho ya Katiba ni kuweko uhuru wa dini. Kwa hakika nataka iwe wazi kwa wote kwamba uhuru wa dini ni kipawa ametoa Mwenyezi Mungu. Ni makosa kudai kwamba serikali imetoa uhuru wa dini. Bali uhuru wa dini aliyetoa ni Mwenyezi Mungu. Ni juu ya serikali kulinda kwa kila mmoja manake juu ya dini yake alindwe lakini sio serikali ati ametoa uhuru wa dini. Bali serikali yenyewe inakuwa ni dini.

Jambo lingine kwenye msikiti wowote pasiwe karibu yake na bar, sehemu ya kunyua pombe. Au penye karibu ya kanisa yote pasiwe na bar bali ipige marufuku bar zote kama alivyopiga marufuku Mwenyesi Mungu. Na Mwenyezi Mungu hataki mambo ya upuzi ya ulevi aliharamisha.

Jambo lingine ni kuhusu Kadhi. Chief Kadhi yatakikana achaguliwe na Waislamu. Asichaguliwe na serikali kwa sababu akichaguliwa na serikali yu atumikia serikali. Yatakikana achaguliwe na Waislamu awatumikie Waislamu. Ajue matatizo ya Waislamu apeleke mbele. Vile vile ofisi ya Chief Kadhi iwe na uwezo ya kummaliza matatizo ya Waislamu hapo hapo. Vile vile ofisi ya Chief Kadhi ihukumu kwa kitabu cha Mungu na shuna sio kwa raiya. Yangu ni hayo tu, natoa shukrani. Asante.

**Com. Abubakar:** Asante sana Hassan Kassim. Ningetaka kutoa fursa hii kwa mheshimiwa Mwakiringo mbunge wetu hapa apate fursa na yeye azungumze.

**Mheshimiwa Mwakiringo:** Asante commissioner. Nilikuwa nafikiria nitazungumza mwizo lakini nadhani hivyo.

**Com. Abubakar:** Ikiwa wapenda hivyo mheshimiwa nitakupa fursa hio.

**Mheshimiwa Mwakiringo:** Nadhania. Yeah.

**Com. Abubakar:** Asante kwa kuelewa mambo haya. Anayefuata ni Swaleh Mwauganga.

**Swaleh:** Shukrani macommissioner wetu karibuni sana. Tumeshukuru kwa kuja kututembelea na wananchi akina mama na akina baba hamjambo? Mimi natoa shukrani hii kwanza kwa serikali yetu tukufu iliyetuletea hafla hii ili tutoe maoni yetu. Ya kwanza nikianza nasema ya kwamba kusema kweli katika nchi yetu ya Kenya uhuru umetolewa nusu nusu. Kwingine kamili kwingine iko nusu. Kama hivi hapa kwetu Taita Taveta tuna shida na matatizo kuhusu ardhi. Nikisema kwa ukweli kwamba maoni yangu uchungu wa mwana ajuae ni mzazi. Boma la mtu ajuaye shinda yake ni mwenye boma. Leo sisi nashangaa hapa kwetu Taita kuwekewa chairman wa ardhi kuwa ni mtu wa kutoka nje, hajui mipaka ya Taita, hajui mila za Taita. Hili jambo limetunyanyasa tena sana sana. Ningeomba Katiba hii, chairman wa ardhi ya nchi kama ni Taita Taveta, ni Kisumu achaguliwe na wazalendo wenyewe. Kama hapa kamati za wazee zichague kiongozi wao atakuwa nani kuwa mwenye kiti wa Taita Taveta watajatejywa na imani naye.

Pili tunasema tunataka serikali ya majimbo. Serikali ya majimbo ndio itatuokoa sisi kwa Pwani. Kusema kweli watu wa Pwani ni watu wanyenyekevu, watu wapole ulimwengu unajua na serikali pia inajua. Lakini kwa wakati huu pamefikia pahali pabaya. Kwanza huyu mwenye kiti wa Taita Taveta district ametunyanyasa, ametusukumma hivi sasa katika miezi hii miwili, mitatu ametuchukua vibaya vibaya ametufanya kama mifugo, hata kutufungia mapenzi katika milango yetu hatuna njia. Wengine wanafanyiwa less business. Sisi hatutakubali. Hatutaki moral, hatutaki gold lakini sasa tuamwambia huyu chairman wa ardhi awache kucheza na ardhi ya wa Taita. Ardhi iliobaki ni ya wajukuu zetu na watoto wetu. Hakuna kitu cha kusema amekuja na barua zake kutoka Nairobi huko kunakotoka barua hizo apatikane ardhi huko. Ardhi iliobaki Taita ni ya wataita na wajukuu zao na watoto wao. Tunaomba tafadhalini, tena mimi nasema kwa uchungu vile tunaviotawaliwa tunatawalwa kama wanyama wa polini. Huyu chairman wa ardhi ya Taita Taveta ana vibaraka wake watatu wanne ndio wanamuongoza. Wajue hawa watu mmoja ni mimi ninasema sina imani na wao. Sina imani na wao manaake hatujui watoto wetu watakuja ingia wapi. Sisi wenyewe tumebaki hata kunyanganywa bedroom manake unakuja na mtu anakuambia hapa ni kwangu, toka. Sasa unashindwa utakwenda wapi. Ukiangalia kaburi la babako liko pale nje, familia yako ulizika pale. Leo waambiwa uondoke hii ni ya Oloo, hii ni ya Wainaina sisi watu wa Pwani tutanyanyaswa mpaka lini? Twaomba Katiba hii iwe ya majimbo. Kwanza lazirimali zetu zitusaidie wenyewe. Kwani tena tunandanganywa Mombasa city, Mombasa inakuwa city, city gani haina university hata moja? Ni kitu gani mwatundanganya? Mwatundanganya ndanganya namna hii.

Watoto wetu hawajiliwi kazi katika buga za wanyama na buga za wanyama hizi ni buga zetu. Kitu tunakataa hatutaki kusikia masquatter. Babu zetu walikuwa wakiishi bila jina squatter, hatutaki squatter. Wenyewe wazee wanajua tutakuwa kukijipimia wenyewe na kumiliki raslimali zetu zote irudi mkononi mwetu. Tafadhalini mimi nilikwisha tumma maombi ya kuandika lakini

haya nayatoa kwa uchungu.  Pale alipo huyo mwenye kiti ya ardhi ya Taita ajue Wataita wote hawana imani na yeye. Anatuchukua vibaya na hata mimi mwenyewe sipati uzingizi wala silali.  Lakini Bwana watume commissioner, mwende muambie kule watu wa Taita Taveta tunatawaliwa sijui mapresident ni wangapi Kenya.  96 Rais Moi alicancel utoaji wa ardhi, na 99 akauda commission ya Njonjo.  Majimbo hatujarekezewa huku tunaabiwa kila ardhi yeyote isiguzwe ikae hivyo hivyo mpaka Njonjo atakapolegeza majibu kwa kila mkoa kwa kila wilaya.  Na huyu President wa Taita Taveta district anayetoa ardhi usiku na mchana ni yupi?  Tunauliza, twataka tunjue President gani.  Kama tuna President wawili tuelewe, kama President ni mmoja tafadhali huyo mwenye kusimamia ardhi hii na watu wake walanguzi wake wakome. Ama si hivyo Taita itachafuka maanake kusema kweli tumestahamili na sasa tumefika ukingoni, tumesukumwa mpaka kwenye ukuta.  Sasa tutatia guu kulegesa nyumma tujikomboe.  Kwa hivyo sina mengi zaidi, ni hayo tu niliyosema.  Asanteni.

**Com. Abubakar:**   Asante sana Bwana Swaleh.  Bwana Swaleh tafadhali uje uandike kwenye register kwamba umetoa maoni.  Asante sana.  Ndugu zangu, nadhani mambo haya yana hamasali si vibaya kuona lakini nyinyi mkishangilia sana mtamzuia fursa ya kuzungumza vizuri.  Mwacheni atoe hamasa zake kwa undani wake lakini tumpe fursa nzuri ya kuzungumza.  Au sivyo?  Au si sawa hivyo?  (Sawa)  Naomba Bwana Mutula ndiye anafuatia.  Ameandika kwamba anatoa written.  Bwana Mutula tafadhali.

**Mutula:**  Commissioners, participants

**Com. Abubakar:**  Bwana Mutula ningeomba kila mtu akija hapa aseme jina lake ndio turi-record maanake ni Mula P.M. Asante.

**Mutula:**  Okey.  Commissioners, participants nawasalimia nyote.  Hamjambo?  Contribution zangu nimeandika lakini nitaeleza kwa kifupi halafu nipeane.  Jambo la kwanza ni issue ya 85% selection criteria ya secondary schools.  Mnajua ya kwamba kila secondary school ya provincial level huwa inachukua 75% ya wanafunzi katika mkoa huo wa hio shule.  Mimi kwa upande wangu nimeona ya kwamba 85% selection rule haidumu vizuri kwa wananchi.  Maanake wengi wetu wale tulisoma na ile system ya mbeleni ilikuwa ni miaka 7 – primary, 4 – secondary, na ingine 2 – A level, na university miaka 3.  Tulikuwa tunaenda mahali popote nchini na unasoma unarudi nyumbani na barua yako.  Shule zilikuwako nzuri na baya kila mkoa lakini kulingana na bidii ya mwanafunzi ulikuwa unaenda ile shule unafikiria ya kwamba itakuhundumia vizuri na tuifaulu.  Hivi utaona mwanafunzi mzuri kabisa amekuwa confined to ile district yake ambapo zile shule ziko si nzuri sana.  Kwa hivyo kwa bahati baya atafanya vibaya na akose kwenda university.  Kwa hivyo mimi naona ya kwamba hio sheria itupliwe mbali.

Ya pili, nimeangalia mambo ya police na nimeangalia upande wa traffic police.  Najua kila mmoja wenu ashaa tembea na matatu ama na bus na mmeona ile mambo inaendelea huko barabarani.  Kazi ya traffic police mara mingi ni kupokea hata si kuhudumia.  Na mara mingi utaona gari iko na makosa mengi, inapita karibu na polic, police anaangalia anatoa ile (inaudible) halafu anaachilia gari inapita.  Ikifika maubu unasikia ile gari imepata ajali si ilipita police, ile ajali imetokeshea wapi?  Watu

wanaumia. Kwa hivyo mimi nilikuwa naona serikali iangalie mambo ya traffic police na kama itawezekana kama wale watu hawana kazi barabarani, waondolewe. Wawekwe mahali ambapo pengine kuna hatari ya nchi kuangalie gari na kama kuna njia ingine yote ile yakuangalia makosa ya gari isuhulikiwe. Kwa mfano, tunaweza kuwa na regular inspection ambapo gari zitakuwa zikiangaliwa na hudumma za traffic police zipunguze. Na makosa ile itapatikana wakati wa inspection basi ipelekwe kotini. Mara mingi ukikataa kutoa ile hongo ndio utakuta yakwamba umepelekwa kotini na pale unatolewa fine ata kubwa kulingana na ile kosa uko nayo.

Jambo la tatu nimeangalia upande wa Local Government zile tunaita serikali za mikoa. Watu wengi wameongea juu ya majimbo lakini mimi kwa upande wangu huwa ninaona hata heri tuangalie serikali za mikoa ambapo tusipatie sheria kali zaidi, tuzipatie uwezo zaidi ndio zihudumie wananchi. Mtu kama mayor wa mji, ata wale watu tumeketi hapa wengine tukiulizwa mayor wa hapa ni nani pengine hatumjui. Lakini angekuwa ni mtu ako na powers nyingi na anahudumia area yake kulingana na zile powers hakuna mtu hapa hangejua major wa Voi ni nani. Kwa hivyo mimi ningeomba badala ya sheria za majimbo ingawaje hio itakuwa ni majimbo ya aina ingine, serikali za mikoa zipewe powers nyingi. Kulingana na sheria za mkoa basi serikali itaangalia ya kwamba ione budget katika budget ya nchi serikali ya mkoa imepewa kiwango kikubwa ndio isilikie mambo ya development za area hio, wafanyi kazi wa area hio na pia mambo kama ya barabara. Na vile zinasemekana hapa barabara zingine mahali pengine ni nzuri, barabara zingine pahali pengine hazipitiki. Sababu ni gani? Wale watu tuko hapa pengine hatuna uwezo wa kulekebisha zile barabara zetu, uwezo unatokana na zile pesa tuko nazo. Katika hio pia nimeeleza ya kwamba zingependelea watumizi wa serikali kama ni walimu kwa mfano ama civil servants wawe katika chini ya sheria katika serikali ya mkoa. Hao wangewachwa katika serikali hao ni wafanyi kazi wa central government ndio kuwe na ile uniformity. Standards siwe zimekuwa set uniform standards katika nchi nzima. Lakini supervision na management iwe iko chini katika mkoa. Mayor in that case then atakuwa mtu anasikilia si town tu peke yake munciipality basi awe na jukumu hata la kuhusika katika areas zingine zile nje small townships.

La mwisho kabisa nimeangalia sheria za customary laws. Juzi wengi wenu mlisikia mheshimiwa na wale wengine kule Bungeni wakijadiliana mambo ya women rights. Ni jambo ambalo limezungumzwa sana hata kwa magazeti, lakini mimi nikafikilia ya kwamba now we have this issue ya women rights fine. It calls under customary laws. Hapo mbeleni issue za kinyumba zilikuwa zinakaliwa chini na wazee. Na kila jamii iko na mila (inaudible) na cultures zake za kulinda ule mji. Siku hizi hata si ajabu yakwamba utaona mwanamke akikosana na Bwanake pale nyumbani, anampeleka polic. Akimpeleka police yule police yuko pale ni kijana mdogo hata umri wa mtoto wake na huyu ni mzee, mimi nashangaa ni vipi basi mzee atakaliswha chini na mtoto wake mambo ya nyumbani ishuhuhishwe. Yangu ni kwamba ningpenda issues kama hizo za women rights zifall under customary laws. Na customary laws ziwe na powers nyingi kuliko vile ziko siku hizi ndio wazee kule kijijini na mahali pengine kule wawe na jukumu la kukalia chini issues za families na kuzisuluhisa. Maanake mara mingi ikifika police, kama vile nimesema you don’t get any solution unapata hata sinda zaidi. Ikipelekwa kotini na sio ati ninadhalau majudges, utakuta pia yule judge pale ni mdogo kuliko wale wazee amekalisha chini pale. Issues kama zile kama ni mtoto wao atasi-sort namna gani? Kwa hivyo mimi ningependa upande wa customary laws ziongezwe nguvu. Yangu ni hayo, asanteni.

**Com. Abubakar:** Asante sana. Sabili ndugu yangu. Asante sana Bwana Mutula. Commissioner ana swali la kukuuliza.

**Com. Kabira:** Asante sana Mtula. Ningetaka kuuliza swali juu ya customary law na women's right. Kwa sababu womens right ni (inaudible) wanawake wanauliza kwa sababu ya vile wanakaa pamoja na customary law. How can you thn put them back for them to be dealt by customary law which they are running away from?

**Mutula:** Asante. Mimi madam commissioner kitu nitakuambia ni kwamba mimi mambo ya sheria sijui zaidi. Kitu ninachangia ni kwamba ningependa customary laws issues za women rights, children issues and so forth ziwe sana sana zinahuzizwa na mambo ya customary laws. Lakini tukiingia mambo ya sheria basi nitakuambia hapo sina ujuzi zaidi.

**Com. Abubakar:** Bwana Mutula mimi nina swali dogo tu unifafanulie. Unaposema serikali za mikoa, sasa hatuna serikali za mikoa.

**Mutula:** Nafikiria ziko.

**Com. Abubakar:** Nadhani unazungumzia serikali za mitaa. Local Government.

**Mutula:** Sawa.

**Com. Abubakar:** Thank you very much, if you can sign the register. Anaefuatia ni Peter N. Ngoa.

**Peter M. Ngoa:** Nasukulu sana kwa kupata nafasi hii na pia narudisha shuklani kwa wote commissioners na wale waliofika. Mimi yangu ni kuhusu wazazi wa walemvu wa Taita Taveta ama popote pale walipo. Mzazi wa mlemavu yeyote yule ambaye amepata mtoto wa tofauti kwa hali ile yeyote mlemavu, kunamlemavu wa akili, wa viungo na sehemu nyingi. Huwa wazazi wa walemavu wenyewe pia yeye ni kama amelemaa sehemu Fulani ya maisha yake hawezi kuwa mzuri kama yule mtu ambaye ana watoto wakamirifu. Kwa sababu hii, mzazi wa mlemavu kuna walemavu wale wanapiduliwa kwa kitanda kila wakati haondoki, hasimami, hawezi kuketi. Wazazi hawa wakiwa ni wawili sasa itakuwa kila wakati mzazi mmoja akiondoka mwingine aache mwingine akimungojea yule mlemavu mahitaji yake vile ataka. Sasa walemavu wakiwa na shida ile hata wengine mmesikia vyema pia wazazi wa walemavu wako na hio shida. Nakumbuka mimi mwenyewe niko na wao na wakati nilijaribu kutaka kumsaidia ilinichukua zaidi ya miaka mitatu mpaka 1971 ndio akaja akapata shule, akaenda akasoma shule na ni matatizo mengi kuishi na mlemavu. Kuna wale wanasungumza, kuna wale hawazungumzi kabisa hata wazazi wenyewe hawaelewi na mlemavu wao wakiwa wamemzaa wenyewe. Kwa hivyo wazazi wa walemavu popote walipo ni watu wana shida kama yule, vile ukiona nyumba iko na mlmavu dani basi mzazi naye ni kama mlemavu kwa sababu kuna shida nyingi anakabidhi. Hawezi kwenda biashara, yule mlemavu niwakuangalia saa zote. Hawezi kwenda safari ndefu, hawezi kukaa kado kwa nyumba yake kwa mda

mlefu kwa sababu ya kulinda yule mlemavu wake. Kwa hivi ningeuliza kama ingekuwa jambo la kufaa au kama inawezekana yaingizwe katika kwanza, mzazi wa mlemavu pia afikiliwe na aangliwe shida zake kwa sababu mara nyingi wengi wao wanakuwa maskini sana kwa sababu ya kupata hawa watoto. Wengine wako na wawili walemavu dani ya nyumba, kwa hivi inakuwa hawa wazazi ama huo mzazi akiwa na mmoja hana nafasi ya kufanya kazi yeyote ya kumletea mapato popote pale. Sasa atakuwa hategemei popote na mara nyingi wanakuwa kama hawaonekani haza wazazi wa walemavu pamoja na walemavu wao. Hawajulikani mahali walipo kwa sababu hakuna siku zote kamati aina zozote ama utawala wote kutembelea kila district ama location ijue kama kuna walemavu wangapi na wazazi wao wako na shida ya aina ngapi. Kwa hivyo ingekuwa vizuri watabuliwe walemavu shida zao na wazazi wao pia waangliwe kwa sababu wao ndio wako na shida kubwa ya kumlea mlemavu (inaudible) kumpeleka kusoma. Na pengine wazazi wakiwa hawajasoma inawezekana na wao wasimpeleke mtoto wao shuleni. Sasa mzigo unazidi kuwa mkubwa. Hio nyumba itakuwa na ummaskini mpaka mwisho manake dani ya nyumba hakuna mtu aliyesoma katika family. Basi hiyo nyumba ni ya kufanyiwa kibarua miaka yote na watabaki hivyo. Kwa hivyo ingekuwa mzuri katika Katiba inayoandikwa sasa mambo ya walemavu pamoja na wazazi wao yaangaliwe na ifikiliwe vizuri ikiwezekana kuwe na hali ya kwamba walemavu wahesabiwe maanake nakubuka cnsus zilizopita wengi hawakupata kuhesabiwa. Basi wakihesabiwa pia itajulikana pia wazazi wake ni watu wa aina gani ili walemavu waingie kwa kuhesabiwa na pia waonekane wazazi wao aina gani ili kama kuna msaada unaweza kutokezea wasaidiwe wasaidiwe kwa njia yeyote ile. Hio ningefikilia ingekuwa vizuri hivyo, pia niko na la pili.

Ya pili ni kuhusu mambo kutoka kwa kijiji kwenda juu. Katika sehemu zetu tunapoishi hapa Kenya kunao wanitwa wazee wa mtaa. Na hawa wazee wa mtaa kuwa wanachaguliwa tu hivi hivi labda kutoka (inaudible) ofisini kwa chief ama kwa DO pote pale, sasa watu wataanza kijijini wanaomchagua mtu yeyote wanamjua wamekubaliana. Na katika hali hio anapochaguliwa mwenyewe hajajaribu uongozi hata siku moja wala hajakua katika kikudi chaochote kinaongoza. Sasa unakuta hicho kijiji kinakuwa na shida nyingi ambapo yule mzee anawasimamia haendi pamoja na wananchi wake. Ningeliomba kama kutakuwa inawezekana wazee wa mtaa tuwe tuna elimu Fulani inafikiriwa. Kama ndarasa la 7 au 8 iwe kuna kiasi Fulani kinafikiriwa manaake mtu bila kusoma hawezi ongoza mwingine sababu yeye mwenyewe hana uwezowa kuweza kufikilia ataongoza vipi. Kuwe na kiwango cha elimu halafu tena kuwe na mda wa ofisi ikiwa tu ni siku zote kukosana na mwananchi anaenda kumstaki mahali pengine kwa high level huko anakuja ondolewa baada ya wiki kwa sababu amekosea mtu Fulani. Itakuwa hivi si vizuli kwa sababu kama anafanya kazi ya kitaifa anasaidia wananchi pale katika ofisi kwa chief ama kwa sub-chief inakuwa je tena chuki ya watu wawili anaenda kuondolewa anawekwa mwingine . Kuwe na mda wa ofisi wa wazee wa mji. Na pia kuwe na miaka ambayo inakubalika. Sasa kama mzee wa mji atakuwa anakaa miaka 21 katika kijiji kuna watu wana miaka themanini, sabini. Mtu amekosana na familia yake huyo mzee wa miaka 68, miaka 70 anaenda kwa mzee wa mji asubuhi mambo nayo yamekuwa pengine ni mambo ya siri ambaye hangeweza yule ni kama mtoto wake hawezi amueleze. Atawamua vipi? Kwa hivi inaonekana hapo hatuwezi kwenda vizuri. Kuwe na miaka inayofikiliwa kama ni miaka 35 kwenda juu ndio mzee wa mji achaguliwe akioenkana amesoma kiwango Fulani.

Pia mwisho kuwe na kitu chochote kama atahitajika kuendelea kuweko wachaguliwe. Basi kuwe na kiwango Fulani cha pesa

wapatiwe ata nao waweze kujieneza katika familaia zao. Yangu ni hayo, sasa hapo nasukulu, asanteni.

**Com. Abubakar:** Asante sana mzee Ngoa. Anayefuatia ni Bwana Vincent P. Rongo.

**Vincent Rongo:** Morning commissioner and other commissioners. My name is Vincent (inaudible) Rongo. Nazungumza kwa lugha ya Kiswahili kwa sababu tuko Coast province. Ningependelea nikiwa kijana mambo ya vijana kwamba vijana waweze kuangaliwa. Kuangaliwa kwamba sisi wengi tumesoma na wengi ni watu wa sport balibali. Ya pili kwa mambo kwa mambo ya migodi tuna migodi hapa tungependa serikali iweze kutuangalia kwa kazi. Ya tatu kwa mambo ya dini tungependa serikali iweze kuangalia ministry za uijiristi kwa sababu hali inayokuwa ya vijana wengi ni walevi, wengi wanavuta bangi, wengi wako katika hali ya kutumia dawa za kulevia na twaweza kukabiliana na hayo lazima tuweze

**Com. Abubakar:** Kidogo ninaomba munipe fursa tafadhali. Asante.

**Vincent Rongo:** Kukabiliana na hayo natummaini lazima wokovu uweze kuzambaswa kwa nchi.

Ya nne ni kwamba serikali iweze kuangalia vijana kwa uongozi bali bali ya siasa, dini, na akina mama vile, vile kuweza kuangaliwa. Ya tano akina mama kuweza kuangaliwa kwa shuguli zao kwa sababu wengi wanategemea sisi vijana. Waweze kuangaliwa, waweze kuangaliwa maslahi zao na shuguli zao pia. Na sina mengi zaidi ya hayo.

**Com. Abubakar:** Asante Vinvent. Sign register hapo tafadhali. Anayefuatia ni Bwana Joseph Kisa.

**Joseph Kisa:** I am called Joseph Kesa and I think I am going to submit my written proposal. The highlights, for the purpose of identification

**Com. Abubakar:** Just a clarification Kisa. You have a choice to give your memorandum without speaking and you have a choice of giving your memorandum with 5 minutes of giving the highlights. Which of the two would you prefer?

**Joseph Kisa:** Both.

**Com. Abubakar:** You can't do both. What you need to do, listen to me Joseph. If you want to give the highlights go ahead and give the highlights and then hand in your memorandum.

**Joseph Kisa:** Yeah. I want to give the highlights.

**Com. Abubakar:** Okey. Thank you.

**Joseph Kisa:** The first thing I would like to propose is the question of identification. Citizens should provide either of the following documents when they are asked to do so by anybody. They can produce the national identity card, either the birth certificate, the baptism card, if you have a work permit it can function, if you have a passport it is also alright or in some cases you can have academic credentials.

I also want to highlight on Legislature – Actually the legislature has the main responsibility of making laws and formulation of policies for the country. Such a body must have credibility and honour. Therefore people elected or nominated to that house must have certain qualifications. For instance (1) It should composed of men and women. These are Kenyan citizens (2) Persons elected or nominated to Parliament must have the following other qualifications. They must be Kenyan citizens for at least 6 years, must have obtained education to at least form four level or its equivalent, must pass moral examination. What do I mean by moral examination? Today it happens that most of, I would say MPs or rather cabinet ministers attained it through corruption. They have scandals, we have Hon. Ng'eny is having a long running court case, then we have others. Why should they be ministers? Others are war mongers like Hon. Ntimama and yet he works for the President. Why should he be in that office? He should be a village elder but not a minister because he has failed moral qualification to join Parliament.

**Com. Abubakar:** Can I just say this since I am chairing this session. That when you are giving your views, that you cannot make allegations against specific individuals in Kenya who have not been found guilty by a court of law. So please, listen to me. Please confine yourself to your views and do not dismiss other peoples character.

**Joseph Kisa:** Now, I would also like to say that MPs should have a fulltime occupation in Parliament i.e. they should work for 5 days in a week. They should start from 8 a.m. to around 4 p.m. We have had cases whereby the speaker have had to adjourn sittings because there are no MPs in Parliament. Two, they should be entitled to a leave in 12 months actually they should have at least 4 months of rest so that they can consult their constituencies. And then those vying for Parliamentary elections must be aged at least 21 years old while those for the President should be at least 30 years old. Voters during an election should be 18 years old.

Then finally, I would also like to touch on the Bill of rights. All Kenyans must under the Constitution enjoy certain privileges. (1) They should have a right to life. Here I mean the death penalty should be abolished. So they should also have the right to freedom of speech. Just a while ago my freedom of speech has been curtailed. So we are saying freedom of speech, movement, religion etc. They should also have the right to own property anywhere in Kenya, right to education, right to health care, right to legal representation, right to shelter, employment and food. We have always had a complaint against the police. Why should a police arrest an hounourable member of the society, a prominent person. I have a case whereby I would rather say, if you are known you are a civil servant, a business man in a place, or an MP there is no need for a policeman to harass you, beating you up, locking you up without giving you a chance. What they should do, they should only serve you with a

notice that you are required to report at a certain police station because you cannot run away for these minor offences. We have had cases where people have died under police confinment.

I would also like to suggest that conditions in our police cells and remand jails are pathetic and torturous. I would like to suggest that police should be prohibited from harassing suspects, subjecting them to torture or any other maltreatment until such people are proven guilty by the court of law. Once They have been sentenced, these inmates as they are called, should have the following rights: Proper. sanitation, there is food, all the meals breakfast, lunch and super. They should also have normal health care, they have a right to treatment. They should have access to news, like in other countries, they should have a TV in one common area where they can get a brief with the current information. Then I'm sure we have several thousands Kenyans who are not going to present their views to this Commission simply because they have been jailed. Who knows others might have been framed.

Then the inmates should also have better clothing. It is very shameful when you walk about seeing other Kenyans, women and men, walking naked because they are prisoners. What's wrong if you can have a different uniform, a pullover, some shoe, the shirt what's wrong with that? How much would it cost us? There's nothing. We should look into that. They should also have occasional visitation and they can be subjected to reform services.

Let me now talk on land and property right. Or just before that there is a question of information in Kenya. The current Constitution denies Kenyans the right to access true information in the possession of the government or any other agent or organs of the state hence I would like to make the following proposals: Any person can have access to information and under any positions if such a move cannot endanger the state security. Students in schools, colleges and universities must have access to relevant information pertaining to them. We have had cases whereby parents and students have complained that the examination results were doctored but when you want to make a follow up you may be given what these students did. So we want it to be law that if I want to know what I did at school in 1990 or 1963 that information should be available to me. This one will help us to stem off these complaints. I think with that I am grateful. Thank you very much.

**Com. Abubakar:** Thank you Vincent. Please sign the register. You are Joseph Kisa. Thank you Joseph. Iwould just like to make this clarification, that when I told you that you should refrain from making the kind of statement you were making, it was not Joseph, it was not to curtail your freedom. It was to enhance your freedom and the freedom of others. Thank you. Thank you Joseph. The next person is Charles Chai.

**Charles Chai:** Kama mlivyosikia majina yangu naitwa Charles Chai na nimekaa hapa Voi kwa mda wa miaka miwili hivi. Nawasalimu nyote macommissioners na wananchi. Mimi napenda kuongea mambo machache kuhusu hii Katiba yetu ya Kenya. Kwa kweli niko na machungu sana kwa sababu nataka kusema kwamba hii Katiba yetu ya sasa inaonekana kwamba ni kama kuna certain people in this country ambao inawapendelea. Nikisema hivyo simaanishi nina lengo kama ukabila, ama

nini lakini ni vile ninaona. Kwa hivyo ningeomba macommissioners wetu ambao wamekuja hapa kututembelea na kuchukua maoni yetu, especially sisi watu wa Pwani hapa Voi, basi hii Katiba si kwamba hizi sheria ambazo ziko sasa ni mbaya sana. Apana. Hizi sheria zilikuwa za wakoroni lakini kitu ambacho kinatatiza sasa ni how to implement to make sure how these laws are getting implemented.There is no proper supervision at all even if you are going to make a very big book say thousands and thousands of pages, hapo ikiwa serikali ama Katiba haitaidumisha kwamba hizi sheria ambazo tutakwenda kuzipanga leo hii, ama kesho, ama kesho kutwa, ikiwa haitafwatwa kuona inafanya kazi namna gani, it will be nothing.

Na kuna swala la kwamba macommissioners waongezewe mda ili waweze kuitengeneza vizuri hii Katiba. Hapo mimi nakataa. Kwa sababu gani? Hawa watu wamechaguliwa walionekana kwamba wanaweza hii kazi and they are learned people. Highly educated wengine wako na Ph.D, wengine wako na masters, hii Kamati they have been approved hata wananchi tumekubali. Ndio sababu leo tumekuja hapa tupeane maoni yetu. Kwa hivyo hata badala ya pengine wachukue maoni kwa miezi miwili, haya maoni yaweza kuchukuliwa hata kwa mwezi mmoja. Not all the people should give out their views in Kenya so that the present Katiba is going to be completed. No, si lazima kabisa kwa sababu itawesekana je watu wote watoe maoni. Mimi kiviangu ningeonelea hivi, huo mda uliopangwa wa hio Katiba ukaweza kuwa tayari ubaki ule ule. Kwa sababu tumesikia kwamba ni pesa nyingi sana zinatumika katika hio Tume, na serikali tunajua haina pesa. How is it? Hii itakuwa kama misappropriation of funds na serikali iwe tayari. Mimi sipendi kuongea mengi lakini nilikuwa ninataka niongee kuhusu hii kitu tunaita (nimeona katika uongozi wa hii Katiba) tunaita basic humman right yaani haki za kimsingi. Katiba yetu au serikali yetu ya sasa haiangalii kabisa katika haki za kimsingi hata kidogo. Ni yupi anastahili kupewa haki hizi za kimsingi? Vile mimi nasema ni yule mtu anaestahili kupata haki ni nani? Can anybody answer this question?

I'll take it myself. Mtu anaestahili haki hii ya kimsingi. Nataka niongee kwanza kuhusu matitabu haki katika health care. Nimesikia kwamba kuna cost-sharing katika mahospitali. Hii kitu inaua Wakenya kabisa. Ningependa Katiba ambayo tutaiuda saa hii lidhinishe iwe hii health care iwe ni mmoja ya zile haki za kimsingi, iwe itakuwa free kabisa kwa sababu ukisema hii matibabu ya afya itakuwa na pesa hapo ndio wananchi wengi wale wa kawaida wanakufa bure. Utakuta anaplekwa mgonjwa anapelekwa hospitali, daktari hamwangalii kwa sababu hana pesa hata siku hizi hata sijui vile pesa imeadikwa pale ambayo ndio utatoa. Kama wewe huna hongo ukashugulikiwa vizuri, basi mtu wako atakufa pale pale. Manake hawa madaktari hawakubali shilingi thelathini zile zimeandikwa pale ofisini. Utakuta kuna mtu anaingia kule anatoa shilingi mia badala ya shilingi 30. Halafu yule yule ndiye anahudumiwa. Kwa hivyo hakuna haki za kimsingi kabisa hapo.Where is the right there?

Pili tunasema katika maskuli kuna bursary na loan za kuendeleza watoto ambao ni mashujaa ama kama genious hivi lakini wazazi wao hawana pesa. Hapo serikali ninaishukulu sana kwa sababu imeweza kutengeneza bursay na kuna loans. Tukiingia hapo utakuta kuna mtoto fulani wa maskini hapo anastahili kupata hio loan ama bursary. Akaenda kujaza form pale atashugulikiwa vizuri sana lakini in the end hizo pesa hutapata atachukua huyo mtoto wa tajiri ndiye atachukua hio loan ama busary. Sasa what is the rule? There are no basic humman rights there. Sasa na ikiwa serikali imesema kuwe na zile loan na ziwe zikisaidia maskini, sasa what is wrong there? The government is failing to supervise this loans so that they can work

properly. Kwa hivyo tutarudi hapa hapa tena. Katiba hii tunaenda kusahihisa turudishe kipengere kidogo lakini sio kufuta sheria zote. Sheria zingine zimeletwa kutoka juu na Mungu, zile za Musa. Kama usiue. Hata kunje nani hawezi kukuruhusu uue wewe kwa hivyo that law will remain there.

Second tumeona kwamba in 1963 tuliambiwa uhuru umepatikana. Halafu afterwards kulikuwa na lands kama za Mazrui na watu wengine hata tumesikia Masai hapo wamehamiswa. These lands, huyu Sultani wa Zanzibar, huyu alikuwa huko kwao. Hakuja hapa na land hata kidogo. They met people there afterwards kwa nini waseme hii itakuwa land ya sultani, hii itakuwa land ya nani. Halafu you know what they did, waliwafanya watu walipe kodi pale. Hio ndio tatizo la leo la squatters, hapa Coast Province. Hapa kuna ungumu. Kwa hivyo unakuta hakuna humman right zile basic humman right ambazo mwananchi wa kawaida anastahili kupata. Hakuna. Sasa wewe unaabiwa wewe ni mwananchi na uko uhuru, serikali ya Kenya ilipata uhuru since 1963 halafu wewe leo hii huna pahali kutoka hii Kenya ipate uhuru halafu sasa. Wewe ni squatter. Can you tell me what development are you to make if you have no land? Hio sasa ni upuzi tu but if the government is looking at it, hawafanyi kitu. Sasa hii basic humman right, sasa ni right gani mwananchi wa kawaida anastahili kupewa lakini ikiwa vitu kama hivi hapati, kuna nini? Kwa sababu, hapo, kama kule Kilifi District kuna mashamba thousands and thousands of acres. Lakini unaambiwa ni individual and this person does not make use of it. Mwakwa imeingia moto, inaingia moto. Hii land kama hii ningependa Katiba ivutilie mbali kama ni mtu ana land lakini haifanyiwi kazi. Jamani, ana shamba ekarii 3,000 lakini haifanyiwi kazi ni ng' ombe tu zinaishi pale. Halafu pale pale kuna wananchi wengi kabisa hawana mashamba. Wanakaa tu na serikali iko pale. Sasa jamani, hii serikali yetu sasa kuna uhuru kweli hapo. Mimi ninaona ikiwa kuna uhuru basi ni uhuru wa mtu mmoja ambaye ni tajiri. Such land kama Mazrui coastal strip ningependa zifutwe kwa sababu ikiwa yeye ni mwananchi, ikiwa serikali inataka usawa katika wananchi wote, jamani zile thousands of land za yule mtu mmoja badala ya kupewa yeye ichukuliwe na serikali. Halafu yeye pia apate kama mwananchi wa kawaida na wale wengine pia wapate. Maanake vile mambo yalivyo ni utumwa kabisa sasa ni kabisa.

Another thing ni leave – Hii kitu

**Com. Abubakar:** Bwana Chai inatakikana ufupishe sasa saa zako zizapita.

**Charles Chai:** Thank you very much. utaniwia radhi kabisa. Ninataka niende mbio, mbio. Kuna kitu kingine tunaita leave. Watu wengi hatukielewi. Hii leave ningependa Katiba yetu hii ambayo tunauda leo tutapokea maoni leo na pengine kesho Mungu akitujalia itatuongoza sisi wenyewe. Hii lease isiwe ya mtu mmoja tu. Sasa hii ni mauaji kwa sababu utakuta pale kuna watu wengine wanaitwa sasa ni squatters. Hakuna raiya anaweza kuchunga mwingine vizuri kabisa isipokuwa ni Katiba yetu hii ambayo tutaiuda. Kwa hivyo lease iwe inapewa kikudi na Katiba hii ama serikali yetu iangalie huyu mtu kama anaweza kupewa hata kama ni 50 acres ama 100 ili hiki kikundi chetu kiwe kikikuwa beneficial to the wananchi si benefit ya individual peke yake, no.

Another thing mwenzangu alizungumzia kuhusu women rights. Women right ni kitu ambacho ni kigumu kidogo. Lakini mimi napenda kuongea kwa ufupi. Kama mzee mwenzangu alisema iwekwe kama traditional law. Hapo mimi namuunga mkono kwa sababu pia ningependa, ninaona kuna mahali panaitwa mahakama hapo. Sasa katika hiyo mahakama kuna mahakama nyingi katika hii Kenya yetu ya mazungumzo. Lakini sasa nataka kuuliza kitu moja katika hii mahakama. Tungeona kwamba kuna mahakama pia ya Chief Khadi. Huyu Chief Khadi nimesikia mtu mmoja wa Ki-islam akisema kwamba awe muislamu. Sasa pale ni mambo ya dini peke yake. Sasa ikiwa mambo ya dini, ni dini ya Kislam. Na kama hatujasahau nimesoma historia kidogo sio sana. Katika historia ile ya Kenya kama ikilinganishwa na ya Uganda tumesoma wakati ule wa Kabaka kulikuwa na dini tatu. Ya kwanza ilikuwa ya Muslim ambayo ililetwa na Waarabu, ya pili ilikuwa ni ya Kristo na pia kulikuwa na wale ambao hawakuwa kwa Kristo wala ya Kiislam. Wale waliiga traditions zipi? Kwa hivyo katika mahakama yetu ama Katiba yetu ambayo tutauda hivi ipeane uhuru wa dini. Traditionally pia idhinishwe iwekwe katika Katiba. Kwa sababu ni hapo hapo kwenye tradition ambapo kuna waganga wa kienyeji. Waganga wa kienyeji nowadays are playing a very important role in the community. Hawa pia nimesikia Nairobi wako na hospitali na wanatibu pia wakitumia madawa ya kienyeji. Kwa hivyo Katiba yetu isiwe tu, yaani mtu akionekana agangua anachukuliwa na police, analipishwa kodi. Huyu si uhuru kwa sababu huyu mtu anasaidia watu ule uganga. Ule uganga unasaidia watu na kwa hivyo haupaswi kumzuia zile shughuli zake, unless ana endanger to the security of the state like anybody else. Lakini kama ni kugangua tu ile ni kutoka jadi kabisa, hata babu yangu alikuwa mganga.

**Com. Abubakar:** Bwana Chai ushaapitisha mara mbili ya mda uliowekewa.

**Charles Chai:** Asante sana lakini wacha nimalizie kidogo dakika moja. (Interjection)

**Com. Abubakar:** Ngonja kidogo. Jamani. Sihitaji usaidizi wenu kumharakisha. Mimi nina njia zangu, asanteni. Malizia kabisa Bwana Chai. La mwisho.

**Charles Chai:** Asante sana Bwana Commissioner. Kwa hivyo sitaki niwachokeshe wenzangu lakini ningependelea hivi, Katiba yetu hii tunaenda kupeana maoni, serikali yetu iwe itafikilia the basic humman rights. Na hizi basic humman rights kama yule mtu anayehusika, ikiwa ni land yule mtu ambaye anaishi pale, pale apewe ile land. Kusiwe na mtu mmoja apewe ekari 20.

**Com. Abubakar:** Ushaasema hayo Bwana Chai, unayarundia sasa. Bwana Chai asante Bwana. Andika jina lako kwenye register utoe na maandizi yako. Asante Bwana Chai. Na si kukuonea Bwana Chai. Sasa ndugu zangu, wazee wangu, mama zangu, dada zangu, list yetu tumefikia mtu wa 17 sasa. Kuna baadhi yetu wamemuuliza katibu, haya majina yanatajwa vipi? Majibu yetu ni kwamba majina haya yanatajwa kulingana na register ile ilioko pale nje. Ikiwa uliingia dani hujajiadikisha pale nje, jina lako litakuwa haliwezi kufikiwa na ni katika kuandika jina lako pale nje ndio tukufikie na tunafuata ratiba hii. Na niliwaeleza ikiwa tutabadilisha utaratibu utakuwako kwa kuzingatia watu ambao wanataka kupewa fursa kulingana na sababu maalum. Sijui kama mnanielewa. Sasa mtaona kwamba kuanzia kutoka kwa Bwana Chai nitakuwa nikiwaadama wakati vizuri

sasa. Ukipewa dakika tano zikifika tano Bwana ukipfikiwa ukiambiwa namna hii Bwana uyamalizie. Sio umeachiwa ndugu yangu, na si kwa sababu ya Bwana Chai. List yetu imefika watu 90. Sijui mnanifahamu? Tumefika watu 90 na sasa tuko kwa jina la 17 kwa hivyo tunaomba mkija kutoa maoni, mtoe haraka, haraka ndio tuwafikie kila mtu. Mtu wa 17 ni Brighton Mwambeka.

**Brighton:** Commissioners, MP na wananchi. Kwa jinalangu naitwa Brighton Mwambeka. Mimi nitasoma kwa haraka haraka ili nimalize.

**Com. Abubakar:** Mzee wangu pengine tutakuwa hakuna fursa ya kusoma yote. Chagua yale muhimu uyasome hayo.

**Brighton:** Asante. Kwamba Katiba ya kitaifa ilioko ni baya na inaadhiri vibaya maisha ya Wakenya hata wa Pwani. Pamoja na hayo haitekelezi kwa manufaa ya haki na utawala wa kisheria na wenye mamlaka ya kidemocracia. Kwamba Katiba peke yake haitosi, hata iweje kulinda haki za Wakenya mpaka serikali na wananchi wenyewe wawe na muamko wa kutetea haki zao za mabadiliko, kimawazo, na kuzingatia malengo ya ile Katiba waliotengeneza. Kwamba kuwe na Katiba ya mfumo ya utawala wa majimbo Kenya. Ikiwa na maana hii. Kwamba kuwe na taifa moja la Kenya, kwamba kila mwananchi wa Kenya awe na uhuru wa kuishi na kuwa na mali mahali popote nchini atakopochagua. Kwamba kila jimbo liwe na mpango maalum wa kuhifadhi na kutumia fedha zinazotokana na raslimali zake. Serikali ya jimbo isimamie na kuhifadhi raslimali za jimbo hilo na kuhakikisha zinatumika kuleta maendeleo ya jimbo lile kisha ya kitaifa baadaye. Kwamba kila jimbo liwe na sheria zake ambazo zitalinda haki za kila Mkenya bila kujali kabila, langi au dini.

Kuhusu ardhi na laslimali zetu – Kwamba Wapwani wanapinga na kuraani propaganda zinazotumiwa kuchafua jina la WaPwani na kuwadhalisha ili kuwanyonya na kuwapuuza. Propaganda chafu hizi ni kama ati wa Pwani ni wavivu na watu wanaopenda kukaa chini ya minazi na miembe badala ya kufanya kazi. Wa Pwani ni wakalili kuwa wanaishi kwa jasho lao na hawategemei cha bure kutoka kwa serikali, kabila au mtu yeyote yule. Kwamba Pwani imetunukiwa na raslimali nyingi ambazo zitatumiwa vizuri kwa manufaa ya watu wa Pwani na ya kitaifa, zitasaidia kuondoa ummaskini katika sehemu hii ya Pwani, kuleta maendeleo na ufanisi mkubwa nchini. Raslimali hizi ni wananchi wa Pwani wenyewe, utamaduni wetu, ardhi yetu, madini yaliopo katika mkoa wa Pwani, buga za wanyama wa pori, misitu, mimea, mazao ya ardhi, viwanda, mahoteli, mifugo, masoko na bahari na raslimali zake. Zote hizi ziko katika mkoa wetu ambazo raslimali zake hazimfurahisi Mkenya.

Asimio kuhusu maswali ya jamii na uchumi: Hudumma za afya. Kwamba hudumma za afya zimetoloteka kabisa katika mkoa wa Pwani. Watu wengi sana wanakufa kwa ukosevu wa matibabu. Kwamba kuwe na matibabu na madawa ya bure kama ilivyokuwako hapo mbeleni. Kwamba madaktari wa hospitali za serikali wasiruhusiwe kuwa na mahospitali ya kibinafsi. Badala yake wawe na mishahara mizuri ya kuwanufaisha kimaisha.

Kuhusu elimu – Kwamba kuwe na elimu ya bure kwanzia shule ya vidudu hadi ya msingi. Kwamba mfumo wa elimu 8-4-4

uondolewe na badala yake kuwe na mfumo wa 7-4-2-3. Kwamba walemavu wapewe elimu bure kuanzia vidudu hadi chuo kikuu. Kwamba kila mkoa uwe na chuo kikuu chake chenyewe. Kwamba Katiba iwe mojawapo ya masomo katika shule zetu za upili zote.

Uchumi – Kwamba ihakikishwe kuwa kuna mipango ya kumuwezeza kila mwananchi awe na njia pahali ya kujipatia liziki na mapato ya kujiendeleza. Kwamba biashara zote za rejareja zifanywe na wananchi peke yao na pia kwamba hudumma ndogo ndogo kama za matatu na kadhalika zitolewe na wananchi peke yake. Kwamba mipango iwe na itekelezwe ya kulida na kusaidia kukua na kuendeleza kwa viwanda vya kienyeji, biashara za kienyeji kilimo cha kenyeji na hudumma za kienyeji kutokana na mashidano kutoka nchi za kigeni. Kwamba watu wasio na kazi wapewe kazi katika shehemu zao. Kwamba sheria ya nguvu kazi itekelezwe kuhakikisha kuwa mtu hawezi kuwa mfanyi kazi wa kibarua kwa zaidi ya miezi sita kabla ya kuajiliwa kabisa. Kwamba wapigwe marufuku watu wa nchi za kigeni kuvua katika bahari yetu na pia zipigwe marufuku leceni za mitungi na majahazi madogo madogo. Kwamba kila mwananchi awe na uhuru wa kufika na kutumia ufuo wa bahari ipasavyo na vikwazo vyote vinavyomzuia hivi vitu vikumuliwe mara moja.

**Com. Abubakar:** Mzee Mwambeka unahitajika kufupisha.

Ukulima – Kwamba serikali itoe vikolombezo vya kuendeleza kilimo kwa kuhakikisha wanatekeleza mipango ya kuhakikisha wakulima wana ardhi ya kutosha, mbolea, mbegu, mboga , vifaa, kusafiri na mawaziliano. Kwamba kila wilaya za Pwani na hata Lamu na Tana River zina matatizo makubwa mno ya kukosa barabara, mandaraja, hudumma za simu na posta na kadhalika. Jambo ambalo ni kikwazo kikubwa cha maendeleo ya aina yoyote na usalama katika sehemu ya mkoa wa Pwani.

Fedha – Kwamba serikali izidiki mabenki na ihakikishe inaweka kanuni ya viwango vya riba ya kutoshwa na mabenki.

Mazingila – Kwamba kuwe na sera na mikakati ya kimaendeleo ya kulida na kuhifadhi mazingila kwa ajili ya vizazi vya leo na vijavyo.

**Com. Abubakar:** Mzee wangu, mambo mawili ya mwisho.

**Brighton:** Kenya tuitakayo – Kwamba Katiba iwe somo la kufudishwa katika mashule. Kusiwe na ubaguzi wa kikabila, kirangi, kidini au kujinsia katika kupeana haki za kitaifa kwa wananchi kama vipande na passport za kitaifa.

**Com. Abubakar:** Asante sana mzee Mwambeka. Thank you.

**Com. Kabira:** Tutaendelea na nitamsaidia Com. Abubakar kwa mda mfupi na nitamuuliza Geofrey Kimego.

**Geofrey Kimego:** Macommissioners na wakaaji wa Voi, hamjambo. Yangu ni kugusia katika maoni yangu ya kurekebisha Katiba kugusia mode of employment. Nalikuwa ninasema kwa sababu Wakenya wote sasa wamesoma nafikiri ingekuwa muhimu sana kama Katiba ingegeuzwa badala ya kuandikwa kuwa permanent and pensionable watu wakiandikwe on contract basis kama nchi zingine jirani. Nafikiri hii itawezeza Wakenya wengine kupata nafasi ya kuumma the national cake.

Ya pili, Wakenya pia ambao wamezawahi kufanya kazi kwa civil service mpaka retirement age, majority holding very senior positions wasiwe employed back in other government organization kama vile imekuwa ikiendelea. Hi itatoa room kwa wale ambao hawajawahi kuandikwa kazi kupata nafasi hizo.

Nikigusia pia swala ambalo kama Katiba yaweza kuangalia kuna kitu kinaitwa experience katika new openings. Utakuta wanasema experience five years, ten years umetoka chuoni jana, hao wataangaliwa vipi? Muangalie kama Kenya itatufungulia college of experience kutoka vyo twende kwa hio ingine au itakuwa vipi kama hio Katiba haitabadilishwa namna hio?

Ningependa kugusia Katiba ambayo inahusu malipo ya hospitali, NHIF maanake wafanyi kazi wengi wanaona ni kama conning. Unakatwa pesa na haziwezi kukusaidia wakati wowote.

Lingine na labda ni la mwisho kama mlivyosikia leo asubuhi wakati tulikuwa pale utasikia mimi ni lecturer, mimi ni commissioner, mtu mmoja Mkenya mmoja ana nafasi mbili za kazi. Wakenya wote wamesoma, wengine unashika huku, unashika huku na kuna mwenzako hana kitu. Kama kuna Katiba itagusia hapo tafadhali Mkenya asiwe na zaidi ya kazi moja wakati Wakenya wengine hawana kazi. Yangu ni hayo.

**Com. Kabira:** Asante sana Bwana Geofrey, utakuja kuandika? Asante. Na leo tutamuuliza Stanley Mwakesi. Stanley Mwakesi yuko?

**Stanley Mwakesi:** Commissioners nafikiri mimi nitatoa maoni yangu Tausa niwakilishe watu wa Voi. Asante sana.

**Com. Kabira:** Nitamuuliza Suleiman Mwakichi. Asante.

**Suleiman Mwakichi:** Basi hivi ama mimi, commissioner abaye amekuja hapa, maoni yangu nitakayetoa sitatumia kwamba naomba, nitatumia kwamba nataka, kwa sababu twataka Katiba mpya. Sisi watu wa Voi watu wa Pwani sisi tunasema twataka Katiba ya majimbo. Katiba ya majimbo tutakayo sisi twataka pia tuwe na Bunge letu la jimbo la Pwani. Twataka makao yetu ya jimbo la Pwani yawe Mombasa. Twataka wabunge ambao watakaochaguliwa hapa kila constituency iwe Bunge iko Mombasa na tuwe na Bunge kuu la kitaifa ambapo kila district ya Pwani itatoa mbunge moja kuwakilisha district katika Bunge la taifa huku katika Serikali Kuu.

Maongozi ya serikali ya majimbo – Twataka naibu wa chief awe ni mtu kutoka sehemu hio hio ambayo naibu wa chief anatoka, sio mtu kutoka nje. Na awe ni mtu wa kabila ya hapo au awe ni mtu wa kabila la jimbo la Pwani.

Chief – Twataka chief ambaye atatuakirisha katika location awe ni chief kutoka location hio awe ni mtu kutoka kabila la hapo au awe ni mtu kutoka kabila la jimbo la Pwani.

DO – DO ambaye atatumwa na serikali ambaye ataajiriwa na Tume ya kuajiri ya wafanyi kazi ya umma, awe ni kijana au ni mzee au ni mama kutoka jamii ya kabila la wajimbo la Pwani au awe ni kabila ya jimbo ya pahali alipotumwa kama DO.

DC – DC awe ni mtu mwanamme au mwanamke ambaye ametumua au ametoka kabila la jimbo hilo au awe ni kabila ya district ambayo ametumwa kufanya kazi.

Kuhusu serikali ya wilaya – Madiwani twataka wachaguliwe kwa miaka mitano. Madiwani hawa wawe wana moyo wa kufanya kazi na wawe ni watu wa maendeleo na wao ni watu watetesi kwa wananchi.

Mayor wa mji - Mayor wa mji twataka wananchi wenyewe wamchague kupitia kwa kura ya siri. Awe ni mpenda maendeleo na ni mtu marufu kwa jamii ya sehemu hio. Pia twataka mayor huyu achaguliwe kwa vipindi viwili. Kwanza ahudumu kwa miaka miwili na nusu kisa apigiwe kura tena kwa mara nyingine. Na awe ni jamaa wa jimbo hilo, awe ni mtu kutoka mahali hapo, sio mtu kutoka mahali pengine.

Naibu wa mayor – Naibu wa mayor vile vile achaguliwe na wananchi wenyewe kwa kura ya siri. Mayor na naibu wa mayor wasiwe macouncillor, wawe ni watu moja kwa moja bila kuwa na viti vyovyote vya ndiwani na wapigiwe kura ya siri.

Katibu wa mji au katibu wa jiji – Katibu wa jiji aajiliwe na Serikali Kuu na serikali ya majimbo. Huyo ni katibu wa mji au katibu wa jiji. Aajiliwe na serikali ya majimbo. Katibu huyu mahali anapofanya kazi awe ni wa jamii kutoka pale, awe ni wa jamii kutoka jimbo hilo la Pwani.

District commissioner DC – PC awe mwanamke au mwanamme lakini awe ni mtu kutoka jimbo hilo, au ni kabila la jimbo hilo hilo. Maanake ninaposema hivi ni kwa sababu DC wanaokuja hapa watakuja wawe wao ndio machairman wa mirandi yote ya maendeleo. Hawana uchungu na district hizo, wao kazi yao nikufanya na kuwacha wajamii wa Pwani wakiwa wamelala hivo hivyo na pesa za maendeleo wakarudisha mahali pengine. Hio hatutaki. Twataka wafanyi kazi wote wawe ni kutoka jamii ya Pwani.

Pia katika Bunge hilo la kitaifa, mbunge huyu wakitaifa ambaye atawakilisha wananchi katika Bunge la kitaifa achaguliwe na wananchi kupitia kila constituency. Kila constituency impigie kura na wale atakaeshidania nao ili akipata kura zaidi huyo ndiye

atakayekuwa mbunge wa kuakilisha Bunge la kuu la Kenya.

Kuhusu mambo ya kazi ya waziri – Waziri ambaye atakuwa amechaguliwa na Waziri Mkuu. Sisi waPwani au mimi mpwani nahimiza kwamba ni lazima mawasiri wachaguliwe wanne kwa kila jimbo. Ni lazima tuwe na naibu wa waziri nane kila jimbo.

Kuhusu Waziri Mkuu – Waziri Mkuu awe ndiye mwendezaji wa serikali ambaye anaweza kuteua baraza la mawaziri na kuvuta mawasiri hawa. Lakini, awe ni mtu hajafungwa, ama hajafanya uhaini ama hajafanya lolote libaya. Pia awe ni mtu mwaminivu, mchaji Mungu ambaye ana familia kwa mfano ana bibi na watoto. Huyo achaguliwe kama Waziri Mkuu. Msiende mkalokota lokota watu kutoka simwa akawa Waziri Mkuu.

Rais wa nchi – Rais wa nchi twataka awe ni Rais ceremonial. Awe tu ni mtu wa kuandaa mambo ya sherehe za kitaifa, kupokea wageni na mambo mengine. Lakini mambo yote yawe chini ya Waziri Mkuu ambaye ndie atakuwa mwenye serikali.

Kuhusu uteusi wa Mkuu wa Sheria – Mkuu wa sheria ateuliwe na barasa la mawaziri.

Kuhusu uteuzi wa majudges – Majudge wote kutoka wirayaani wawe wameteuliwa na Mkuu wa Sheria. Na Judge Mkuu ateuliwe na Waziri Mkuu.

Kuhusu kikozi cha police – Twataka kikozi cha police kuanzia police yenyewe, police tawala, police jera, police wa polini. Mapolice hawa wakisajiliwa wakienda katika chuo na kwisha hitimu kila mmoja afanye kazi katika jimbo lake. Kila police afanye kazi kwa jimbo lake. Maana ya kusema hivyo ni kwa sababu kuna majimbo mengine ambayo haipewi ile keki ya kitaifa, lakini sisi wa Pwani tuna kasoro ya police tutajua tumenyanyaswa. Kwa hivyo twataka police wetu watakaoajiriwa walegezwe Pwani.

Kuhusu majeshi wa nchi – Majeshi ya nchi ni lazima yaandikwe kila kabila. Kila kabila iandikwe katika jeshi la Kenya kwa sababu jeshi hili halitakuwa likifanya kazi ya mkoa peke yake. Litakuwa ni jeshi la kulinda nchi na mipaka yote ya nchi bila kujali kwamba ni jimbo lipi ama ni jimbo lipi. Hili ni jeshi ambalo latakikana kila kabila liingie katika jeshi hilo kulinda nchi ya Kenya.

Kuhusu mambo ya ardhi – Sisi twataka commissioner wa ardhi, mpimaji na kila kitu aletwe Pwani Mombasa. Hatutaki aketi Nairobi wananchi wakistakabadhi huko na kila akija hapa aseme fulani ameondolewa ardhi hii si ya kwako. Twataka jimbo la Pwani tuwe na commissioner wetu kutoka Pwani na awe ni mPwani na awe ni wa kabila kutoka Pwani. Kwa haya machache nawashukuru kama kuna mmoja nimemguza haya ndiyo maoni yangu.

**Com. Kabira:** Asante sana Bwana Suleiman. Na leo tutampatia wakati Maria Chao Mwakio. Maria yuko? Tutasikiliza

Edith Odiambo tukimngojea Maria. Edith yuko? Hayuko? Edith Odhiambo. Okey. Raphael Mwachofi? Uko?

**Raphael Mwachofi:** Macommissioner na wananchi, majina ni Raphael Mwachofi kutoka Voi. Maoni natoa kulingana na wilaya ya Taita Taveta district. Walemavu wa Taita Taveta wamefikiria kwa makini kuhusu mjadara wa Katiba ya Kenya. Na furaha kubwa kupewa nafasi hii kutoa maoni yao. Naomba maoni yetu yazingatiwe. Kitangulishi.

Mlemavu ni mtu ambaye hawezi kutumia viungo vyake kama mtu ambaye ana viungo vyake. Tunaomba tume ya haki la kuishi kama wengine. Idadi ya walemvu haijulikani hapa Kenya na hata wakati wa kuhesabiwa huwa hawako kwa karatasi za kuhesabiwa. Naomba tuwe tukihesabiwa tujulikane idadi kamili na hali ama ulemavu wetu.

Mlemavu na Katiba – Katiba ya Kenya ambayo iko sasa haimtabui mlemavu kwa kipengere chake. Kwa hivyo sisi walemavu wa Taita Taveta tunaomba Katiba ya Kenya iwatabue walemavu kiKatiba na wapatiwe nafasi sawa na watu ambao hawana ulemavu wowote. Walemavu wahusizwe kwa kila jambo. Katiba ilioko yasema Rais ataondolewa mamlakani wakati hajiwezi. Lakini kutojiweza kusihuzizwe na ulemavu.

Haki za kimsingi – Walemavu wapewe haki ya kuishi na kusiruhusiwe kwa mwanamke kutoa mimba ilio julikana atazaa mlemavu. Wakati wa vita walemavu walindwe kiKatiba wasisubuliwe maana hawawezi kukimbia kama wengine.

Haki ya uhuru – Watu wa hudumma ya jamii wawe katika mahakama police station ili waweze kuzuia kugadamizwa kuwa walemavu wa akili ambao wangefikiliwa kwa makosa ya kuwa wamevunja sheria. Walemavu walindwe na utumwa na kazi za kurazimizwa.

Haki za elimu – Mlemavu au walemavu wapelekwe shuleni na wapewe elimu sawa na wengine asiekuwa na ulemavu wowote. Wote wawe wakisoma darasa moja. Walemavu wapewe elimu ya bure.

Haki ya afya bora na hudumma zake – Madaktari wawe wakifundishwa mambo ya walemavu na lugha ya vitendo, waandike Braille. Walemavu wasinyimwe kazi kwa sababu ya ulemavu, na kuwe sheria ya kuwalinda wapewe haki ya kurasisha maisha kwa kupewa utafsiri wasiosikia na kupewa vifaa vya kusikia, kutembea na hata kuandika kwa wale wasioona.

Sheria za kimataifa – Serikali ipitize sheria ya umoja wa kimataifa, standard rules, na Tume ya taifa ipitizwe Bungeni.

Uhuru wa wa mazingira – Sheria ipitize majengo ya umma yote yajali masilahi ya mlemavu, barabara, lift siwe za computer za kuelezea mahali imefika na ambazo wheelchair zaweza kuingia ndani ya lift. Magari ya usafiri pia yajali masilaha yetu. Simu zote za umma siyajali maslahi ya walemavu. Vioo vya umma vijengwe kulingana na ulemavu waweze kuingia dani bila wasiwasi. Katika jamii watoto walemavu wapatiwe usawa na watoto wengine wa jamii ambao hawana ulemavu.

Uridhi mali, wapatiwe elimu sawa. Walemavu wapewe nafasi katika kugombea uBunge na ucouncillor lakini uajichague wenyewe katika wakilishi Bungeni. Angalau kwa district tupate wawili na kila division, kila county council, municipal council tuwe na councillor wawili walemavu hata town council.

Pili kuongeza yangu mwenyewe mlemavu wa ajali kuhusu lawyers. Hawa lawyers tungekuwa tukipendelea kama waki-receive case kuwe wataandika cheque zao tofauti na za walemavu. Walemavu wengi wameadhirika sana wakifikisha case wanakuambia bado, bado mpaka mwishowe inapita namna hio. Asanteni.

**Com. Kabira:** Asante sana Raphael.

**Com. Abubakar:** Kuna badhi yetu wangependa kutoa miswada yao bila mazungumzo. Watu wa aina hio wana ruhusa ya kuja kuandika register jina lao na kutoa miswada na kutuachia. Tumepata ombi kwamba kuna watu wangetaka kutoa miswada na waende zao. Una fursa hio kuja ukitoa mswada wako, ukaandika jina lako halafu ukawa na haki ya kuondoka. Na kama unavyona mda unazidi kuenda bio tunajaribu kusimamisha mtu kwa zile dakika tulizo toa. Dakika 5 kwa mtu anaetoa maudhui muhimu ya mambo muhimu anaezungumzia kwenye mswanda wake na dakika 10 kwa mtu ambaye hana mswada. Asante.

**Com. Kabira:** Asante sana Mwakala Mwanyumba.

**Mwakala Mwanyumba:** Asante sana commissioner pamoja na wananchi kwa ajili ya kuchangia Katiba yetu hii mpya. Lile jambo la kwanza ningetaka kuongea, tunataka uhuru wa majimbo. Kwa sababu tunaposema tunataka uhuru wa majimbo ni sababu sehemu zetu tuseme kwa fano hapa nchini kwetu Pwani tumekuwa maskini. Tumekuwa maskini kwa sababu mali zote zinatoka hapa nchini sehemu za Pwani nazo sehemu za juu. Tunaona kwa mfano mambo kama ya maji, tunaona mambo hii ya park, mambo ya madini yote mali zote twapenda pahali za juu. Tunaona sehemu ya Pwani inakopa pesa kutoka nje ambazo ni pesa zake. Na ni ajabu mtu utoe pesa zako mwenyewe pale kwenda kuzikopa. Kwa hivyo tunataka uhuru wa majimbo. Wapendwa kusema kweli sisi tusipokuwa na majimbo watu wa Pwani tutazidi kuangamia.

Nafikiri jambo la pili ni la squatter. Wananchi wamebatizwa wakaitwa squatter ni jambo la ajabu. Hii jina likikuwa la mkoloni, mtu kuitwa squatter. Na ni ajabu squatter ndiye anaanza mji. Tunaona squatter anaanza mji wake kama ni hapa Voi, ananjenga mji, nyumba moja nyingine anaingia hata mpaka zimefika 50. Serikali tayari inaenda kujitokesha mahali pale. Wale watu wamefanya mpango wapate electricity moto mpaka maji. Wale watu tayari serikali imepiga macho pale, ameona maendeleo. Hapo tayari squatter ataanza kuzukumwa na hapa ni pahali pa kupeana watu wengine. Jambo la kusikizwa sana katika Katiba tunaichangia. Jina la Katika katika Katiba yetu jina squatter liondolewe. Mwananchi halisi ni mzaliwa, ameishi mahali mda wa miaka kumi anaondolewa kama mtu asiyejulikana ni Mkenya. Jambo la aibu. Mtu ameishi miaka kumi. Amezaliwa amekaa miaka 100 ama 90 amekaa miaka 40 wengine 60 anakuja tolewa kama hapa si kwao. Watu wametoka

Nairobi mji bora Nairobi unaabiwa hapa uchukue mahali kwa mzee Tisa ama Mwanyumba ondoka hapa. Watoto wako wana miaka 40, watoto wana miaka 30 unaondolewa uhame. Hapo mkikaa chini kusema kweli wapendwa wanapata shida. Ni haki mtu akipata mahali ameanza mji serikali imupate pale imsaidie, imujengee nyumba vile inavyotakikana kunjenga. Jambo hilo nataka Katiba iandikwe.

Nitaongea juu ya mayor – Mayor awe mtu amechaguliwa na wananchi. Mayor awe mtu wa aweke cheo mda wa miaka 5. kilauni ya miaka miwili ni kazi gani? Miaka miwili ni kitu didogo sana, unaingia mayor leo kabla ya mwaka mmoja utaanzisha mayor hajapima pamoja mladi gani? Hujatembea Voi nzima ukaimaliza na miaka miwili imekwisha. Naomba Katiba iandikwe kwamba mayor aongozewe mda uwe miaka 5.

Naongea juu ya police – Kama uko police hapa usikize. Police wamekuwa na mamlaka makubwa zaidi. Tunaomba katika Katiba tunaichangia police wawe wakipewa training kwa miaka miwili ama miaka miwili na nusu ikiwa mahali anapost ama anatumwa. Miaka miwili na nusu ikimalizika apelekwe mahali pengine. Kwa sababu anapokaa mahali pale anajuana na wananchi wote wanafanya makosa, wakiiba wanakwenda kumpa kitu. Basi hapo mambo hapo haitakuwa mazuri.Kwa hivyo jambo hili liingie kwenye Katiba yetu. Police akiishi zaidi ya miaka 10 katika kituo kimoja. Atakuwa rafiki na wananchi. Ukikosa jambo hili anakuwa ni rafiki yako. Tunaomba katika Katiba iandike jambo hilo katika kuchangia kwetu.

Juu ya ummaskini – Nataka kusema ummaskini hapa kwetu hautakwisha. Lakini tutakapokuwa katika majimbo tunajua ummaskini utapungua kwa sababu siku hizi naona pesa zetu zinaenda nje. Hapa kwetu Pwani kumekuwa ni maskini. Hatuwezi kuokoa maskini mwenzangu kama pesa sina na enda kuokoa menzangu na pesa sina namna gani? Haiwezekani. Lakini kama pesa ziko hapa dani tunaweza kujua kwamba hawa wakubwa wetu wa Pwani ndio walitufunya hivyo imeshindwa, serikali ya sasa haiwezi kuinua maskini. Kwa hivyo wapendwa serikali iwe ya majimbo. Kuwe na governor wa Pwani, kuwe na Rais wa Kenya nzima. Mipango ya Pwani ni ya Pwani. Kwa kila jimbo kuwe na mpango wake.

Mamlaka ya Rais – Asipewe mamlaka mingi ambayo vile kama Rais wetu yuko sasa. Inaonyesha kwamba Rais akiwa amekosa ameiba hawezi kushitakiwa. Lakini mamlaka iwe mamlaka ya chini kama kawaida ya wananchi wengine. Kwa sababu kama amepewa mamlaka hiyo kama hawezi shitakiwa atakura mali, pola mali mpaka mwisho. Hata itakapokuwa mda wake umeisha anatoroka anakwenda zake ngambo. Nchi ameacha maskini. Mamlaka ya Rais ipunguzwe. Yangu ni hayo machache.

**Com. Kabira:** Asante sana Bwana Mwakala. Rev. Silvanus, M.M.. Okey. Asante.

**Rev. Silvanus:** Macommissioner na Wakenya wenzangu na Waislamu nawasalimia nyote. Wasalaam aleykum. Ningependekeza kwamba niseme tu kwa uchache maana mengi yamekwisha semwa. Ni kwamba Mkenya aweze kuwezeshwa na Katiba hii mpya kumiliki mali ile ilioko mahali pale aliko. Kama vile kwa mfano pale kwa pale Kachigau kuna mali lakini

ukiangalia barabara huwezi ukaamini mali inayotoka kule ndio inatoka mahali pale lakini ni mali nyingi sana ambayo inaenda kujenga kule Nairobi na mahali kama Kachigau tumeshalalamika na mali yote inatoka mahali pale Kachigau.

Pia nikiangalia katika hali ya makanisa ambapo limesemwa na mmoja wetu, amesema kwamba makanisa katika Katiba ya sasa yaweze kutabuliwa na ikitabuliwa hivyo basi kusiwe na uwezekano wowote karibu na kanisa. Kuwekwe distance fulani ambayo itawezeza mambo kama bar, mambo kama disco kubwa kubwa ziziwekwe karibu na makanisa. Kwa hivyo kuwe na nafasi ya kumtabua Mungu maana yeye ndiye ametupatia mambo hayo yote. Pia hivyo hivyo kuna makanisa yanayochipuka yasiwekwe karibu. Kuwe na distance fulani ambayo Katiba itaweka kiasi kwamba kanisa itakapokuwa hapa lingine liwekwe mwisho kule la kuhudumia wengine likiwa la Kikristo. Pia vile vile kama ni mosque kanisa lingine lisiwe karibu an mosque kiasi kwamba wanapoabudu kule yule Mungu mmoja tunayemwamini kuwe pia huku anaabudiwa. Tafadhali kuwe na long distance ambaye itwozeza miskiti na makanisa mengine kuwa hivyo. Pia mwananchi aweze kumiliki serikali moja kwa mja. Kwa nini niseme hivyo? Ili kwamba yule ambaye amewekwa mahali fulani awe amedhibitiswa na kuchaguliwa na Mkenya, mwananchi mwenyewe badala ya kuchukua mtu kuwekwa mahali fulani.

Elimu iweze kupeanwa bure kutoka mashinani mpaka ngazi za juu mpaka, yaani kutoka nursery school mpaka university. Vile vile Katiba hii ambayo tunazungumzia ambayo nyanya yangu hajaijua, na mama yangu na uhakika hajui nini, iwezekane sasa kuwekwa katika lugha inayoeleweka kwa mtu yule wa chini ili ifunzwe katika shule.

Kuna hii equal division of national cake. Kuwe na mgao sawa sawa wa yale yanayotoka katika Serikali Kuu pale juu kwa sababu tunaweza kuona sehemu zingine unaweza kwenda ukute electricity imegawanywa mpaka mahali pale haitakikani kugawanywa, na sehemu zingine haiko kabisa. Pia katika hali hio kuna wakosaji katika serikali yetu. Sasa wanapositakiwa na kufungwa, ile mali walioiba yapotea. Sasa kuwekwe kufungu katika Katiba hii kwamba atakapochukua mali, alipe na aende atumikie kifungo na tena aachizwe wadhifa ama kazi ile alioko nayo. Mara nyingi tunazungumzia mambo ya vijana katika Katiba zetu za viama, katika sehemu nyingi utasikia kijana. Lakini utakapoangalia kijana anayekuwa represented katika that office is not even a youth, si kijana. Ni mzee na tunaye kijana angeweza ku-present, kuchukua nafasi kama kijana. Kwa hivyo nafasi zile za vijana nazidhibitiwe na vijana.

Pili Katiba hii sasa tunaiandika tumeng'ang'ana, tumesukummana ndiposa sasa tumefika tunarekebisha. Sawa. Kuwekwe kipengere cha miaka mingine ijayo, watoto wako, watataka tena kurekebisha, maanake haitawafaa wakati huo. Watakuwa ni watu wa dot com na kadhalika, basi irekebishwe kwa haraka tusije tukawa na mgogolo kama vile hii tuliyokuwa nao mpaka ikaja kuwa hasa limefikia kukubaliwa. Asanteni na tuendelee kurekebisha Katiba.

**Com. Kabira:** Asante sana Bwana Rev. Silvanus. Maria Chao amekuja? Hajaingia? Na Edith Odhiambo. Ok. Cerestina Mwamburi.

**Cerestina Mwamburi:** Macommissioner na wananchi wenzangu, kwa jina naitwa Cerestina Mwamburi na hapa pia nawakilisha walemavu. Tumeandika na mwenzangu lakini mimi nitagusia juu ya basic rights na nitatumia Kingereza.

Nitaanza na people with disability. The Constitution which is there now.

**Com. Kabira:** Would she prefer to sit down?

Pia kuna mambo hii ya uchaguzi wa mayor. Uchaguzi wa mayor ningelipendekeza ya kwamba uwe unachaguliwa na wananchi wote. Pia mambo ya machief, mambo ya ma-assistant chief, hii ningeomba ya kwamba ni vizuri kwa sababu ni hawa watu wako karibu na wananchi, wachaguliwe na wananchi wenyewe. Pia kuna mambo ninasema ya kwamba kuna watu wanapitania kwa mfano ile ya u-Rais nilisahau kidogo lakini nitaomba msamaha ya kwamba Rais awe ni nani? Anaweza kuwa mwanamke awe ni mwanaume. Na mimi sitaki kuguza mambo ya walemavu anaweza kuwa mlemavu mwanamke ama mwanamke. Kwa hivyo ni mtu ambaye anaqualify kwa kazi yeyote ile awe Rais anaweza kuwa Makamu wa Rais anaweza kuwa mbunge, mambo kama hayo.

Twangalie mambo ya kwa mfano utekelezi wa mbunge. Utekelezi wa mbunge nafikiri inatakikana asikie kutoka kwa mwananchi, sio mtu atekeleze kwa mawazo yake mwenyewe halafu anaenda kufanya au anaenda kusema mswada ambao hajatumwa na wananchi. Ni mtu arudi kwa wananchi aulize. Hali kadhalika Rais ni hivyo hivyo. Hali kadahalika councillor ni hivyo hivyo. Mtu asije akafanya mambo kwa akili yake halafu yakaleta collision.

Pia maoni yangu ni kwamba kwa upande wa walemavu ni kwamba ninaunga mkono kwa dhati yale yaliosemwa na wenzangu. Na katika haki ya uajiri tunataka tuseme ya kwamba wanastahili kuajiriwa kama wengine. Nilisitikika juzi ya kwamba hata interview tulifanya za assistant chief hio longo tu halafu mtu aki-qualify, si ana-qualify kama mwanadamu ama kama mwananchi? Kama mtu haja-qualify, haja-qualify kama mwananchi. Hatujali kama ni mwanamke, hatujali mlemavu, hatujali nini. Lakini kuna mtu ambaye alitamka tamko ati kigulu aweze kufanya hii kazi ya assistant chief? Jambo ambalo linaudhi. Kwanza ile matamshi kigulu, kiwete, kidhini, sisi vile tulivyosoma ni kwamba vitu visivyo na uhai. Kwa hivyo unapoita mtu ki- weka ziwi, kiziwi, tunataka matamzi hayo iandikwe KiKatiba wakati umeita mtu namna hiyo utachukuliwa hatua kamili.

Na lingine ni kwamba wazazi tumefanywa sisi kuwa na elimu duni wale wazazi ambao tunazaa walemavu hata mimi naweza kuzaa mlemavu kama mlemavu na pia wewe sio mlemavu unaweza kuzaa mlemavu na hata kama wewe si mlemavu pia unaweza kuwa mlemavu wakati wowote kwa njia ya ajali na kwa njia yeyote ile. Kwa hivyo inastahili ya kwamba tusifiche hawa ndugu zetu walemavu kama wananchi. Tuwasomeshe sawa na wengine. Tuwape uridhi sawa na wengine. Mambo kama haya yanastahili tufanye hivyo. Na tena mambo ya walemavu tunaomba ya kwamba ikiwa yanasimamiwa yasimamiwe na walemavu wenyewe sio ati tunaambiwa ya kwamba inasimamiwa na mtu mwingine on behalf of walemavu. Hatutaki namna hio tunaomba kikatiba iandikwe ya kwamba ikiwa ni mambo inayohusu mlemavu, ahusiswe mlemavu mwenyewe. Pia kuna swala lile lingine la kuhusishwa. Yaani kuhusiswa na kujihusihha. Ile representation iteuliwe na walemavu wenyewe kwa mfano saa hii tukisema wacha mzazi wa mlemavu tutume kama Kayanda ama tutume kama Ngoa, au tutume Mangeka iwe imetoka kwetu ama tutume Christina ama kwa mfano Omar watu kama hao. Tuwe tumewatumma sisi wapitie kwetu na hio itakuwa ni muongozo mzuri na ni pendekezo letu.

La mwisho ni kwa nafasi zile za uchaguzi. Ninajua kuna mambo yametajwa ya census ya kwamba walemavu wawe

wakihesabiwa na hali zao zijulikane huyu ni mlemavu wa macho, ni mlemavu wa viungo na mlemavu wa masikio na aina hizo. Wakiwa wakihesabiwa mambo haya yaandikwe na idadi yao injulikane kamili. Halafu hio upande wa uchaguzi iwe ya kwamba walemavu wapewe nafasi katika ucouncillor, katika uBunge na katika kila hali wakati wanachagua. Wajichague wenyewe. Kwa sababu sasa nikianza kupigana na mtu ambaye ana miguu yake yuko na viungo viake kisiasa, wengine wataniita kigulu, wengine wataniita kiziwi, wengine wataniita majina yale mengine ya kwamba huyu hastahili. Sitaona hata hio kura. Lakini kama sisi wenyewe tutajiteua, tutateua mtu wetu atuakilishe kama Bungeni, basi itakuwa ni haki. Kwa hivyo ni kwamba tungeliomba kwamba Katiba iiandikishe katika kila mkoa tuwe na angalau wabunge watatu walemavu wakiwakilisha mkoa na pia katika kila division tusikose mlemavu mmoja akiwa kama councillor. Hio ni pendekezo letu na tutafurahi kwamba tumehusihwa hata katika siasa kwa kuwa tumehusihwa kwa kila nyanja ili kujiwakilisha kama walemavu. Asanteni sana Mungu awabaliki.

**Com. Kabira:** Asante sana Mr.Mwaganga tutauliza councillor Roy Mwakadhi.

**Roy Mwakadhi:** Macommissioners mlioko hapa, wananchi, nafurahi kwa kupewa nafasi hii ili nizungumze machache. I will be very brief and to the point. Mimi ningependa kuzungumzia juu ya pensioners kama mimi mmoja. Yaani pension ni kitu ambacho serikali imeweka lakini inaonekana kwamba tukisha tengeneza, tumefanya na wizara balibali, tulipoondoka ni kama kwamba sheria haijaweka kipengere cha kuona ya kwamba pensioners huwa wameongezwa chochote lini. Huwa unatoka ukishaa toka basi ni kama umesahauliwa na ni kama umekufa, unapewa tu karatasi mwisho wa mwaka u-sign ya kwamba umemaliza mwaka na bado unaishi. Tungetaka sheria hii ambaye inageuzwa i-include kipengere ambacho kinasema pensioners watakuwa wakiongezwa baada ya miaka mingapi. Maana unajua salary reviews huendelea na hazijalishi pahali pengine ni miaka miwili, pahali pengine ni miaka mitatu, pahali pengine ni miaka mitano, lakini pensioners hawana pahali ambapo wako covered. Kitu kingine ambacho ningetaka kusema ni hizi allowances za civic leaders. Tumesikia hapa ya kwamba wabunge wanacommission yao nafikiri ya kujiongezea mshahara. Lakini kama civic leaders wote hawana hata forum ya kujiongezea mshahara. Na tena wanategemea pesa ambazo zinaletwa na wananchi kwa kodi, kwa fees and charges. Lakini ningependekeza ya kwamba wakati ujao wakati tunandiika Katiba mpya kuwekwe kipengere hata kimoja cha kusema kwamba civic leaders walipwe kutoka kwa consolidated fund.

Kitu cha tatu ambacho ningetaka kuguzia ni kwamba naona mambo ya kazi yamekuwa mabaya sana. Tunaambiwa hakuna kazi hapa Kenya lakini kuna kazi nyingi kama kwa mfano nikitaja police, KWS, prisons, KPA and all other parastatals bado ingawaje wana-retrench huwa wanachukua trainees. Maana taifa lolote ambalo halichukui vijana wakiingia kazini basi hilo taifa litakuwa na ugonjwa wa kuja kupata watu wote wamekuwa wazee na hakuna watu wa kuwa-replace. Lakini vile inavyoendelea ni kwamba wakati ambapo kuna interviews za police ninaona hapa Voi, nazungumzia nafikiri hata huko kwingine kwingine kuko na namna hio. Utakuta ya kwamba kama ni interview ya police, KWS, prisons ama KPA kama hujui mtu siku hizi, mtoto hawezi kuandikwa. Hata watu wanakuja hapa kiwajani tunaabiwa ya kwamba ni Taita district. Watu wametoka Taveta, wametoka Wudanyi, Mwatate, Voi na unakuta kwamba watu wote ambao eventually watachukuliwa ni wale ambao wametoka na barua ya minister, ama wametoka na barua kutoka juu pengine kwa Commissioner wa prisons, mtu mkubwa

pahali fulani mtu mwenye influence kama ni wa KANU pengine huku juu ndio ambao wanapata kazi. Hata mimi nimekwenda kwa interview ya police karibu miaka mitano sasa. Kila siku ikitangazwa, mimi huwa niko kiwanjani pale na watoto nachanganyikana na wananchi lakini unaona yakwamba wale ambao wanakuja kuchukuliwa eventually inakuwa ni watoto ambao wamekuja na barua, na form. Wengi si wa Taita, wametoka huko walikuwa recommended kwa hivyo wanachukuliwa. Wanachukua nafasi za Taita. Nikuonyesha ya kwamba tukiendelea miaka miwili, mitatu ama kumi ijayo tutakuwa hatuna Wataita katika police, au naweza kusema kwa vile anasema kwa Kenya nzima nasema ya kwamba tunakuwa hatuna pengine Wapokot huko, tutakuwa hatuna Wasomali huko, tutakuwa hakuna watu fulani. Yaani tunataka local people wawe presented. Tafadhali itokee ya kwamba tuwe na sort of quota system ili ionekane ya kwamba mtu anayeandikwa kazi hapa Taita ikiwa ni interview awe ametoka locally hapa Taita. Asiwe mtu ambaye ametoka nchi ingine, sehemu nyingine ya nch,i awe ametoka hapa maana ikiwa tutategemea wakubwa pengine sisi hasa hatuna wakubwa. Kwa hivyo tutakuwa hatupati hizi kazi. KPA imekuwa a very good example imekuwa na shida sana na KWS na police to mention those three.

Kuna hizi appointment – political appointments – Mimi nashangaa sana siku hizi inaonekana political appointment labda vile walivyosema, wasemaji waliokuwa hapa mbeleni wamezungumza wakisema ya kwamba powers ziwe (is it divored or whatever) zipelekwe kwa labda Bunge, ili appointment nazo ziwe placed equally kulingana na qualification. Maana kuna certain qualifications lakini kila mzazi hapa katika Kenya anapeleka watoto wake nursery, shule, mpaka university. Karibu watoto wengi sana hapa wamesoma na wengi wamefanya tarmacking, na kuna watu ambao waliacha kazi ambao walikuwa waneahuruwa lakini kwa bahati mbaya walikuwa pengine wamekosana na wale ambao wako politically rightly fitted. Kwa hivyo hawawezi kupata political appointment kwa sababu information inapelekwa na wale wale walikuwa nao. Tunaomba kwamba katika Katiba hii mpya tafadhali iangalie cases kama hizo ili iweze kurekebisha mambo fulani fulani. Kuna appointment za machairmen, ambassadors etc huo ni mfano.

Kwa upande mwingine ningetaka kuzungumzia jambo la nne na la mwisho ambalo ni mambo ya vyuo vikuu, universities. Pengine ningechanganya niweke universities, na teachers training colleges. Kwa sababu hapa, mtu akizungumza huwa zaidi anazungumza but mwamba ngoma hupitia kwake. Upande huu tuna shida moja. Shule moja ambayo ni nzuri sana Macommissioners mkiangalia hapa Taita iko hapa hapa nje. Ilijengwa pamoja na shule ya Makui Teacher Training College miaka kumi na zaidi iliopita. Nyingine iko Garissa, nyingine iko sijui wapi. Zilikuwa tano za World Bank. Na hizi zingine zote zinafanya kazi. Ya Taita haifanyi kazi na sijui ule mpango yaani watu wanaoiangalia kwa njia gani? Tumeambiwa kwamba hii college or institution ingekuwa constituent college of the university pamoja na Bandari college. Ifundishe theology na ifundishe tourism. Two courses. Lakini tumengonja kila mwaka, mwaka njoo mwaka nenda, mwaka njoo mwaka nenda. Hakuna kitu kinafanyika hapa. Tunataka kama haifanyanyiki, kama pengine hawawezi kufanya hivyo basi ni vizuri watwambie Wataita tuingie tufanye. Ikuwe na kipengere ambacho kinaweza kutukumbalia sisi tuingie hapo tufanye kama ni secondary school, kama ni nini, tutumie hio mali maana hata sasa ule ambaye yuko hapo ni mkopo wa World Bank kweli, lakini sisi Wakenya ndio tutakaolipa. Na tutalipa pamoja na ile ambazo zinafanya kazi. Kwa hivyo sioni ni kwa nini tukae na vitu ambavyo haziwezi kufanya kazi na hio nusu nusu kama vingine vimemalizika pesa za hapa Taita zilienda wapi? Maana bado haijamalizika, ukienda

unakuta milango sasa labda inaanguka na viti vinachukuliwa kwa hivyo tafadhali tuangalie utajiri wa nchi hii uwe spread equally. Kama sisi wa Coast, pengine Coast ni ndogo kwa province lakini tupewe ule undogo wetu. Kama ni 20%, 30%, 40% tupewe na sisi vile vile.

Kuna miradi ambayo ilikuwa miaka iliyopita.

**Com. Kabira:** Councillor uko karibu kummaliza?

**Roy Mwakadhi:** Namaliza sasa. Kuna mradi mmoja ambao tumeona hapa na haujazunguziwa hapa hata siku moja. Lakini kwa vile ni mradi unahusu wananchi wote na unahusu Kenya nzima, unahusu Central Government. Tumeona kuna miradi ambayo imefanywa. Kuwe na kitu ambacho kina-mention muradi ukianza na serikali kama hauwezi kummalizika. Kenya imekuwa na shida hio maana pesa zinapewa wale wanatumwa wanakwenda labda wanakura zile pesa, basi miradi inabakia. Tuna mradi hapa wa government haujamalizwa labda sasa ni miaka 20. Uko hapa unaitwa Insect. Insect is government project which has been there for the last 15 or 20 years. Na pesa zimetumika, zimemwagwa, yaani wanaanza badala ya kujenga nyumba moja iishe na ya pili iishe wanamwaga wanafanya mizingi karibu 40 ili wa-justify kura zile pesa. Kisha pesa tunaambiwa zimekwisha na hakuna kitu kinafanyika. Asanteni sana kwa kunisikiza.

**Com. Kabira:** Thank you very much councillor Roy. John Majana. Ako? 43 na akimaliza tuna Wakia Jumma. Hayuko? Na Clement Mzozo? Uko. Richard Mwangeka. Okey. Na KiBwana Mwakibingu? He has presented? Okey. Na Tony Mbololo? Uko. Na Patrick Masese. Kuna S.N. ameenda? Okey. Swaleh Mohamed na Gabriel Nyambo, Yuko. Allois Mwamburi? Ako. Hayuko. Okey. Kwa hivyo tutaanza na John Majana.

**John Majana:** Wana-Commissioners na wananchi nawasalimia. Langu la kwanza ni kuhusu Rais. Kuwe na sheria ya kumushtaki Rais ikiwa ameharibu mali ya serikali. Kwa mfano hapo nyumma tuliona kulikuwa na pembe nyingi za ndovu na silichomwa sana. Na huko tunasikia amenunua ndege. La pili Rais awe ni Rais na Mkuu wa Majeshi peke yake, asiwe ni Vice Chancellor wa University of Nairobi, Vice Chancellor wa Egerton university anawachia wananchi wengine ili wapate mkate wao.

La tatu Rais anapochagua mawazili, ma-ambassadors, ama chairman, lazima aangalie qualification kwa sababu ni kazi. Kwa sababu mwananchi wa kawaida pia anaulizwa qualification. La nne Tsavo National Park iwe chini ya Voi municiple. Kwa sababu ukienda Samburu National Reserve utapata mpaka senior sergent ni Msamburu mpaka yule mtu anakwambia pale kwa kambi ni Msamburu. Mimi mwenyewe nimefika. Ukienda Masai Mara kutoka kwa gate mpaka ndani unapata ni Masaai, huwezi pata Mkikuyu, huwezi pata Mjaluo, huwezi pata Mkamba wote ni kabila ile ile. Basi naomba Tume iangalie hilo jambo kuhusu Tsavo National Park iwe under Voi munciple council.

Na la tano nilikuwa nakataa majimbo lakini naona hapa majimbo inaingia kidogo lakini majimbo italeta shida nchini Kenya.

**Com. Kabira:** Asante sana John. Okey. Si hio ni maoni yake? Asante. Clement Mzozo.

**Clement Mzozo:** Macommissioner wapendwa, wakaaji wa Voi wapendwa mimi kama Clement Mzozo nina maoni yangu juu ya Katiba ambayo ningeipenda. Kupatana na vile tulivyopanda katika civic education, tumepata kwamba ile Katiba ilikwenda kuchukuliwa na baba zetu kule Lancaster house imepigwa viraka mingi sana zaidi ya viraka 30 kwa hivyo hio si Katiba. Tunapendelea kwamba Katiba ambayo tunahitaji sasa imuelekeze mwananchi kama number one na sio aweke number 7 ama number 10. Na pia napendekeza Katiba hii ambayo tunaazimia iwe Katiba inaelekea majimbo na iweke kwamba kutakuwa na majimbo nane, just vile Kenya ilivyo na province nane na Katiba ambayo katika jimbo kuna Bunge lake, kuna governer wake, na ma-judge wake ama wakuu wa sheria na kila kitu chake.

Mengine yameguziwa isipokuwa tu ningependa kwenda kwa uchaguzi. Naona pengine nilichelewa lakini wakati ule niliingia mpaka sasa hili jambo halijazungumzwa. Mimi ni mtu sasa wa miaka 50 na ingawa sikuwa mwanaharakati wa chama abacho kiko madarakani nimekuwa nikiona shinda sana kinaitwa KANU. Kwa sababu tumekuwa tukiona watu wa chini hawatendewi haki. Utaona mtu hajapata kura lakini ndiye anatangazwa kuwa mshindi. Mtu anakuja kutoka Nairobi ama Mombasa anakuja kununua uongozi. Naomba Katiba ambayo tunahitaji sasa mwananchi wa kawaida hapo mashinani ateuliwe kama ni councillor. Ateuliwe na wananchi wawe kutoka viama mbali mbali na hivi viama nimependekeza katika kila jimbo at least kuwe na vyama viine. Na nitavitaja hapa. Ningependekeza katika Katiba tutakayounda katika jimbo tuwe na vyama vine: chama cha ki-communist, chama cha ki-democracia, chama cha ki-socialist na chama kilicho na sera ya majimbo pia.

Basi nikiendelea kwa uchaguzi ni kwamba katika mahali watu wanaenda kupigia kura, kile kituo cha watu wanaokwenda kupigia kura iwe list iliyo na orodha ya watu. Hesabu ya watu walioandikisha katika kile kutuo. Halafu ionyeshe watu ambao wamepiga kura. Ionyeshe kura zilizoharibika na ionyeshe kura ambazo ni nzuri ni ngapi. Hivi kwamba hapo tutagundua ni kura ngapi, ni watu wangapi waliandikisha kura, ni wangapi walipiga kura, ni kura ngapi zimehalibika, kura zilizopigiwa Rais, kura zilizopigiwa mbunge, kura zilizopigiwa mayor ama diwani ama mwenye kiti. Sasa hio itakuwa rahisi kwa kuondoa ufisadi. Kwa sababu mara nyingi tunakuta ukiwa na pesa ndio utapigiwa kura kama huna pesa basi wewe haiwezekani upigiwe kura. Kwa hivyo tukiwa na kipengere kama hicho kwenye Katiba tunayohitaji ambayo imeweka mwananchi kama jambo la kwanza, ambayo ni Katiba ya majimbo, ambayo itatoa orodha kama hii, ukweli ufisadi ingawa hautaisha kwa sehemu fulani utakuwa umepungua.

Na nitaenda kwa haki za kimsingi. Haki za kimsingi hapa maoni yangu binafsi ni kila mwananchi wa Kenya awe na hewa safi. Tunataka katika viwanda kwa mfano hapa Taita Taveta viwanda via mkonge kuna wakaaji hapo ambao hawahudumiwi na yule tajiri ama mmiliki wa kile kiwanda. Kila wakati maradhi hata kwa watoto hayaishi kwa sababu ya hewa chafu. Sisi wakaaji wa Voi tuko hapa tumezunguzwa na National Park. Pollution imemzidi. Kila wakati mafua, because of pollution ya wildlife.

Ningependa katika Katiba tunayotaka sasa iangalie mwananchi awe na hewa safi.

Haki ingine ni maji safi. Nashangaa katika Katiba ilio mandarakani sasa haimuingilii yule mwananchi wa kule mashambani, Wanjiku ambaye anatoa maji kwenye mto ama Wakesho ambaye yuko mlimani anaenda kutoa maji kwenye kile kihindi cha Mwatate. Kuna public health officers ambao tungeonelea katika kipengere cha Katiba sasa kiruhusu, kwa mfano mimi natoka kule Taita mlimani. Kuna vichezo mingi juu. Kuna maji ambayo inaweza kuangaliwa kama ni mazuri for humman consumption na mengine yakaondolewa. Na hayo hayo basi yatengenezwe vizuri yatambazwe kwa wananchi. Hio ndio haki moja ya kimsingi ya mwananchi.

Nakuja kwa elimu – Naonelea hapa mimi nimeishia class ya saba na si makosa yangu kuishi katika darasa ya saba. Nilikuwa mtu hata wa kuniendelesha lakini hii 8-4-4, it is 8 – 4 – 4 = 0 kwa hivyo hakuna elimu kwa sababu mtoto wangu aliyekwenda secondary she/he can’t express himself in letter writing in English. Sasa tunaelekea wapi sisi Wakenya? Hio naomba hio elimu iliondolewa irudishwe ile elimu yangu nilisoma ya 7-4-2-3. Hiyo ndiyo haki ya kimsingi.

Haki ingine ya kimsingi na hapa nitaongea kama Mtaita. Mtaita asili ana tamaduni zake na ana dini yake. Pengine singependa kuwalaumu wazee wangu kwa sababu ya kushika biblia sana lakini walituharibu kwa kutupeka kwa ma kama kuitwa Clement, bila kutufundisha utamanduni wetu uko wapi. Lakini mimi kama msomi wa biblia na unatamaduni, ninajua kweli wazee wangu walikuwa na dini zao. Na dini zao zingine zilikuwa za kutumia maji, dini zao zingine zilikuwa za kutumia pombe zinaitwa mfungande. Ni sawa kwa Wataita? Naomba kipengere cha Katiba tunayohitaji iheshimu dini na elimu ya kimila, sherehe za kimila, kwa mfano kuwapa wasichana wetu kuwaondoa kutoka utoto kuingia utu ukubwa, ama vijana kutoka utoto kuingia utu kubw. Hizo tamaduni siheshimiwe na ikiwezekana baba zangu waketi na sio tuweke biblia kado, kwa sababu utamaduni na biblia zinaambatana. Pengine niwapatie theological mathematics. Theological mathematics equals 2, tradition, less witch craft, add Jesus Christ equals to African Christianity.

Naja tafadhali mtaniwia radhi kwa dakika tatu tu niingilie mambo ya mipaka ya hapa Pwani. Pwani sisi ni masquatter wa watu wa bara na mipaka yetu kule Mtitu wa Ndei imenyakuliwa kule Makueni district. Mipaka sasa hatuko, ile Mtito wa Ndei haiko Taita. Na ngoma la mzee (in Kitaita). Hapa Macknon Road na nilikwenda miezi miwili iliopita kufanya utafiti kabla hamjakuja wale wanaishi kule ni Wataita asili na wengine wametoka location moja ya kwetu, wakahama huko. Hata mzee mmoja alikuwa hapa ambaye wazazi wake walihamia huko. Lakini wanaambia sisi ni Kwale district hatujui kwa nini. Na jambo lingine, na hio iwekwe katika Katiba, ile mipaka ya zamani irudishwe kusudi Mtaita awe na haki yake. Na jambo lingine la mwisho naomba Mtaita hawezi kuwa maskini nchini kwake na mtu wakuja aje kutajirika Taita. Utajiri wetu ubaki kwa Wataita. Asanteni sana.

**Com. Kabira:** Asante sana. Tuna Richard Mwangeka.

**Richard Mwangeka:** Asante sana Commissioners walio mbele hapa na wananchi, hamjambo? Mimi kwanza niko na vita na

hii Tume. Ati wanaongeza mda wa miezi minane? Na hio miezi minane will cost 0.5 billion ambapo mwalimu analia kulipwa pesa ambazo zilikubaliwa na serikali. Naomba hivi ndugu zangu, mkirundi muambiwe Pal Yash Ghai, Mwangeka amesema pesa hizo zilipwe walimu phase II.

Ya pili, kumbukumbu la Torati, mlango wa 32, kivungu cha kwanza mpaka cha kumi hapo ndani inasema hivi, "Mwenyezi Mungu aliumba kila taifa na mahala pao." Taita Taveta, Kwale, Kisumu, Kajiado, Kiambu, Nyeri kuna nani hapo? Lakini sisi tumekuwa watu wa kupokea tu. Twapokea tu. Nataka Katiba iandikwe hivi, wakati wa kupiga kura, kura ipigwe na Mtaita mwenyewe peke yake. Peke yake kwa sababu huyu mtu aliyekuja hajui Mwangeka yu aishi vipi, hajui candidate huyu yuko vipi, yeye achangia tu kupiga, kutuharibia, ndio sababu hakuna maendeleo Taita Bwana. Hakuna maendeleo kabisa. Because we have leaders who cannot even speak. Umeskia tuna tenure of office miaka 10 na bado vile hakuna viongozi wa kuzungumza. We have a whole minister, foreign affairs, wengine, wengine.

Jambo lingine, kama ni mimi there should be no political parties in Kenya kwa sababu viama hivi vingi vimekuja ni vya ukabila. Kwa sababu ninavyosema hivyo ni kwamba vyama vingine vime-instil fear kwa wengine, kwa wapiga kura. There should be no political parties. Sasa kama ya kuua politial parties here, kuwe na registrar of political, wawe na chama chao cha kuandikisha sio the registrar of societies. Bwana Obaga unatumiwa tu kuumiza wengine.

Powers za President – Ningependa kusema ukweli kwamba powers hizi zipunguzwe kwani tumeona madhara na tumeona ukatili unaotumika katika mahala mbali mbali, uteuzi. It is very funny nimesema sitaji majina lakini how can a prosecutor become a Chief Justice, a prosecutor. Hio si mzuri, si mliona au haikuwa hivyo. Alikuwa kwa prosecutor alikuwa kwa mkubwa akarudishwa prosecutor, prosecutor akawekwa Chief Justice. Hizi ndizo powers tunaona zinatumiwa vibaya. Ni wapi nchi gani uliona kuna wizara mbili katika mawazili wawili katika wizara moja? Si ni Kenya peke yake, that is misuse of power. Kipengere kingine kiandikwe kwamba katika Katiba inayokuja kila wizara itakuwa na minister moja.

Vagrance act – Tunataka hii Vagrance Act ilegezwe. Kuna watu wamefanya uhalivu kwingine wamekuja hapa wametuletea shida kweli kweli. They are jail birds, akifungwa cha yu arudi ndio afanye makosa tena. Wakisha fungwa tena wapelekwe nyumbani kabisa walipoti kwao huko. Tumewachoka watu zambuli hio.

Provincial administration ni haifai hapa Kenya. Isiwepo kabisa, hivi sasa ninavyozungumza wako an mkutano, sisi tuko na mkutano hapa, wao wako na mkutano Mbirikani. Wale watu ambao walikuwa supposed kuja hapa kupeana maoni hawatapeana maoni au watapeana? Kuna mkutano kule opposite wa DC. Wasiwepo kabisa hawa ndugu hawa. Ndio wameweka shida zote za land.

Mambo ya pollution sitazungumza hapa kwa kweli kuna sheria iandikwe ama kama ipo itumiwe. Ndugu zetu hawa pollution imezidi. Juzi nikapelekwa kotini wamekuwa fined 100 shillings. What a shame! Shilingi mia moja. Kampuni ilipigwa kotini.

Hapa wengine hamjui, mimi najua. Unajua mimi ni watchdog, naangalia kila pahali. Nikizungumzia haya mambo ya sisal Estate kwa kweli ililipiwa pesa zamani za kale Decemba tarehe 4 mwaka wa 64 zililipiwa. Mwanyumba wakati huo marehemu alikuwako waziri wa works. Aliendа akachukua pesa huko (young brothers) akaja akalipia zote hizi haya makonge haya. Lakini mpaka leo ndugu zetu wangali wanaimiliki, hujui lease itaisha lini, they have conspired with the government. Wanaanza kuuza sasa, mimi nashangaa kumbe lease huuzwa? Iko hapa inauzwa 6.3, sijui 3 million. Mtaita tutanunua hio shamba kweli?

Nikiianza na wenzetu Bwana Commissioner mlemavu ambayo yametatiza lakini hata hivyo tunataka tuwe na Constitutional Court. Court ye Kikatiba. Hio itatufaa sana katika mambo yetu, na zaidi ya yote, tungetaka kuwe na vivungo vya Katiba. Sijui ndugu yangu Julius Kabarare alitumia vipi akasema watu wawe na kilimo cha kufa na kupona. Na kweli walipona bwana, walipolima wao. Sisi hatulimi, hapa twangojea mahindi ya msaada tu. Kwa hivyo haya mahindi ya msaada yanapokuja kuweko kifungu katika Katiba haya yaje watu wapewe lakini wafanyie kazi. Si kupea hivyo yanje lakini watu wafanyie kazi.

Vile vile ningeomba elimu iwe bure na iwe ya lazima. Mwish kabisa walio na shuku ya majimbo, majimbo yanakuja wataka hutaki. Kwa sababu ndio tumeona ndio suluhisho la watu wa Pwani na wewe uliohapa ni mavani. Sasa kama hutaki uanze kuondoka mapema kwa sababu itakuja majimbo.

Ya mwisho, uchaguzi wa mayor, madiwani na deputy mayors. Nafikiri tungependa yawe challenge. Wananchi wenyewe wachague, ili kuondoa ile mambo ya u-councillor ndani kwa ndani pale. Na vile vile Bwana Commissioner kama sheria hii iko, we don't want commercial politics. Sheria iandikwe watakaoshikwa wakihonga, kwa sababu imekuwa ni commercial politics siku hizi, watu kununuliwa tu, mia tano, mia mbili, unga wa mahindi kilo mbili, this is mockery, yaani shida tu. Ningependa kwa sababu umekuja hio sheria iandikwe.

Mwisho kabisa ninashaka na Commission hii. Commission hii wamenaza mapambano, kupigana. Yash Pal Ghai ako na kikundi chake sijui na mwingine ni nani simjui. Sasa tuna uhakikisho gani mambo haya yataenda, kwa sababu tumeona Commission nyingi sana Kenya. Zachukua vizuri vizuri bu. Unaenda state house unakura ugali, kwisha. Twataka tuhakikishiwe ya kwamba maoni haya tunayoandika kwa kweli yatatumiwa na tutakuwa na Katiba mpya. Ukweli ni kwamba kwafanywa Bill nyingi sana. Hata hawa civic education providers walipita pita hapa na kama nilivyomwambia juzi walipata wananchi wamechoka. Wanaitwa, hawaendi. Ndio kwa maana unaona kila jamaa akiingia yu aenda zake, huyu akija yuapinga hii. Kwa sababu tangu uende hatujakutana kama Wataita Taveta. Hatujakutana. We have no leaders to keep us together au nasema ulongo. Hatujakutana. Ndio kwa maana ukisikiliza kila mtu asema hili, asema lile, asema hii. Kwa hivyo shida yetu ni kukutana. Ningeomba Kamati hii kwa sababu mnakutana kutana huko tunalaumu viongozi wetu. Mimi binafsi nandika barua kwa major, mwana Wakiringo yuko hapa waite leaders meeting at least one day to discuss about Wataita. Lakini hakuna naabiwa sisi, we are opinion leaders. Sasa tunatakiwa tuwafunuliwe siri. Kwa hivyo sijitetei lakini ni kwamba matatizo ya ndugu zetu wanaogopana. Juzi tulikuwa kwa DC, DC akasema nimejaribu lakini nimeshindwa na hawa ndugu zenu, because mayor cannot sit with Mbela but Mwakiringo can sit with everybody. Hapo ndio nilipata kidogo nafuu. Kwa hivyo tunajaribu.

Sasa shida zangu utanijibu ama vipi? Kwa sababu nina wasiwasi na Commission hii. Tena mtapeleka mambo wapi Bungeni. Sasa wabunge wakipitiza hii 0.5 billion muendelee nafikiri wabunge wamekosa kazi au mnasema aje wananchi? Yes. Thank you.

**Com. Abubakar:** Asante sana Bwana Mwangeka, lakini nyinyi mwajua Bwana Mwangeka mchokozi? Ataka tu niseme tu.

**Public:** Sema tupumue na sisi.

**Com. Abubakar:** Leo sina la kusema kazi yangu kupokea maoni lakini kwa ufupi tu kwamba nadhani nilipokuwa hapa nilizungumzia maswala haya haya kutokuaminiana, na watu kuwa na shaka, sijui kazi hii itaenda mbele au itarudi nyumma maoni yetu yatadhaminiwa au yatatupwa jalarani. Mambo haya nafikiri tushaa rudia mara nyingi. Ningependa kusema mawili tu. Mawili peke yake.

La kwanza kuhusu kuongezewa mda, kaguzia Bwana Mwangeka na la pili kuhusu maoni yetu sisi wananchi yatachukuliwa na yatumike kuunda Katiba mpya au hayatafanyika hivyo? Kwanza sisi tumetoa, nilipokuwa hapa nilisema tutakutana tuamue habari hii ya mda. Kwa hivyo sikuwa nimendanganya Bwana Mwangeka nilipokuwa hapa tutaongezea mda na tutoe shauri, tumekata shauri tumewaeleza Wakenya kwamba mda uliombakia kupitia October hatuwezi kummaliza kazi hii na kulingana na uzoezi wetu wa kazi na tajiriba tuliyoipata kutokana na kazi tuliofanya na wananchi wa Kenya inatueleza kwamba kila hatua iliyowekwa katika sheria na wabunge, ukifuata kila hatua itachukua mda huu kwamba ikiwa hatutahitaji kura ya maoni tunaamini tweza kummaliza kazi hii kufikia March mwaka ujao. Ikiwa kutahitajika kura ya maoni yaongeza miezi miwili ambayo itatumika kutayarisha na kufanya kura hiyo ya maoni. Sasa Bwana Mwangeka akisema tupunguze hizo sijui anataka tukate wapi. Tukate tuseme leo tutakutana hapa asubuhi tu mpaka saa sita halafu kuanzia saa saba tuende pande ile ingine mpaka saa kumi twende zetu. Mambo ya kukata vichochoro yatatuharibia Katiba. Katiba lazima ifanyike kwa mipaka iliyowekwa katika sheria. Sijui kama tunaelewana. Sisi tunasema hivyo kwa sababu tunaelewa sheria na tumetumma obi letu Bunge hatujiongezei mda sisi wenyewe. Tumetumma obi letu Bunge, na mbunge wetu hapa Bwana Mwakiringo atakuwa mmoja kati ya wabunge watakao kaa chini kuchunguza maombi yetu na sababu tulizozitoa zikiwa zina maana na zinaingia akilini, watatoa uamzi kutuongezea mda au kutotuongezea mda. Kwa hivyo tungonjee mashauri ya wabunge watasema je.

La pili kuhusu maoni ya wananchi wa Kenya, sheria inatulazimu sisi kujenga msingi wa Katiba mpya katika maoni ya wananchi wa Kenya. Ndio tukasema tusaa kuja kuchukua. Na nadhani tuanze kuaminiana kwa sababu tukishaanza kutoa ahadi, Bwana tutarudi siku fulani kuja kuchukua maoni, si tumekuja? Basi imani iongezeke kidogo. Isiwe kama wakati ule mwingine kila tukitimiza ahadi moja imani iongezeke. Lakini mkiwa mnataka mtu ambaye atasimama mbele yenu na mimi mwajua mimi mtu mmoja wa Pwani, ikiwa atasimama mbele yenu aseme mimi nina hakikizo la kuwapa nyinyi kwamba tutapata Katiba mpya, huyu anachukua mamlaka ya Mwenyezi Mungu. Mimi sina hata hakika kwamba nitatoka hai hapa. Nikienda kurala pale kwenye hoteli asubuhi nione nimeamka bado ni hai, na nisipokuweko itakuwa nini? Naweza kuwaambia kesho niko hai mimi?

Ndio nasema kuambatana na haya mahakikisho tuyafanye mahakikisho ya kibinadamu kwamba Bwana Mwangeka ukiamka asubuhi wewe watuulizia Katiba imefika wapi? Ukienda kurala watulizia Katiba imefika wapi? Ukiniona mtaani nisimamishe tuyazungumze haya. Hatuwezi sisi kama Tume kulijenga Katiba mpya peke yetu. Sheria inatulazimu na majukumu yetu mbele ya Mungu, tulikura kiapo mbele ya Mungu na wananchi wa Kenya. Nasema tutilie maanane na tudhamini maoni ya Wakenya. Na tukisha andika report yetu, itarudi kwenu mwangalie, je yale yalioandikwa pale ndio yale mlioyatoa? Ikiwa haitafanyika hivyo hapo ndio mtulize maswali lakini kwa sasa jamani, maoni yanje tena kwa funjo na wingi wala sio funjo ya kuzuia wengine lakini maoni yawe yanatoka na kuongezeka. Mpaka sasa list yetu imefika watu 208. Sisemi hio ni mbaya nasema ni nzuri na wengine wanasema tutaje majina kama kumi wajue kama wako karibu. Hayo nitamuachia Com. Kabira. Asante.

(Inaudible question from the public)

**Com. Abubakar:** Mambo mawili ndugu, kwanza kusema kwamba sisi haRamu si kweli. Sisi tumepitizwa katika sheria Bungeni ndugu yangu. Sheria chapter 3A ya Constitution of Kenya Review Commission ni sheria inayotumika hivi sasa. Kwa hivyo ni sheria iko inayotumika. Pili mambo ya entrenchment ni kuhusu ungumu wa Tume hii kuondolewa kisheria. Haya muulize Bwana Mwakiringo yuko hapa mheshimiwa. Hoja hio bado iko Bungeni hata yeye hafai kuizungumzia iko Bungeni tayari. Wewe una wasiwasi wa ubatiti wa sheria, na unataka nizungumzie mambo batili ambayo hayaruhusiwi. Hoja iko Bungeni. Kwa hivyo ndugu yangu subira, subira hufuta heri taratibu mambo haya. Maoni jamani. Najua kuna wengine wanataka nizungumze lakini si leo, maoni naona.

**Com. Kabira:** Asante sana Com. Abubakar. Tulikuwa tumetaja jina la mheshimiwa Mwakiringo na ninaona amerudi. Tumpatie wakati? Okey, asante.

**Mheshimiwa Mwakiringo:** Asante Com. Kabira na Abubakar. Mimi nikutoa chagizo zangu na mengine kuzizitiza yale ambayo wenzangu watakuwa wamezungumzia. Na nifafanue kidogo, sitaki kuwatetea Macommissioners, lakini muelewe kwamba mda ambao tuliupitiza Bunge wa Commissioners kufanya kazi, walichelewa kwa mwaka mmoja na nusu wakizozana baina ya kamati ya Bunge na ile ya Ufungamano. Sasa mda huo ulipotea na bando ndio walikuwa wanaomba kama wanaweza kuongezewa lazima tufikirie kwa laini hio.

Pili tusiwe na haraka mnakubuka Uganda wamefanya hivyo na sasa wamerudi nyumma wakasema hapana tulifanya haraka tulifanya makosa sasa wamerudi nyumma kuanza kuandika Katiba mpya ambayo inakuwa ni ghalama zaidi. So sitaki niwatetee lakini mchukue kwa njia hio. In any case tunaulizana hivi, ikiwa tumekaa miaka hio 39 bila Katiba mpya, miezi tatu, nne ndio kungonjea basi ndio imekuwa shida? Basi nirudi kwa maoni.

Kwa maoni yangu ni kwamba jambo la kwanza. Uongozi ni kitu cha muhimu na ningependekeza Katiba iandikwe ikisema kwamba, yeyote yule ambaye atataka kuwa diwani, mbunge, Rais na chochote ni lazima awe na familia iliyo imara, must have a

steady family kwanza, uwe umeoa. Hatutaki kiongozi na watu ambao hawana mabibi nyumbani, ama hawana maBwana. Maanake ikiwa haujanielewa na mtoto kwa panja, hutajua kama ninakatwa ama huwa nimepanguzwa, lakini ni lazima uwe na family. So for one to be leader either MP, councillor or President, you must have a steady family.

Number ya pili ambayo ningependelea ni kwamba mambo ya ardhi. Ardhi iwe ni ya wenyenji wa pale. Iwapo utakuja unataka ufanye biashara basi upatiwe nafasi ujenge nyumba peke yake lakini ardhi iwe niya pale. Siku ile umechoka uiuze hayo, lakini ardhi iwe ni ya wananchi wa pale na mtu asipate title deed kwa ardhi ya wananchi. Pata title deed kwa ile nyumba ambayo umejenga pale peke yake. Tatu, Katiba iseme kwamba maofficer wa serikali maDC na maDO na machief wasihusike. Tukiwa hapa tutakuwa wakarimu vile Mwangeka amesema, lakini ikija mambo ya uongozi wa kuchaguliwa, basi wenyenji wa pale waachiwe uchaguzi, wenyeji wa pale ndio wawe wanasimama kwa viti hivyo. Nyinyi ambao mmekuja kufanya mabiashara na mambo mengine, muwe wa kusaidia peke yake kupigia mwenyeji wa pale kura. That is all, but otherwise wasisimame watu wengine kutoka nje. Wawe wasaidizi tu wa kupiga kura manaake bibi ya pili hawezi kuja kaingia kwa mji ule akafukuza wa kwanza (in Taita). Bibi wa pili hawezi kuolewa aje atoe bibi wa kwanza “aa mimi ndiye alishauliana na Bwanake ndio wewe ukapatiwa nafasi ya kuolewa,” maana huyo wa kwanza angekataa hungeolewa. Kwa hivyo nyinyi ambao mmekuja tufanye na nyinyi biashara, na nini, muwe wa kusaidia peke yake katika kupiga kura lakini ni lazima wenyenji wa pale wasimame katika viti hivyo vya kugombaniwa.

Nne, kuwe na uhuru wazi bila kusubuliwa kwa vyama vyote vya kisiasa. Ni aibu kuona kwamba Kenya yetu hii tangu tuingie mvumo wa vyama vingi, bado utasikia vile mwenzangu musemaji wa mbele alisema, wajumbe, madiwani viongozi wa vyama wanaenda wakisumbuliwa hata na askari kifaragha tu kwamba tumesimamisha mkutano wako kwa sababu ya kiusalama. Ni wakati gani unatakikana ujulikane usalama uko ama hauko. Ikiwa mkutano umeitishwa na wananchi wametoka na ni kuzungumzia, kaa pale ulinde wananchi wa pale. Kwa hivyo there must be freedom of all political parties.

Ya tano, mwananchi wa Kenya asisumbuliwe wakati anahitaji kitambulisho. Kwa sababu tunajua kwamba mtoto akizaliwa huwa anapatiwa birth ceritificate immediately. Hio birth certificate ningependelea copy yake iwe inapelekwa kwa registrer of persons ili mtoto huyo akifikisha miaka 18 na kwa sababu tumeingia katika computer age, iwe ni rahisi akiomba maombi computer inaonyesha ulizaliwa date fulani, wakati fulani birth certificate apate identity card na anapopata identity card itoke pamoja na ile ya kupiga kura badala ya kuingiza ghalama ya kitambulizo kwanza halafu kura baadaye. Zitoke pamoja wakati mmoja.

Sita, ni vyema kwa sababu nchi yetu hii ya Kenya ina matatizo balibali kulingana na mazingila ya sehemu bali bali. Kwamba hizi local authorities serikali za wilaya sipatiwe fedha kutoka kwa Serikali Kuu kwa kutekeleza mambo yao katika sehemu hio. They must be funded from the Central Government to exercise and do their project at their local level. Na hiyo nadhani itakuwa ni sehemu moja ya majimbo. Lakini tunapozungumzia majimbo ni lazima yaelezwe ni majimbo ya kufukuzana au ni majimbo ya kiuchumi. Tusiseme tu majimbo kienyeji ni lazima yafafanuliwe, it must be explained.

Saba, vile nilivyozungumzia nikasema kwamba ardhi lazima iwe ni ya wenyeji, ni kwamba hata hiyo lease. Lease ikiwa iko ya miaka 99 miaka 999 ya miaka 10, ya miaka 20, hiyo miaka ikiisha ardhi hiyo irudishiwe wenyeji wa pale wanamue wantaka nini. There should be no extension unless wananchi wameulizwa wa sehemu ile waseme tunataka huyu mtu aendelee kukaa kwa ardhi hii au la. Hio lease ikiisha, imeisha. Biashara iishie hapo na ardhi hio irudi kwa wananchi.

Nane, vile tumesema nchi yetu pia ina raslimali nyingi ni kwamba sehemu yetu hii ya hapa pesa zitengwe za kuwezesha wale ambao wako katika sehemu ya maadini waweze kusaidiwa katika utafiti, prospective, na pia katika kuchimba maadini hayo. Na ikiwa raslimali hizo ziko hapa Taita Taveta yeyote ambaye ajae kutoka nje whether ni Mkenya kutoka sehemu ingine ama ni Mzungu ama ni nani, 51% katika kampuni hiyo ambayo itakuwa ikifanya hapo iwe ni ya wenyenji wa pale pale. Our local people must be involved. Isiwe ni Mwakiringo ameregister kampuni yake huko basi ni kuje kuingia na wenyenji wa pale vijana wa pale tunawaacha wakiwa pale. Lazima wao nao pia wawe na share holding kwa sababu ya ardhi yao ile ya pale.

Tisa, kwa upande wa walemavu, wamezungumza mambo mazuri sana I have liked their presentation lakini ningependelea hivi. Kwamba na kufunguliwe ofisi katika ofisi za chief au za maDO za kuweza kuwasajiri wale walemavu so that wajulikane wako wangapi na wale waofficer wakuu ambao wanashughulika na mambo ya walemavu waweze kuja na kuwatembelea katika zile sehemu ambazo walipo. Na mzazi ambaye ana mtoto mlemavu ambaye hakujiadikisha ama hakuandikisha mtoto huyo achukuliwe hatua kwa sababu, kwa nini anaficha na huyu mtoto ana haki ya kuishi manaake aliletwa duniani na Mwenyezi Mungu?

Na mwisho ya kumi ni kwamba uteusi wowote ule uwako ni wa mashirika mbalimbali ya serikali kama Permanent Secretaries, parastatal chiefs, majudges na wengine. Hiyo ni lazima mapendekezo hayo ya majina yapelekwe Bunge ndio Bunge iweze kupitisha kulingana na tabia ya mtu vile mtu mwingine alivyosema tangu alipokuwa akitambaa. Tujue tambia zake. Maanake Kenya ya sasa wakora ni wengi vile wale walemavu walisema. Wengine ni rapist, wengine tabia mbalimbali na bando unaona ndio anawekwa kwa ofisi kubwa. Lazima ataendeleza mambo yale ya uongo alikuwa akifanya kwa sababu hakuna sheria inachukuliwa. So ni vizuri majina ya wale ambao wanataka kuteuliwa yapelekwe Bunge yawezwe kupitizwa na Bunge ili wajue kwamba wako accountable kwa wananchi. Nimesema asante, na ningesema. Mda ulikuwa mfupi wa civic education haikufika ndani sana watu wakaelewa. Ndio unaona bado, lakini nashukuru watu wamejaribu kufika. Wamepata ukakamavu kidogo lakini mda ulikuwa ni mfupi bado na Civic Education Providers ambao walikuwa wakifanya hiyo were not properly funded to reach the interior. Asanteni sana. Thank you very much.

**Com. Kabira:** Okey asante, mheshimiwa utajiandikisha, asante sana. Nitataja watu kumi.

(Inaudible communication from the public)

**Com. Abubakar:** Swali langu sijui kama limefikia mheshimiwa ambaye nilikuwa nataka atufafanulie hii. Yeye hapa amesema habari ya majimbo, sasa ndio nataka muelewe je aunga mkono majimbo ama hayuko katika majimbo, manake masikio sikusikia hayo.

**Mheshimiwa Mwakiringo:** Nimesema serikali za wilaya zipatiwe uwezo kwa kupatiwa fedha kutoka katika Serikali Kuu ili ziwe na uwezo wa kutekeleza miradi yao katika kiwango chao, kwa sababu hao ndio wanajua shida za wananchi. Na nikasema hio ni mfano kama wa majimbo. Lakini nikasema kwamba majimbo naye yafafanuliwe kama ni majimbo ya kufukuzana au ni majimbo ya ki-uchumi. Kwa hivyo anayezungumzia mambo ya majimbo, ni lazima afafanue hayo aingie kwa mwananchi so na mimi siwezi kuamua ninaunga mkono ama siungi mkono na bado zijazungumzia. Ni kama msichana kumuuliza utanioa na hujamtongoza bado, nitasema je mimi?

**Com. Kabira:** Asante sana mheshimiwa. Tuna Tony Bololo. Patrick Masese na after that tuna Martha Kigandi ako? And then Gatrude Wakesho. Getrude yuko? Hayuko. Halafu D. Kizalo, I think he is a councillor. A.G. Mwaloma. S. mwandawilo, David Makanga, Marian Mwagugu, hayuko, Gladys Wacara, hayuko, Amina Swala, hayuko, Paul Okala, hayuko. Peris Lusaka, hayuko. John Mojale sorry John Mojale yuko lakini hazungumzi, huyo mwingine ni Shilingi, Shilingi yuko, Amos Moramba, hayuko, James Mwangombe, ametoka. Kwa hivyo tunarudi kwa Tony.

**Tony:** Macommissioner, wananchi je hamjambo? Nitakuwa nikizungumza juu ya my views lakini utakuta kwamba yale nitazungumza labda nitayarudia kwa sababu yamekwisha semwa na wenzangu lakini kwa vile ni views zangu, nita-mention, sitatoa kwa kirefu. Zingine nimeandika kwa ile language ya Kimombo kwa hivyo nitawasomea kwa Kimombo vile vile nimeandika.

Kwanza kabisa nina-recommend majimbo na mimi nasema majimbo system so that more powers are devolved to the municiple and county council.

Pili nazungumzia juu ya appointment of ministers, assistant ministers, permanent secretaries, ambassadors, and so forth. Those high ranking positions. Maoni yangu ni kwamba appointment hizi sikifanyika zipelekwe Parliament ili ziwe ratified.

Powers za President naomba zipunguzwe. Yaani President ambaye atakuja tawala Kenya asiwe above the law. I am recommending that the President commits a political offence or otherwise he should be subject to impeachment, na term yake mimi na-recommend iwe for 10 years only.

Appointment of Judges – Judges should not be appointed by the Executive. They should also have a security of tenure. Their appointment should be recommended by the Judicial Service Commission and ratified by Parliament.

Land – All the land which lies under county council formally known as State Land should be transferred to Trust Land so that it falls under the jurisdiction of the county council.

Presidential candiditure – Presidential candidature should rotate to all the 42 tribes. Sijui kama mmenielewa.

Nominations of MPs and councillors – There should be no nomination of these positions. All MPs na councillors should be subject to election, ama vipi?

Natural resources – Naingia kwenye mawe sasa. Indigeneous citizens of Kenya should own the natural resources. Any mineral below 3 feet from the surface should belong to the indigeneous citizens of Kenya who own that particular piece of land.

Kwa haya machache ningetaka kuongezea mambo ya National Park. Tungetaka tusaidiwe na hii National Review na hii Constitutional Review kwa sababu sisi Wataita hatukuchagua kuzaliwa na wanyama. Tulikuta, baada ya kuzaliwa, tulijikuta tuko na wanyama wetu. Na hio ilikuwa sababu fulani Mungu akatupanga na wanyama wetu. Kwa hivyo tunaomba kipengere kiwekwe pale ya kwamba hizi national ambazo ziko na wale watu wenyenji, sirudishwe kwa wenyenji. Tunaomba hii Tsavo, sisi turudishiwe Tsavo yetu kwa sababu ukiangalia wale wanyama walikuwa kwa hii National Park walikuwa wengi sana. Wamekwisha pungua. Wamepungua kwa sababu wale ambao wana-run hii National Park hawako committed. Na hii tukipewa sisi iwe under county council tutakuwa sisi tuko committed tukijua kwamba watu wetu watakuwa wameajiliwa kazi pale, watalinda hio National Park, tutakuwa na commitment, na hawa wanyama wataongezeka. Kwa sasa unaweza kuingia kwa hio National Park usione hata simba. We are actually now conning the Mzungu. Wanaingia hapo kuona simba, hakuna simba, hakuna ndovu maanake ndovu wamesaa uliwa na watu ambao wameconspire na officials Bwana wakazimaliza. Sasa we are being robbed our own animals. Sisi wataita tunaibiwa wanyama wetu. Lakini tukipewa mamlaka ya hio National Park.kama vile kijana mmoja alikuwa amesema hapa akasema sungusungu alisaidia hapa Voi akasaidia police, ni kweli kabisa. Sisi tutaweka sungu sungu kule. Tutaweka sungu sungu ama si kweli? Nashukuru asante.

**Com. Kabira:** The rotational President, how do we rotate?

**Tony:** Nataka i-rotate namna hii. Kama Kabila fulani imekwisha tawala, imekwisha. Haiwezi kurudiwa tena. Kama alizatawala Kikuyu hio term yao ilikwisha. Kama alikua Mkalenjin term yao imekwisha. Sasa tunangonjea term ya Mtaita, Mswahili wa Taita, Mswahili wa Mombasa na kadhalika.

**Com. Kabila:** Asante. Na huyu meingine ni Patrick Masese.

**Patrick Masese:** Bwana Commissioners asante sana kwa kufika hapa Voi kuja kusaidia watu wa Voi na mkoa huu wa Pwani. Sisi kama kuna watu wamenyanyaswa ni Wataita ndio wamenyanyaswa sana watu wa Pwani. Kwa sababu watu wa

Pwani tumelaliwa sana na watu kutoka juu. Hata tunaposema mambo ya majimbo naipenda sana majimbo hata ukisema inakuja kesho tunafurahi kwa sababu sisi majimbo yetu si ya kufukusa watu. Nataka mwenye kujenga nyumbake akae hapa lakini aelewe yeye yuko chini ya Mtaita. Asiwe yeye ndiye anafanya sheria zake, apana. Sisi kwa upande wa land kwa hakika tumelaliwa sana watu wanatoka Nairobi wanakuja na barua hata labda ni ya uongo, si ya kweli lakini inanyanganya mtu shamba lake kusudi ati yeye amepwa title deed. Kila tukisema tunataka tuone ule mwenye kutoa title deed ni nani, tunazunguzwa hivi, tunazunguzwa hivi hutampata kumuona. Kwa hivyo tunataka, sheria hii ya leo, Katiba hii ya leo mtu asitoke Nairobi kuja kupata ardhi Voi kabla watu wa Voi hata wenyewe hawajui, aje aketi na council, apitie kwa council aidhinishe ndio apatiwe hio plan. Yaani asiwe anapata land kwa kununua na pesa zake na kutoka huko. Apana. Nataka Katiba hii ya leo isaidie sana mwananchi wa kawaida hana zile nguvu.

Ile mambo ya kutoka Nairobi twataka kusema kweli sisi tuna wazee wetu hapa hata akifika Nairobi anashindwa ni wapi maofisi gani ataingia kuchukua hio barua ya land. Barua zetu ziletwe Mombasa, tupatiwe hapa Mombasa, ofisi zetu ziwe hapa kusudi tupate mtu kuteremka mara moja na kuchukua barua yake. Lakini mambo ya Nairobi nasema sisi hatuwezi, kwa sababu ni wanyonge sisi. Katiba hii iwe ya maskini. Iangalie maskini, isiwe ya matajiri peke yake. Kwa sababu Katiba iliyopita ilikuwa Nairobi, ina Katiba yake, ukiteremka kidogo ukifika Mtito ina Katiba yake, tukifika Voi city ni ile maganda madogo tumesikia. Hata vile tukisema hatuzikizwi wala hatujulikani sisi tunasema nini. Naona mtu ametoka Nairobi, anakuja kufika Voi basi ni Bwana mkubwa. Sasa sisi tunabaki tukisema huyo Bwana mkubwa ametoka nchi gani? Kwa hivyo tunaomba Katiba ya leo isijali maslahi ya wanyonge, wale ambao ni wanyonge kabisa. Afikiriwe kama Mkenya mwingine, na sheria ikiwa ya Kenya ama Katiba iwe ya Kenya iwe katika Kenya yote, isiwe kwingine, inafanya zingine na kwingine inafanya zingine. Kwa hayo machache mengi imesemwa na wenzangu hasa kuhusu mambo ya land sisi tumeumia sana juu ya land. Kwa hivyo asante sana.

**Com. Kabira:** Asante sana Bwana Masese nafikiri DO ameingia. I would like to recognize his presence. Did you want to say something Bwana DO? Okey. Martha Shighachi.

**Martha:** Tume yetu, wananchi hamjambo? Jina langu naitwa Martha Shighachi mimi nimeanza na ya kwanza.

**Com. Kabira:** Martha tafadhali tumia microphone.

**Martha Shighachi:** Ninaanza na hii Chief's Act. Mimi ningependa kuambia Tume hii ya kwamba hii chief act ambayo iliondolewa inatufaa sana. Nikieleza ni kwamba Chief Act ingechukuliwa pamoja na mzee wa mtaa kwa sababu mambo mengi yanatendeka yanapelekwa police na police utasikia imerudisha kwa chief. Chief amemaliziwa madaraka, hana jukumu la kutekeleza wajibu wake. Sasa unaona kwamba police haelewi yule mtu amekuja ku-report, lakini tukipitia kwa mzee wa mtaa ambaye anajua yule alikosa, tunapitia kwa chief. Chief anachukua jukumu la kuangalia matatizo, kwani pia tukiachilia police mambo mengi yameharibika. Kwa sababu utaenda kushtaki mambo yametendeka kwenye kijiji, bibi amepigwa na Bwana, ukienda police anasema ni family affair. Sasa unaona akina mama wanaendelea kupigwa. Lakini kwa chief mambo

yatachunguzwa, mzee wa mtaa ataitwa, itaonekana kama Bwana ni mkorofi. Atapigwa fine. Kwa hivyo hiyo Chief's Act ningependa irudishwe.

Halafu, haki za akina mama pamoja na raping. Raping imekuwa juu zaidi, tunaona hii hukumu inatolewa kotini haifai. Wasichana wengi wana-rapiwa sana (mtanisamehe wazee mlioko hapa) unakuta hata mzee hata ana-rape mtoto wake hata wa miezi miwili, ni uongo akina mama? (Ni kweli). Kwa hivyo hii raping tunataka tafadhali ipitizwe isiwe ni kifungo kabisa, iwe ni mwanaume akikutwa ame-rape mtoto wake apelekwe police. Ikiwezekana mambo yote yaharibikiwe asifanye kazi tena, kwa sababu ya kufanya hayo mambo.

Pesa za umma, – Hizi pesa za umma, unakuta pesa za umma zinatumiwa. Nikirudi kwa raping nitaguzia kwanza niko na uchungu sana kuna minister ali-rape msichana, sitaki kumtaja jina, tunaelewa tulisoma kwenye magazeti, ali-rape msichana na case yake ilimalizika hivyo hivyo. Ni uongo ama ni ukweli akina mama? (Ni kweli) Kwa hivyo hii raping sisi akina mama tuna uchungu sana sana. Mtoto ana-rapewa wakati huu ni mbaya, kuna ugonjwa wa ukimwi mtoto ame-rapiwa, hatujui kama sasa yule mtu ana ukimwi ama ni vipi. Kwa hivyo tunataka tafadhali rapist wapelekwe hospitali kila kitu kiahidiwe.

Pesa za umma – Golden bag, munajua Golden Bag scandle. Sisi tumekuwa maskini na hizi pesa zilikuwa za wananchi. Utakuta ni minister wetu wamefanya maneno wameachiliwa. Wengine wako ngazi ya juu. Mmesema tusiwataje tunawajua. Kwa hivyo Golden Scandle hii kama ni minister amekutwa amechukua pesa za mwananchi amekula, mali yake ichukuliwe, kama ni mashamba yachukuliwe yauzwe, manyumba, magari yauzwe. Kwa sababu nchi tunaona sasa inazidi kuwa maskini, Golden Bag scandle karibu 68 billion za mwananchi, tunajua, za bank zilichukuliwa na minister mkubwa kiongozi mkubwa, saa hii. Lakini kwa sababu sheria haiko kikamilifu, unaona hizi pesa zimekwenda tunazidi kuwa maskini.

Tunakwenda kwenye education – Sisi kama mama tuliona hii case ilikuwa wakati ule watoto walikuwa raped. Ingewezekana katika education wafanye schools for girls and schools for boys. Tuepuke hii mambo ya girlfriend na boyfriend. Tukienda kwenye mikutano mingi utakuta walimu wanatueleza matatizo yaliyo kwenye shule. Utakuta wana taabu. Hapo hapo shuleni utakuta boyfriend and girlfriend. Ni kwa sababu gani wanasoma pamoja, mixed schools. Tafadhali kama sinaweza zitenganizwe ziwe schools for girls and schools for boys. Sasa hivyo tutaepuka wasichana wetu kupata mimba wanatoka shule wakiwa form two form one utakuta ametiwa mimba na student pale pale shuleni. Asanteni sana.

**Com. Kabira:** Asante sana Martha. Mwingine ni Dick K. Kizaro, councillor. Councillor Dick Kizaru.

**Dick K. Kizaro:** Commissioners na wananchi, natoa shukrani kwa kuwa hapa. Kati ya yale nitakayotoa kwa sasa mengi yameshaguziwa, lakini nitasema machache. Kwanza kama vile mnavioelewa katika Taita Taveta district 62% ya nchi hii ya Taita iko kwa KWS. Na hii, mimi nikiwa ni mmoja ya macouncillors najua huko juu, kuna watu wengi sana ambao hawana mahali pa kulima, yaani wako landless.

Pili tukiingia katika natural resources Taita Taveta district ndio inaongoza kwa Kenya nzima, yaani kwa Kenya nzima Taita Taveta district ina 70% ambayo kwa Taita peke yake inaweza kulisha Kenya government for over 50 years. Sasa swali ni hili, kama sisi Wataita ni matajiri kwa nchi (maana ikiwa 62% tuko na wanyama) na madini ndio hayo, ukiangalia utaona Mtaita anaogelea katika bahari ya ummaskini. We are wallowing in poverty. Naanza kujiuliza mimi mwenyewe kama ni hivyo maana tunafahamu kila watu walipatiwa utajiri wao tuseme maanake ukweli uzima usemwe. Sisi tunafahamu kama ukisoma bible, wakati Musa alikuwa anakwenda Canani kuonyesha wana Israeli ilikuwa anafika mahali anaabiwa na Mungu, "Hapa uziguze ni kwa kizazi cha Lot." Wanaendelea anaabiwa "Hapa uziguze ni kwa kizazi cha Esau." Sasa ukweli ni huu ambao tunakubali, sisi zote kweli ni wa Kenya sawa lakini tunasema ni Wakenya lakini kuna makabira, Taita, kwingine kote, sawa sawa. Katika kuishi sasa, kuishi pamoja ni sawa sawa. Ajabu ni kwamba, huko ninakotoka kama kuna sehemu ingine ambayo pengine kesho na kesho kutwa inaweza kuwa pengine utajiri huo ni ya wageni watupu, yaani ndugu zetu ambao walitoka nje, labda ni madharau. Kwa hivyo, ombi ni hili nauliza hivi kwa sababu National Park ya Taita tangu imeaziza sisi zote hakuna Mtaita yeyote anafaidi hata nusu moja. Kwa hivyo tunaomba ya kwamba katika Tsavo East maana hapa ziko Tsavo mbili, kuna Tsavo West na Tsavo East. Tunaomba Tsavo East ipewe county council ya Taita Taveta ifanywe trust land halafu ifanywe game reserve. Ili kwamba iwe ikitufaidi kama Masai Mara na sehemu nyingine zote. Kwa sababu ni ajabu hata wakati mwingine wakijua yale tunapitia. Na mimi hata kama councillor utakuta nakwenda katika county council nafuata allowance yangu naikosa na utajiri wote uko huko. Hilo naomba Macommissioners huyu ni ukweli ulioko kwa sababu kila watu walipewa utajiri wao. Ukienda huko juu kuna utajiri wa kahawa, kuna utajiri wa majani, kuna utajiri wa pyrethrum. Ukienda Kasarau utakuta nchi kavu sana lakini ikapewa utajiri kwa sababu hata ukienda hapo panapoitwa Mangare ijapokuwa uone ni mahali pamoja tu, utajiri ulioko pale umejulikana karibu dunia nzima. Hata dunia nzima inajua Mangare ni mahali gani.

Ajabu ni kwamba mimi nina experience, maana pia nina prospecting right. Kuna wakati ambapo mimi nilikwenda kuregister mahali. Nilipopeleka Nairobi, ajabu ni kwamba nilirudishiwa majibu nikaambia ati your claim is overlapping na mtu mwingine, na hapo hakukua kuna mtu mwingine. Sasa jambo lingine ambalo lina a lot of sijui kama mtakuwa na forum maalum ya kupendekeza mambo kama haya kwa sababu nilipoambiwa ya kwamba hapo kume-over-lap, mwisho nikeja nikajua kulikuwa na game warden mmoja ambaye ni warden of mines and geology ambaye alikuja ku-resign. Siku moja aliniambia councillor sisi tunajua ni mambo gani yanaendelea huko. Kwa sababu sheria Mining Act cap 306 inapa prospectus nafasi ya kufanya claim gapi, location ngapi? Nane? Ikawa serikali ilikuwa inafanya afadhali kufanya mpango tuzikumbuzwe nane ziwe sita, kwa sababu wewe mtu mmoja ukienda ku-beg achukue sehemu nane unazuia watu wengine wasipate nafasi.

Kwa hivyo Commissioners tunawaomba na nina shukrani kwa sababu hivi sasa tumeletewa geologist katika Taita Taveta district. Na tunataka tukae naye tujue ya kwamba ni kitu gani kitasaidia Wataita kwa sababu ukiangalia section 6 ya Mining Act, cap 306 inaumiza wananchi. Wale wanaochunga kule, ukienda hata kuokota kajiwe kadogo ukija kushikwa nako, unatoshwa faini shilingi Ksh. 2,000 au kifungo cha mieze 6. Kisha katika ile Mining Act inasema hivi, mtu yeyote akipata PR (Prospective Right) unaweza ku-prospect katika Kenya nzima. Hivyo ndivyo ilivyo. Kwa hivyo kitu kilichoko ni kwamba

utahitajika amendment ya Mining Act, kutahitajika amendment hata ya Local Government Act ambayo ni cap 265.

Nikitoka hapo, kwa haraka haraka kwa sababu ninajua saa zimekwisha, katika upande wa settlement scheme tunataka 75% iwe ni ya wananchi. Halafu, kama nitakwenda bio bio, sasa hapo hapo, katika Local Government ningeuliza hivi: county councils all over the republic of Kenya zipewe uwezo zaidi, devolution of power, wawe na uwezo. Pia sisi tunaweza kusimamia kama ni Malindi, na katika Trust Land, mali yeyote ambayo iko trust land iwe ni ya county council kwa sababu ukosoma bure section No. 10 ya mining inasema ya kwamba kitu chochote kilochoko chini ni mali ya serikali. Kwa hivyo ningeomba ya kwamba katika county council ambayo iko katika county council ambayo iko katika public land na hiyo ndiyo ikawa chini ya county council, hiyo iwe ni mali ya wananchi, yaani ya county council.
Halafu nyingine

**Com. Kabira:** Hiyo ingine ndio la mwisho? Uko karibu?

**Kizaro:** La mwisho ni hili na ukweli lazima usemwe. Tulifukuza Waingereza ili kwamba tupate kujitawala sisi wenyewe, na hakuna watu wengine ambao wanadefine rights from God, from heaven. Kwamba wanawacha Trust Land zao kule wanakuja hapa kama wamekaribishwa. Sasa ukifika wakati wa kuchaguliwa wanataka kusimamia mpaka viti vya county council. Nataka kusema hivi, huu ndio ukweli ulioko kwa sababu hata unaposema culture and what not, inatokana maana county, district, viti vyote. Mimi nasema apart from urban areas that all county councils in the whole republic of Kenya viwe vikipiganiwa ni kabila ya pale kamili. Kwa sababu nasema hivi, mimi nina experience. Labda mimi nimefuka mara tatu nikipingwa ni watu wametoka nje. Tena hao ni kwa sababu wako hapa katika settlement scheme ya Kuguta wala hawana property yote katika land ya Kasilau. Kwa hivyo tunaomba tafadhali kwa Kenya yote, nzima iwe viti vya county council mtu yeyote hata kama imekuja umekaa miaka mingapi hapo viwachiwe wananchi wenyewe. Otherwise this will bring problems. Kwa hayo machache kama iko ambaye nimemuudhi aniwie rathi.

**Com. Kabira:** Asante sana Mr. Kizaro. Thank you very much councillor. Now A.G. Mwaloma. Mwaloma hayuko. Akiwa hayuko tutamuuliza Amina.

**Amina:** Nashukuru kwa wakati huu. Mimi majina ni kama vile mliambiwa. Naitwa amina. Mimi kitu nilikuwa nataka kuguzia sana ni kuajilriwa kazi hapa Taita kwetu. Kama Wizara ya Afya, mambo ya health yaani, hapa kwetu Taita Taveta tuko na watoto waliosoma sana. Kama ni wasichana washaasoma wanaweza kuajiriwa kazi ya nursing, ama vijana wanaweza kuajiriwa kazi ya udaktari pia mwanamke anaweza kuajiriwa hata kama ni daktari. Lakini nasikitika sana hapa kwetu Taita hata nyinyi mnaweza kuangalia hapa Moi Hospital, tuko na Wataita wangapi ambao ni nurses? Tuna na wanawake wangapi ambao ni nurses? Wachache sana. Na pia upande wa KWS nikiangalia hivi naona wardens wengi, wengi ni hao tunaita Walia, ama ni ulongo? Sasa nilikuwa nauliza ule ujuzi wao wako nao kwa nini sisi Wataita hapa tusiajiriwe vijana wetu katika hio kazi? Kwa nini watu watolewe nje waje waajiriwe hio kazi na sisi ndio wenyeji katika Taita Taveta district. Sasa itakuwaje watu wa

kado waje wafanye kazi hapa kwetu ambako vijana wetu wako wengi ambao wanakosa kazi. Hata nilikuwa nahimiza Katiba yetu ile mtakaoandika mrekembize at least wakati ule watu wanaajiriwa kazi, sema kwa mfano wizara hii ya afya wakati watu wanaajiriwa kazi, kama mtu anataka nursing, sisi wengi tumefanya application ndio tunataka nursing, lakini tukiangalia hio nafasi hatupewi kwenda kusomea hio kazi ya nursing ili tuje tuajiriwe. Kila mahali lazima kuwe na hospitali. Lakini sasa ingekuwa vizuri at least population kubwa ipatie wanaoajiriwa wawe wanatoka within that area. Lakini sasa nasikitika sana. Sasa ndio nilikukwa naona, maoni yangu ni hilo moja yaani mambo ya kuajiriwa kazi.

Pili wakati watu wanaoajiriwa kazi haswa sisi vijana tuwe tunaajiriwa kazi, at least in that area itoke at least 60% from that area. Halafu hawa wengine pia wakiingia ni sawa. Maanake hivi navyosema kama kwa mfano sisemi kikabila lakini sasa ule ukweli ulioko. Hivi hapa kwetu Moi hospital najua kuna kabila nyingi sana idadi yao ni kama either 80% hivi ndio kabila nyingine na 20 ndio sisi Wataita. Kwani sisi hatuwezi kusoma jamani ama hatujahitimu? Tumehitimu lakini sasa ile nafasi ya kwenda course ndio hatupewi. Saa ile watu wamefanya kama ni recruitment kule district level watu wakishaa ngojea report kwamba watu waende college, haupati. Unangojea haupati. Sasa wale waliopata ni watu kutoka outside our district ambao ndio wanakuja kufanya kazi hapa kwetu. Ni hayo tu.

**Com. Kabira:** Asante sana Amina. Mr. Gabriel Nyambu nafikiri ulikuwa nje lakini unaweza kutupatia maoni. Kwa jina mimi naitwa Gabriel Nyambu. Mimi ni mmoja wa watu waliokuja kutoa maoni yao. Mimi ni mzee, nina miaka 70 na nilikuwa hapa wakati wa Muingereza, kwa hivyo nitaweza kuwapa historia ambayo inaweza kwenda nyumma. Matatizo yetu yote ya Wataita haitokani na serikali ya leo, haitokani na Wakikuyu ama na kabila zingine, matatizo yetu yanatokana na Muingereza. Muingereza alikuja hapa kwetu akachukua nchi yetu akaanza kututawala bila ruhusa yetu, bila ruhusa akatutawala sisi. Tulikuwa na serikali yetu mbeleni. Serikali ilikuwa yaani serikali ilikuwa ni dora sisi yaani ni taifa, yaani tulikuwa na lugha yetu na tunaye lugha yetu mpaka sasa. Tulikuwa na dini zetu, tulikuwa na culture yetu, tulikuwa na kila kitu chetu. Kwa hivyo sisi ni nation. We are not a tribe even we are nation na nation ni dora kama Mwingereza mwenyewe aliitwa.

Kwa hivyo Mwingereza akaja akatufanya sisi ni makabila, akaanza kututawala. Akavuja utaifa wetu, na akavuja na raslimali zetu, akazifanya ziwe za umma akasichukua akasifanya tuungane na mataifa mengine 41 tuwe 42. Na sisi si makabila sisi mataifa. Kama tungaliwachwa uhuru leo tungalikuwa tuko katika United Nation. Tunatabuliwa kama Muingereza kama vile wahindi kabila zingine. Lakini huyu Mwingereza akaja akatuvuja vuja na akachukua kila kitu chetu. Akatufanya tuingie pamoja na makabila mengine 41. Utaifa wetu ukavujwa. Katika kuvuja utaifa wetu akachukua tena nchi yetu hapa Wataita sisi. 62% ambaye ilikuwa inaelezwa hapa ya nchi yetu, tukabaki na 38% ambayo tena imechukuliwa ikapewa sisal estate. Kuna wazungu walipewa hizi mashamba ati ni zawadi Mzungu yule Mwingereza anampa maskari wa kiingereza waliopigana na Mnjeremani 1914 wakapewa zawadi ya mashamba yetu, Taveta, Mwatate, Sisal estate na Kidali.

Tatu, juu ya hio tena wamechukuwa National Park 62%. Uhuru ulipokuja wakai-hand over tena kwa serikali ya mwananchi Muafrika na sisi tumekuwa utawala hatutapata huu utawala mpaka wa leo. Leo twatawaliwa na kabila, na watu ambao ni

mataifa mengine wameungana pamoja makabila makubwa wakaanza kututawala. Mpaka leo sisi Wataita hatujatawala bado. Mpaka sasa tunatawaliwa. Twatawaliwa na nani? Tunatawaliwa na makabila makubwa, yaani majority tribes. The minority have no powers. Niwambieni siri kama hamjui, hata kama tunayo government ya sasa ambayo inatawaliwa na Mkikalejin.

**Com. Abubakar:** Mzee Nyambu, sorry sitaki kukukatizia lakini umeongea dakika tano hivi na hujasema kuhusu recommendation hata moja. Historia ni sawa lakini hatutandika hio katika Katiba mpya. Utueleze

**Nyambu:** Lakini mtaelewa namna gani Katiba yetu kama hamjui nyumma tumetoka wapi?

**Com. Abubakar:** Sawa sawa, lakini utueleze sasa Katiba itusaidie namna gani.

**Nyambu:** Okey, sawa. Number one nataka Mwingereza maanake serikali yetu haina pesa za kuturudishia ridhaa ya National Park, imechukua 62%, nataka Commission hii irecommend kwa Mwingereza ambaye alitutawala hapa miaka sijui mingapi, akachukua nchi yetu akaipa Wakenya 41 tutawale pamoja, ndio wanakura mapato ya National Park. Twataka Commission hii irecommend kwa Mwingereza aturudishie ridhaa ya 62% ya nchi yetu aliyochukua, halafu tena tuataka kama tutaendelea na Kenya KWS, tupewe 62% katika ile National Park. National Park imbaki na 38%. Tutataka tena watoto wetu wandikwe kazi hapo majority. Twataka tena tukubaliwe sisi tunachunga mifugo yetu dani. Hili ni shamba letu halafu tunakatazwa tena kwenda kupeleka mifugo yetu, na sisi Wataita hatuumizi wanayama tunaishi nao toka utotoni, toka zamani za kale. Leo tunaambiwa ya kwamba watu wengine wanaharibu wanyama.

No. 2 Mwingereza huyo huyo, alipochukuwa nchi yetu 62% akachukua na maji Mzima Springs, akapeleka Mombasa. Yakapita hapa kwetu hata hatuna tone la maji hapa. Akapeleka Mombasa. Anaauza maji yetu 35 cubic meter inaenda Mombasa kila siku. 35 thousand cubic meters zauzwa Mombasa. Sasa utachukua kitu cha mtu hapa unaenda uza sisi hatukupata hata nusu cent waenda uziwa watu wengine upate pesa za unaziita revenue ya economy ya nchi nzima. Wanaokunywa maji ni makabila hayo 41 nilikuwa nasema. Na pamoja na sisi wachache. Kwa hivyo maji yetu twataka Commission hii iandike kwa Mwingereza aliyechukua nchi yetu ya maji bila kutuuliza turudishiwe mali tupewe percentage ya maji kutoka 1948. Hio ni National Park, ile ingine ni maji. Hatuwezi kupeana maji yetu hivi kila kitu free na ni nchi yetu. Tena msisahau nyinyi sisi tumepeana maji na National Park for the benefit of the whole nation. Now wale nation zingine 41 wametupa sisi nini? Central Province kuna coffee, kuna pyrethrum, kuna chai, hii chai wao wako na title deed wanauza nje wanapata faida hawa wajamaa inaingia kwao binafsi wana title deed, sisi maji yetu na National Park wanaitumiwa wao ni ya umma yao wana-bank. Ni haki gani hio? Bwana Commissioner uangalie hio. Na sisi hapa na tunauambia huu mkutano nataka Commission ya Constitution hio inaendelea particularly kama vile ya Electoral Commission, tukiwa na matatizo kama haya tunayapeleka. Kama hukufanya hii marekebisho tunayosema ya kupeleka kwa Mwingereza tutachanga pesa sisi tushtaki wewe. Tushtaki Constitution.

Mwingeza hakusimama hapo, akachukua tena barabara yetu hapa akachukua nchi kutoka Mtito wa Ndei huko Ndarajani mpaka Talu. Ati anatengeneza barabara, atengeneza railway line, hii railway line yapita magari ambayo sisi hatuyatumii. Yafanya uchumi wa Uganda na Sudan, yafanya uchumi na Zaire, yafanya uchumi na Central Province sisi hatupati chochote hapa na barabara yetu imetumiwa ikakatwa kilimeter kutoka 155 mpaka Mtito. We have not been compensated for that. It has gone. Mtu ameiba huyu na tena akaenda bila kutuaga, anatoka kisiri siri anaenda zake. Halafu twataka maana sisi hatuna magari yakupita hizo barabara hizi, magari yana wenyewe huko mwajua. Sasa basi na magari yanaenda Sudan, yapitia kwetu hapa. Bwana Commissioner tunataka a percentage of this road kutoka shinyanga mpaka Tasa irudishwe kwa county council yetu wapate kitu katika hio. Yaani unaweza kuchukua nchi ya mtu namna gani utumie kwa manufaa yako ya manuvaa ya umma watu arabaine na moja, hawa 41 tribes, watumie wao wenyewe wao ndio wenye magari, sisi hatuna. Make hivyo hivyo. Now Bwana Commissioner, where is this justice? Yaani what is it? The Taitas have contributed so much to become Kenya citizens. Yaani tulipwe National Park, halafu hatukulipwa, maji hatukulipwa yameenda Mombasa inanywewa, barabara zetu, railway line hapa yapita magari hatujui, barabara zetu zile za ndani na Mbogoi tumelima sisi, hatuna matatu sisi, matatu inayopita ni ya wageni. Watu wachache. Hii ni serikali gani ambaye takes somebody's property for the benefit of many.

Kwa hivyo twataka before we join forces na the rest of the 41 tribes we want to be compensated. Yaani tujue tunaingia namna gani katika hii umoja unaitwa Kenya. Na huu Kenya tunaingia pamoja halafu tena wanatunyanyasa. So we cannot just go to join 42 tribes. What is our contribution, what is their contribution. Now to give an example mzee chairman I have spoken about tea and coffee. Hatupati hio coffee. It goes to individuals. Something came the other day called loan. Hiyo, vijana na akina mama, ni pesa zimekuja special kwa watu wa Central Province, watu walio na kahawa. Nyinyi hamna maskini. Mna maji mmepeleka na nini lakini hawa wamepelekewa pesa na standard kutoka ulaya ikaletwa ili zipewe hawa atiriri ambao kwa sababu wanapendwa. Now the Constitution actually favours the Kikuyus, why? Let me tell you why it favours the Kikuyu because a) they are the majority in the country, they are about 10 million people you are 250. Sasa basi hawa wakabila wanapewa pesa wanakuja kugawana. Sasa tumeona katika benki hazitolewi lakini ni zao. Sisi hatuletewi chochote. Hatuna coffee, lakini tuna barabara na tuna maji yanaenda haturudishiwi. Sasa basi, Kisumu, Bwana Commissioner, Kisumu have got their lake. Wana samaki pale. Hawa Mwingereza na Kenya na Moi wamemkubalia Mjaluo ama mtu mweusi na manyanga kuvua samaki Kisumu binafsi ingalikuwa ni ya umma hio. Lakini wanavua samaki wanatuuzia sisi Wataita na kabila zingine. Wanapata pesa kutoka uchumi wao. We don't get anything from our uchumi. Now what type of partnership do you want to join with you people when we are not benefiting anything from your samaki we buy it? We are not benefiting from Western Province ambao wana mahindi unaabiwa kwamba Western Province is the cradle ya maize, kunatoka mahindi kule. Tumeyanunua haya mahindi. Everything we buy from Kikuyus, from Western, from Nyanza. Sisi tunapeana yetu free Bwana. Suluhisho ni turudishiwe pesa kiasi ambacho ilichukuliwa sisi wataita tupewe sehemu yetu, na mtu wa kupata hii pesa ni Mwingereza. Mwingereza yuko tayari kupeana hizo pesa na halafu tupewe from siku ile tulichukua. Because they robbed us. They grabbed our land and forfree I am giving to you and who is benefiting? The Kikuyus because they are majority. Siwatukani Wakikuyu lakini kweli majority. Now let me tell you why the Kikuyus are benefiting in this country.

(Inaudible comment from Com. Abubakar)

Mimi nina dakika kumi mheshimiwa. (Interjection)

Commsioners I have one announcement to make.

**Com. Kabira:** Asante sana Bwana Nyambu. Okey. Thank you very much utaandika jina lako kwa hio kitabu yetu.

**Com. Abubakar:** Nataka kufanya matangazo fulani kabla hatujaendelea. Ningeliomba tafadhali tutii ile sheria ambaye imewekwa. Dakika tano ni yako wewe ambao ulio na memorandum yako uileze kwa kifupi, lakini naona tukifuata huo mwongozo wengine hawatapata hio nafasi kwa sababu mwisho ni saa 12. Kwa hivyo ningeliomba kwamba wale ambao wako na memorandum zao, wa present memorandum zao. Halafu wale ambao wako na oral, yaani wanatoa maoni yao kwa mdomo, ya kwamba watoe maoni yao kwa mdomo. Lakini kuna pendekezo fulani ambalo nimepata kutoka kwa wananchi ambao wanatoka mbali. Kuna watu wanatoka Sagala na magari yako na shida sana. Kuna watu wametoka Kasigalau na iko shida. Ningeliomba ya kwamba mnielewe kama wananchi. Sisi ambao tunatoka karibu tuwapatie wale ambao wanatoka mbali nafasi ya kwanza. Lakini before we do that, ninataka ku-identify, niwangapi ambao ni wa Sagala hapa? Ni wawili, na Bololo, not Bololo. Bololo wako na nafasi kesho. Kasgau, Kasgau ni wangapi? Kwa hivyo watu wale wametoka Sagala ni watatu. Madam Commissioner ni watatu wale wametoka Sagala ndio watapewa privilege kwanza halafu ndio sisi wengine wa Kasgau ni wangapi? Kwa hivyo ni watatu. Halafu mmoja ambaye anataka kuondoka Mombasa kwa hivyo watakuwa ni watu wanne. Kwa hivyo Wasagala mnaombwa mmoja mmoja watu watatu ambao wame-raise mkono yao.

**Com. Abubakar:** Halafu ndugu yangu pia namna hii, tafadhalini sana tujaribu kufupisha. Ukiona jambo lishaatajwa na mwingine usiendelee tena na kurudia rudia. Pitia pitia juu ndio tummalize. Tuko na watu 209, na hatuwezi kummaliza tutakaa mpaka asubuhi.

**Churchill:** Macommisioner, wananchi wenzangu, hamjambo? Mimi yale ambayo nilikuja nayo hapa yamezungumzwa yote na wenzangu lakini mawili nataka kuzungumza. Jina langu ni Churchill Ngati kutoka Kagau.

Macommissioners katika Katiba hii ambayo tumekuja kuipendekeza leo, nina na mambo mawili, matatu hivi. Jambo la kwanza nilikuwa nasema hivi. Kiwe kipengere hapo katika hio Katiba cha kuwezeza wananchi, sisi wenyewe wananchi, wapiga kura ambao tumepewa kura kuchagua mbunge na kuchagua diwani, tupatiwe uwezo kamili wa kupigia mbunge huo kura na kumfuta. Yale ambayo anatuahidi hatekelezi tupatiwe fursa hio miaka mitano asimalize. Tumuondoe aende viake. Tuchague mwingine. Diwani pia hivyo hivyo. Manake hawa tunawachagua wakaenda Nairobi wanalala huko. Ukimfuata hapa anakwambia labda umeshindwa kidogo na fee ya mtoto akwambia hatuzaa pamoja. Mwingine anakwambia hio pesa niliokupa iliisha. Sasa ni kama wananunua watu. Tupatiwe nafasi hio nzuri kabisa hio.

Jambo la pili.  Kupitia Katiba hii ambayo tunapendekeza, ninaona kuna wafanyi kazi wengine wa serikali ambao wanapata taabu sana, hasa viwango vya chini.  Mtu anastaafu, kama mwalimu, madreva wa serikali wa maDO, wa maDC basi atandai pesa miaka mitano kama mtu alikuwa hafanyi kazi.  Mpaka watoto wabiwe waache shule ukienda Nairobi kuuliza pesa unaabiwa file ilipotea.  Number yako ya kazi haiko huku, ilikuwa anapata mshahara vipi?  Iwekwe kipengere hapo, hii Katiba mtumizi wote akiwacha kazi baada ya miezi mitatu awe amepewa mali yake yote.

Nitazungumza habari za dini – Dini tungetaka serikali ichunguze haya mashrika yamekuwa mengi sana.  Kila kukicha twasikia dini mpya, kanisa mpya.  Mengi yamekuwa ni ya biashara haya makanisa.  Tena wamekuwa ndio wanyakuzi wa ardhi.  Haya makanisa yachunguzwe, yale ambayo hayafai yafutiliwe mbali.  Bona Waislamu wana dini moja tu peke yake?  Sitaki dini, mimi ni Mkiristo, lakini yamekuwa mengi.

Jambo la mwisho ni hili, Katiba hii ambayo tunataka kwenda kuitengeneza, tungetaka ihesimu utamaduni au mila za Muafrika. Naona bado kuna chembechembe za ukoloni.  Kwa nini pombe iitwe haramu?  Kama pombe ni haramu, hata bear ni haramu pia, hata whisky ni haramu sababu ukienda unakunyua unalewa.  Kama ni kuvuja zivujwe zote.  Pendekezo yangu ni kwamba sisi Wafrika kila kabila lina pombe yake, ihararishwe.  Tuwachiwe pombe yetu tunywe.  Hii pombe ya kuimba imba hii ndio inaua watu, nifanyie haraka haraka kumbe unapewa sumu.  Unasikia mama ongeza ingine kube unapewa sumu.  Hii pombe tupewe tunywe.  Asante sana.

Mashamba – Lease zote za mashamba zifutiliwe mbali za ukoloni.  Mwananchi wa kawaida kama mimi nipewe ika 20 za shamba.  Kama ni kampuni ikali 100 iwekwe sheria.  Tangu uhuru watu wamezaliwa wengi sana na nchi hii haifanuki, watu ndio wanakuwa wengi.  Hizi buga za wanyama nilikuwa na pendekezo moja – Wajiriwa kazi katika hizi Tsavo 75% iwe Wataita. Na mapato pia 75% ipatiwe hapo hapo ndio huyu malikia mmpelekee hio 25.  Asanteni.

**Mwangeni:**  Macommissioner pamoja na wananchi hamjambo?  Kwa jina ni Biljai Mwangeni.  Mengi yameshazungumzwa sasa nimeshayapunguza sasa mtayasikisha yale ambaye haijaguzwa.  Yale haya nimesikia kwamba hayajagusia ni hivi.  Mme ana uwezo wa kuridhi mke katika mambo hao akiwa aliwachwa na mkewe iwe kwa ajali au ugonjwa bada ya kuhararishwa kwa kituo cha afya.  (noise from public)  Hebu tulieni wananchi, kama hamjanielewa, hebu tulieni nimeona matatizo mengi sana. Hii ni kusema ya kwamba mwanamke chini ya miaka 60 anaweza kuridhiwa na mme katika mlango wa kwao.   Baada ya wote wawili kuhararishwa katika kituo cha afya.  (Interjection)  Nafikiri bila shaka tushaaelewana  haya sawa maanake hapa mimi nimeona machanga mingi sana ambao huwa yanatokea mwanamke anaenda kuridhiwa kiharari kwa sababu ya uzima ule tuliopewa na Mungu.  Sasa unasubua mpaka mwanamke anaenda, anaruka anachukua ukimwi huko analeta katika boma na hali huko nyumbani katika boma yake kwenyewe kulikuwa kuna mme aliye salama anaweza kuchunga kiafya.

Ingine la pili, mtu ana uwezo wa kupata sehemu kwao iwapo aliolewa kisha akaachana na mme kwa kutoelewana na hayo

makosa kudhibitizwa na wazazi wawili wa mke na wa mme mara tatu.

Lingine mtu akitunga msichana mimba na kumkataa atalipa mahali ya kumuoa na ile mahali itamsaidia wakati atakapokosa wa kumuoa au akiolewa mtoto akikataliwa na mme yule aliyemuoa ile mahali itamsaidia au mwenye mimba amgharamikie mtoto wake atakuwa ni wake ila mama atabaki. Msichana na awe akiolewa na mtoto ile mahali watatumia watu wake. Bila shaka tushaelewana hapo.

Nina pendekezo la dini – Katika upande wa dini hii ni mambo yalio magumu kwa sababu haya ni mambo ya rohoni mtu wa mwili ni kuyatabua ni vingumu. Dini zisiwe na ushuru wa kulipa kwa kuwa haziendezi biashara. Viongozi wa kidini wana uhuru wa kuhubiri dini popote bila kukosolewa au kupigwa na kupingwa pia. Bora wawe wanahubiri kweli ilioandikwa.

Lingine ni kwamba ni hatia mtu yeyote kupokea rushwa au kumshtaki mwenzake kwa uongo na kila neno lidhibitishwe na mashahidi watatu kama ni mshtaki na mshtakiwa iwe kuna sababu maalum ya kuonyesha kwa nini wanasimama wao wenyewe wawili kwa mambo hayo. Mara nyingi kumekuwa na shida katika shehemu za hudumma za utawala. Report za utawala, pendekezo langu ni kwamba wabakie vile vile, lakini isipokuwa tu hudumma zao ni sawa isipokuwa mara nyingi hujihuzisha na ujambazi kwa ajiri ya jaa kusimamisha watu ovyo ovyo na kuomba rushwa, ilhali mishahara wanalipwa. Kwa hivyo hudumma zao watekeleze sawa sawa na ipasavyo kulingana na vile iko na ni hayo tu niliuoandaa. Asanteni.

Macommissioners na wananchi ambao wako hapa, hamjambo. Mimi ningelipenda kutoa

**Com. Abubakar:** Sema jina lako.

**Mwakina:** Julius Mwakina. Ingawaje nimeandika mengine, mengine ningetaka kuzungumza, la kwanza nataka kuzungumza juu ya aina ya Katiba ninayoitaka iwe katika nchi yetu ya Kenya. Natoa maoni kwamba Katiba ya Kenya iwe ya majimbo. Majimbo yawe nane. Nairobi ikiwa kama special jimbo kwa sababu Rais ataketi hapo. Kila jimbo liwe na Bunge lake na governor wake. Governor awe in-charge wa police na GSU na jela katika jimbo lake. Governor a-control ama asimamie uchumi wa jimbo hilo. Hii ni kusema kwamba kila jimbo litumie mali yake kama ilivyoamlishwa na Mwenyezi Mungu maana kila kabila la kila jimbo lilipewa mali yake. Central Province ina mali yake, Eastern ina mali yake ya asili lakini hapa Pwani, mali ya Pwani ndio mali ya national, ya umma. Kwa mfano, Bwana Commissioner na mama Commissioner, Kenya port iko Mombasa na ni katika Pwani, lakini uchumi wa Kenya Port wote unakwenda kuliwa Nairobi na Central Province. Hio si halali. Samaki zilizo Mombasa ni katika mkoa wa Pwani lakini hatuzipati faida zinakwenda kufaidi watu wa juu. Ni makosa. Madini yalio Taita Taveta yanatumiwa na watu wa Central Province. Sisi hatupokei hata kitu, ni makosa. Wanyama ambao wako hapa wanatuua sisi wanakanyanga sisi wanakura mimea yetu, wanakura wanyama wetu, wanalipiwa pesa hakuna hata senti moja inabaki katika district ama katika province zote sinaenda huko maana ni mali ya umma.

Maji ya mfeleji wa mzima yanatumiwa na umma lakini mali ya watu wa Taita ni mali ya Pwani. Na zinginezo kama misitu hayo naomba commissioners watilie mkazo yaangaliwe.

Ardhi – Ardhi imekuwa ardhi ya Pwani, hata Taita, ndio ya watu wote Kenya. Na inatolewa huku Rais anatangaza amefunga maplot yasiuzwe lakini inatolewa na tunaona. Hii nataka kusema wazi ya kwamba ni maonevu ya ajaabu kwa sababu Mtaita hawezi kupata ardhi, hawezi kupata location ya ardhi rahisi lakini Mkikuyu anakuja na karatasi tayari na hajaishi hapa. Mimi nimenjenga pale nimefanya biashara pale unambia ondoka hapa ni kwangu. Hii italeta shida baadaye. Hio naomba macommissioners tafadhalini mtusaidie hio shida iondoke.

Halafu katika hali ya upokeleshaji ya kubadilishana ardhi kuna kitu kinaitwa squatter. Naomba Tume hii igeuze kabisa ama Katiba ijayo isiwe na jina la squatter. Mimi nasema kwamba ni aibu Wakenya miaka 39 wanakuwa squatter katika nchi ya kuzaliwa. Inakuwaje mtu awe squatter mahali alipozaliwa? Halafu serikali ikatunyanyasa hasa mtu anaitwa Commissioner of lands. Yeye anatoa ardhi kwa watu binafsi kuwatoa watu maelfu au mamia walio pale halafu ardhi hio inatangazwa kwa Kenya gazette, Kenya gazette hio haitangazi open, wananchi hawajui inatangazwa halafu inapitia katika government offices wanaojua ni watu wa ofisi. Je mwananchi huyu anajulishwa kivipi? Kenya gazette iondolewe mbali kama allocation inafanywa basi allocation hio itangazwe kwa magazetti ya kiwasili na radio na watu wakipinga isifanyike.

Halafu kuna mashamba makubwa yaliotolewa mtu mwingine anasema, yaliotolewa na kitu kinaitwa lease, miaka 999. Huu ni wizi wa mchana wananchi wameporwa na Mzungu halafu wakaporwa pia na serikali ya Kenyatta, na wanaendelea kuporwa na serikali hii tuko nayo sasa. Haya mashamba yalegezwe na mambo ya lease ya 999 years, iondolewe kabisa. Mashamba haya yagayaaniwe wananchi wa pale mahali. Na nisisitiza kwamba vile zilizotolewa zawadi kwa wageni wahindi, wahindi hao hawana mpango na Wakenya, wahindi walileta na Wazungu. Kwa hivyo wahindi mali yao iko na Mzungu huko Uingereza. Tulipomaliza na mwingereza tulimaliza na mambo yake yote lakini alimbakisha wahindi hapa ndio wanaendelea sasa kutunyanyasa na kupewa mali katika mambo ya lease. Iangaliwe hayo tunaomba.

Mambo ya wanyama nimesema lakini kuna sehemu nataka kuguzia Bwana na mama Commissioner ya kwamba inapofikia wakati wa kuajiriwa kazi, training ya kufanya kazi ya KWS iko hapa na wanyama wako hapa, na watafanya kazi hapa, na wanaokanyanga wako hapa lakini unapata 90% ama 95% ni watu kutoka huko. Wataita wanaenda tu, wanachezewa chezewa hapo wanaandikwa watatu ama wanne hii naona kwangu ni aibu kubwa. Hio naomba ibadilishwe. Wenyeji wachukuliwe 85%, 25% itoke nje.

Mambo ya madini – Leo hii ni hatia kwa Mtaita ni hatia kuwa na sehemu ya madini pale pale hapa Kaslau, hapa (inaudible) ni hatia. Ukienda kujaribu wewe, utaoneka umetoka mbinguni hujakuwa hapa Kenya. Hio ni kazi imepewa watu kutoka juu hii ni unyanyazaji wazi wazi mimi naomba kwamba Commission Katiba ambaye inaenda kuandikwa iondolewe kabisa jambo hili mali ya madini ni mali ya asili ya watu walipo. Hii ni mali ya Wakenya, ni mali ya Wataita, ni mali ya WaPwani. Ibaki pale na

itumiwe na watu wa pale.

Uajiri wa kazi katika civil service – Wakati walimu wanandikwa inatangazwa kwa magazetti. Kwa mfano, walimu wataandikwa Wudanyi 400 lakini watu wanaokwenda kuandikwa Wundanyi majina yao hutoka Nairobi, wameandikwa kabisa. Watoto wa Kitaita ni waende pale wapigwe na baridi halafu radio itatangaza watu wameandikwa 400 kutoka Wudanyi, lakini hawa huwa ni wa Kikuyu na Wabaluhya na Wajaluo. Watu mlio hapa mnisamehe kama nimewakosea. Halafu ndio unaona skuli za hapa hazina walimu wa Kitaita. Police vile vile inapotangazwa police wanaandikwa police wanambiwa wanandikwa Wundanyi watakwenda wakimbizwe pale Wataita wavule mambavu bure lakini wanaandikwa ni wa kutoka juu ndio unaona kila police station Wataita hakuna. Kijeshi siwezi kusema kwa sababu sijafika katika camp za jeshi sijui vile walivyo lakini nafikiria ni hivyo tu. Na katika other departments, other ministries za serikali, Wataita hawana nafasi ama watu wa Pwani.

**Com. Abubakar:** Pendekezo lako ni gani bwana?

**Mwangeni:** Ni kwamba 85% ya watu wanaoajiriwa katika district watoke pale mahali.

Pombe – Bwana Commissioner na mama Commissioner, hakuna wakati tunaweza kuzuia pombe kunywa, hata tukaombe kichwa chini na miguu juu. Kutaokoka watu na bado kuna watu wa kunyua pombe, lakini kila siku wanahangaishwa na police na kushikwa na kupigwa fine na kulegeswa maskini watoto wakose fee. Pombe ihararishwe. Kama haihararishwi basi hata bear zifungwe ama iwe wakati wa kunyua ni saa kumi na moja mpaka saa mbili. Bar zote zifungwe na vilabu vyote vifungwe. Lakini miti dawa ni sahihi inaendelea pombe ya kienyeji, wenyeji wanashikwa na kuwekwa ndani. Naona kwamba hio si sawa.

La mwisho, dawa za kienyeji – Dawa za kienyeji hizi si za Taita peke yake ni za Kenya nzima. Muafrika inaonekana hawezi tengeneza dawa za kienyeji. Inaonekana wakati ule dawa ilipotoka ya kutibu ukimwi yule Bwana alipigwa vita mpaka nyinyi mnazijua, haina haja kusema. Lakini ile dawa leo ingalikuwa inaokoa watu wengi kufa. Kwa hivyo Katiba itoe ruhusa ya Muafrika kutafuta dawa, maana miti hii ndio inatengeneza dawa na Wazungu. Lakini tunandanganywa dawa ni ya kizungu inaponya na Kiafrika hakuna. Ya Kiafrika inaponya, kwa hivyo dawa mizizi ya Kiafrika ikubaliwe halafu ile mambo ya kuogopa ogopa iondolewe na dhambi haitakuwako. Naomba nifike hapo na asante sana.

**Com. Abubakar:** Tafadhali ningeomba ya kwamba kuna watu wengi wanataka kutoa maoni. Ukija hapa fupisha kabisa ili kila mtu apate nafasi. Tafadhali. Kwa hivyo unapotoka tafadhali njoo. Halafu mwisho ni huyo halafu list inafuatwa sasa maana tulisema watu wainue mkono.

**Ronald Nzai:** Asante Commissioner na wananchi. Mimi kwa jina naitwa Ronald Nzai na niko hapa kwa niamba ya NCK

Taveta DCC. Kwanza katika chini ya makanisa katika Taita Taveta tunayo mapendekesho machache ambayo tumeonelea kueleza kwa Commission leo ili yaweze kuingizwa katika shehemu ile ya Katiba. Ya kwanza ni uhuru wa kuabudu. Uhuru wa kuabudu tumekuwa na religious clashing, religious conflict kwa sababu wale ambao wanakwenda kueneza dini haende kusimama akazungumza mzuri wa dini yake anakwenda kuingilia dini zingine. Kumekuwa na so many religious conflicts na ni kwa sababu ya ku-abuse the freedom of worship. Mfano mzuri utaona Waislam anakwenda kuingilia biblia, badala ya kusimama na kuzungumza uzuri wa kolan anakwenda kuzungumzia juu ya biblia.

**Com. Abubakar:** Kwa hivyo tufanye namna gani?

**Ronald Nzai:** Kwa hivyo uhuru ukuwe na clause act kwamba yeyote atakayeingia imani ya mwingine ni hatia. Hio iwe ni hatia. Ili katika freedom of worhip, kuna Commission ambaye imeundwa kuangalia juu ya uabudu wa mashetani. Na hii haikuweza kutolewa mpaka sasa. Imekuwa imewekwa in a shelf na hii imekuwa ni hatari kwa Wakenya. Tunaona visa vingi vimetokea kama Mbobolulu, kama Kianguli na mambo mengine. Hatujui ni kwa nini. Pendekezo langu ni kwamba kila dini inayokuja kwa njia ya dini iwe ni mungiki, iwe nini ichunguzwe kwa makini na ikionekana sio halali ipigwe marufuku.

Ninarudi pale katika Local Government – Mtu kuwa councillor awe amefikia form 4 level kwa sababu kumekuwa na matatizo katika council zetu na municiple zetu ni kwa sababu tunapata watu ambao sisemi kwamba hata mtu asiye na elimu si kiongozi lakini kiongozi with a limit. Kuna level fulani ya uongozi au form 4. Councillors wachaguliwe direct na wananchi na mayors, na chairmen wa county councils wachaguliwe direct na wananchi. Sio watu wachache kwenda kuchagua mamayor na machairmen. Wakiwa ishirini, mwenye pesa anaweza kuwahonga na wanapatia mtu ambaye hastahili.

Jambo lingine ni powers za President – Katika land unaangalia katika ufuo wa habari anayeruhusiwa kutoa kibali ni President. Pia tunasema kwamba Constitution ingizwe katika syllabus ya education ili elimu ya Katiba ifundishwe katika mashule yetu. Huu ni ujinga ambao tumefanya miaka mingi, Katiba haikuweza kuingizwa katika ile syllabus ya education na ndio unakuta Wakenya wengi hawaelewi maana ya Katiba ni nini. Kwa hivyo ingizwe katika syllabus ya education. Mfumo wa elimu urudishwe. Tunataka mfumo ule wa akina Curry Francis urundishwe, huo urundishwe .

Mwisho katika jumuia ya makanisa Taita Taveta haikubaliani na Commission kuongezwa mda. Jumuiya ya makanisa Taita Taveta inakataa Commissioners kupewa mda zaidi kwa sababu tumechunguza tumeona baadhi ya Commissioners, they have become hyenas. Kwa sababu kuna mlo pale mda uongezwe ili waendelee kura. Hilo hatukubali. Tumeona baadhi ya Commissioners fulani wanatumiwa kuzitisha tiza ile council ya urekebishaji wa Katiba kwa manufaa ya watu binafsi. Hio hatutaki tukiwa jumuia ya makanisa, Taita Taveta hatutaki. Kuna wale ambao nao sasa they have Kenyan blood wanasema lazima tuimalize Katiba kwa wakati ufaao, wananchi waingie kwa uchaguzi kwa Katiba mpya. Kwa hivyo inagawanyika mara tatu. We have hyenas na Commission. Tuna watu ambao wanatumiwa kwa benefit ya mwingine na kuna wale ambao wana Kenyan at heart. Thank you very much.

**Com. Abubakar:** Makofi kidogo kwa yule mzee. Jemimah Mambuliki. Tinah Wambui. Gladys Mwangombe. Jambo Phillip. Stella Wakio. Edwin Mwambiti. Dollah Muinda. Christine Rejai. Eric Mwanzai. Kizingo Vic, Kelly Samuel Pauline Mwanombe, Angela Chao, Peter Nyerere, Charles Goro, David Bombo.

**David Bombo:** Jina langu naitwa David Bombo na nimekuja hapa kutoa maoni kulingana na Katiba ambayo ningetaka. Ukweli ni kwamba ninaomba nitoe wazo kidogo kwa ndugu zangu kulingana na mambo mmeendelea kutatua. Hio nafasi yangu ya mda wangu. Ya pili naona ndugu niwaelimishe kidogo. Mjue kabisa watu karibu millioni 10 Kenya watatoa maoni yao. Na msije mkafikiria kwamba itaandikwa Katiba ambayo ni ya watu millioni 10. Itaandikwa Katiba kulingana na mambo ambayo mmetoa yaende yaangaliwe yametolewa na watu wangapi na ina uzito wa aina gani. Endapo basi wewe utakuja hapa ati unatoa maoni halafu useme mengine nayakata maanake mwenzangu amesema, haya mambo yakitoka pale itakuwa labda wewe peke yako ndio umesema, na kumbe hamjasema watu kumi. Sasa ikiangaliwa yataoneka ni mtu mmoja amesema kumbe hapa tuliingia ndani, zote tunataka kusema jambo halafu unaogopa kulisema. Lakini kama unalo neno unalotaka uliseme na mwingine aje, aseme na mwingine aje aliseme litaonekana limesemwa na wengi ndilo litaingia kwenye Katiba. Lakini usije ukasema I sitasema hivi kwa sababu limesemwa na watu wengine. Ha ha mnapoteza nafasi ndugu wapendwa. Kama ni mtu amesema juu ya majimbo nawe ukija sema juu ya majimbo, inaonekana majimbo, majimbo, na tu wengi ambao tunasema jambo hilo. Tuko pamoja.

Haya naingilia mambo ya Katiba. Katiba kwa mawazo yangu au kwa pendekezo langu iwe ni funzo shuleni tena kitabu kitolewe cha Katiba ambacho kitanunulika na mwananchi wa kawaida.

Mawaziri – Mawaziri kutokana na pendekezo langu ni kwamba wasichaguliwe kutoka kwa kudi la wabunge. Kwa sababu gani? Wambunge tunapowachagua tunawapeleka Bunge ili waende watutetee lakini anapochaguliwa waziri katikati ya wale basi hatatutetea tena bali atakuwa anatetea serikali. Sasa itakuwa kwamba hatuna maana ya kuwa na mbunge pale. Tume zote zinapoundwa si kwamba siundwe na Rais. Kwangu mimi nakataa jambo hilo kwa sababu Rais ameunda Tume nyingi sana na tumeshuhudia na hakuna Tume yoyote ambayo iliotolewa tukaisoma kama imeishia wapi. Kila Tume inapoundwa pesa zinatumika bure halafu mwishowe inatumwa mahali, manake aliyetoa ana uwezo wa kusema isitolewe nje. Kwa mfano ya Devil Worshiping. Kitu ambacho kimeibwa na bado kinaendelea tunazidi kuumia hivyo basi pendekezo langu ni kwangu ni kwamba, Tume isiwe tu ni ya Rais iwe ni ya Bunge la Kenya. Uchaguzi ama appointee kama vile Attorney General ama Chief Justiceuisiwe wa Rais kwa sababu mara nyingi tumeona ya kwamba anachagua marafiki zake ama watu kulingana na wale mawaziri wake walioko kwamba mchague fulani, halafu atakapochaguliwa hatatimiza wajibu wa kazi yake. Inakuwa ni kwamba ana upendeleo fulani. Tukiangalia kama case ambazo zilitolewa moja katika municiple council ya Mandera na nyingine ilikuwa ya Ngeny, halafu zikaisha tu hivyo hivyo kwa sababu kuna upendeleo fulani. Kwa hivyo mimi nasema ya kwamba watu kama Attorney General ama Chief Justice wasichaguliwe na Rais, bali wachaguliwe kwa mudo Fulani kwamba anaweza kufutwa na anaweza akaandikwa.

Majimbo sikutaja, mimi ninaunga mkono majimbo, na naunga mkono kihivi. Uwe wa kiraslimali, yaani sio kwamba ni mambo ya majimbo tufukuze fulani aondoke hapa, huo hafai, aa a. Ni kwamba tuwe na majimbo lakini resources ziwe within that province there. Na hilo jimbo ama majimbo haya yawe vile vile tulivyo na majimbo sawa.

Uhuru wa kuabudu – Uhuru wa kuabudu ufafanuliwe zaidi. Kwa sasa tunaona kama hauna mipaka, ni uhuru wa kuabudu hata ma devil worshipers pia wana uhuru wa kuabudu. Hilo ni jambo tumeona halifai.

Head of parastatals wasiwe wanachaguliwa na President, wachaguliwe na Bunge. Na mawaziri wanapochaguliwa hata ikiwa hawatachaguliwa na President, lakini wachaguliwe watu ambao watu ujuzi kulingana na elimu yao. Sio kwamba mtu mlinga wakati mwingine alikuwa Minister of Health, mtu ambaye alitoka standard six na anajua tu kushika bunduki.

President wa nchi should be a man of good education, sio tu mtu wa standard 8 kama mimi halafu anapelekwa kuwa President of Kenya.

Uhuru wa vyama kama vile iliviopitizwa na IPPG hatujauona, kwa sababu gani? Tumesikia hata hivi juzi tu ama siku mbili zimepita, Mwahima ameshikwa simply because alijulikana kwamba ako rafiki wa mtoto wa Nyachai. Sasa huo sio uhuru tena wa vyama. Uhuru wa vyama ukubalike kama mtu yuko na chama chake awe huru kuwa vile anavyotaka. Halafu pale pale nikiongeza ni kwamba juzi tu tulisikia chama kimetoka kingine, kikaingia kingine ambapo kulingana na chama hicho katika Katiba ile ya mbeleni, ni kwamba mtu akikataa kile chama kilichomwingiza katika Bunge, sasa uchaguzi unaenda kufanywa upya pale. Watu waamue watamuingiza Bunge na chama gani. Lakini sasa ilienda ikavujwa kidogo ama ikapinduliwa watu wakatoka wakaingia kwa chama kingine. Hio isiwe. Kama mtu ametoka chama lazima uchaguzi ufanywe mpya.

Kenya Broadcasting Corporation – Hiyo imekuwa ni ya chama kimoja. Ikiwezekana vyama vyote vipewe fursa na watu wote wana vyama wakubalike. Wanaponeneza jambo lolote wanapozungumza litoke kwa KPA.

National schools zinaingiwa kwa kupitia what people call quota system, all national schools in Kenya. Lakini jambo moja ni kwamba maplot katika mambaraza yetu ya municipality hayatolewi kwa quota system how? Hivi kwamba natoa mfano hapa Voi tuko Wataita na hali utaona plots zimetolewa mtu yeyote mwenye uwezo wa kifedha anapata. Na ni wengi kwa sababu Wataita hatujakuwa matajiri. Halafu utakuta wengi wamebahatisha wengi wanachukua zile plots kwa sababu ya pesa zao. Sasa plot zinatolewa mahali popote katika municiple areas zitolewe kulingana na quota system.

Mayor achaguliwe na wananchi kama vile Rais anapochaguliwa na wananchi. Na pia nataka mtu awe na one job at a time. Tunaona katika Kenya yetu ya sasa mtu mmoja ni chairman wa huku, chairman wa pale, hizo zote anazifanya ni kazi ambazo zingepewa watoto wasifanye. Kwa nini tuna mtu mmoja anafanya kazi kumi. No. One man, one job.

Na kuchagua wabunge, kuna mwenzetu alikuja hapa aliposema ya kwamba wabunge wachaguliwe na watu wote, wenzangu wakamake, lakini mimi nilimuelewa. Ni hivi, wabunge wa watu waende pale kizibani, kila mtu achague yule anamtaka. Maanake ule mtindo mara nyingi tumeona rigging imefanyika hata wale walioko ndani wamekuja wametuambia baadaye pale Bwana kulifanyika rigging. Fulani kama angetoa pesa ndiye angeshinda. Kwa hivyo kama watu wamesimama kama wawili ama watatu, wachaguliwe na kura na waweze kupigiwa kura.

Halafu rapping – Hili jambo la rapping limekuwa monotonous. Mtoto mdogo awe rapped, hakika ninasikitika sana. Kama kuna mzazi ambaye ana uchungu na watoto ama na bibi wa mtu awe rapped wanawake should be a man rapping a woman or a woman rapping a man, hii iko lakini inafichwa maanake hao hawasikii, lakini imefanyika even with houseboys. Yamefanyika kwetu. Akipatikana mtu kama huyo awe sterilized. I don't know how a woman is going to be sterilized.

Kuweka pesa katika benki za nchi – Ipigwe marufuku katika Katiba mpya kama itawezekana, yaani mtu asiluhusiwe kuweka pesa huko nje. Pensioners katika Katiba mpya pensioners wote wawe na mfuko wao special. All pensioners nchini kwanza wawe na ukweli kwamba nimetumika katika nchi nangoja siku zangu za kufa. Kwa hivyo kila mwezi ikiwezekana kwamba kuna mfuko uliowekwa special kwamba ana hakika ya kupata, na kado na kule kupata kila mwezi ama kila mwaka kulingana na watu wengine vile wanavioongezwa zile pesa za mshahara, naye pia awe mmoja wa kuongezwa. Kwa sababu gani? Kwani pensioners maisha yake yamebandilika? Duka ni lile lile, njia ni zile zile, nauli ni zile zile, kwa pensioners. Utakuta mtu alikuwa anaenda kupata pension labda 1980 anapta 2000 mpaka leoanapata 2000. Wakati watu walikuwa wanapata mshahara 2000, that time 1980, today some of them are earning 20,000 ama 30,000. Ninaelekea kummaliza. Sasa langu ni kwamba pension iwe imewekwa katika mfuko mmoja.

Halafu nomination ya wabunge na macouncillors hio kwangu napendekeza isiweko. Kama ni wabunge wamechaguliwa kwenye Bunge let them go. But picking somebody because it is a friend or your sister going there, no. Isiwe nomination.

Rotation of Presidency – Mimi pia naunga mkono kwamba President kama kabila moja limetawala katika Kenya, lisitawale mpaka labda pengine naye imemaliza. Sio kabila moja itawale leo kesho tena inatawala, kesho kutwa as if we don't have people in Kenya. No.

Halafu mfumo wa elimu mimi nasema hivi – ibadilishwe ule wa zamani wa Carry Francis ingawaje wengi wanaita ni wale walikuwa na mfumo wa elimu wa Curry Francis wako na ujuzi mwingi wa kufanya hesabu. Lakini hata hivyo urudishwe ule ule wa Curry Francis.

**Com. Abubakar:** Galgai Mwangemi. Jonathan Msigai, Kiondo, Mwambuli.

**Alfred Mwamburi:** Commisioners na wananchi nina furaha sana siku ya leo kuja kuchuckua maoni yetu mahali hapa. Maoni yangu ni kuona ya kwamba hapa tuko tunataka kuzungumza Katiba, yaani sheria. Sheria zenye zilikuwako wakati tuliunda uhuru mpya katika uraya ilikuja ikageuzwa ikamalizwa. Sasa tunaambiwa hio sheria imepinduliwa mara thirty, 30. Lakini sasa tufanye sheria mpya. Bwana Commissioner mimi naona hivi. Jambo lingine ambalo ni la kutatiza katika serikali kwa watu wadogo ambao hawajiwezi, mimi nimekuja pahali ya shule. Pahali ya shule Bwana Commissioner nasema kwamba shule ziwe za bure kutoka juu mpaka chini. Kwa sababu hio inamaanisha kwamba mtu akiwa hana kazi mtoto wake atasoma. Hapa ni nmemaliza.

Nimekuja pande ya hospitali – Hospitali Bwana Commissioner ziwe za serikali zile free kwa sababu watu wa mtu asio na kazi atakufa nyumbani kwa sababu ya pesa. Hapo nimemaliza.

Bwana Commissioner hapo nasema hivi – Habari ya nchi ya Kenya tangu tulipata uhuru tunasikia kila mahali naskia nchi inaitwa squatter. Hii squatter ilinunuliwa na nani halafu sasa mwenye nchi apewe squatter. Serikali ya Kingereza ilipopata uhuru nchi ilikuwa ni ya wananchi na wananchi ni serikali. Kwa hivyo nasema hivi, sina mambo mengi zaidi kitu nataka ni hii, serikali ifanye wananchi wawe serikali si wafanyi kazi kuwa serikali. Maana inaonekana Katiba iligeuzwa. Mwananchi si yeye serikali, mfanyi kazi ndio serikali. Bali mwananchi anapokaa anaishi kama squatter. Sasa mwananchi yuko wapi? Kwa hivyo ningeuliza squatters liondolewe kwa wananchi. Asanteni.

**Com. Abubakar:** Asante sana. Jackson Sekaya.

**Jackson Sekaya:** MaBwana Commissioners wananchi wenzangu nashukuuu kwa sababu nilipata nafasi kama hii na sitakuwa na mengi sana lakini naona mengi yamesemwa lakini huwezi unakosa kitu la kusema. Lakini mtanisikiza kwa sababu ni maoni yangu pia. Kwanza land issue and land body. Actually the land laws ningesema mambo ya ardhi iangaliwe sana kama inawezekana hii mambo ya leasing itoke kabisa nchini ya Kenya, kuwe hakuna mambo ya kulease. Kama ni nchi ya wenyewe tupewe wenyewe na mambo ya kulease tuachane nayo.

Pili sijaona manufaa ya provincial administration – provincial administration ni mkono wa mkoloni wa kunyanyasa raiya wa Kenya. Na singeona kama ni vizuri tukae na kitu kama provincial administration tena katika Katiba instead ninge-suggest kuwe na regional development committees equivalent of councillors and the chief ambao hao ndio watakuwa wanakaa kama ni hapa Voi wanakaa hapa kwa municiple. Tuseme ni Bunge ya hii area ya Voi. Halafu tukae na regional Bunge ya region hio ambapo watakuwa wanaenda ku-present hizo views zao. Instead of provincial administration to replace hio system na a kind of government ambayo inahuziza mwananchi wa pale. Nimeona kama provincial administration ndio inatu-let down kwa maendeleo kwa sababu utakuta the DC is the chairman of all development committees. Na tunapopitiza maendeleo fulani tufanye, inakuwa ni kukutana kwa sababu yeye sio wa hapo. Hajisikiii kibinafsi kuwa yeye ni mwenyeji hapa na itamfaa. Kwa hivyo provincial administration maokni yangu ni kuwa tusiwe nayo nchini Kenya.

Tatu, about Electoral laws – Mimi ninge-suggest kuwa campaign ya urais yenyewe inatosha Ni mzigo kabisa mraiya wa kawaida ufikirie ni nani atakayekuwa. Karibu Presidential candidates wanane ama zaidi kuwe basi i-separatiwe na the other general election. Tu-separate presidential elections from the general election of the members of Parliament and the councillors. Kuwe siku yake ya President na kuwe na siku ingine pia za hawa wengine.

Katika hapo hapo pia, ninge-suggest majimbo iwe pia within that government – in short kukae na wabunge wa jimbo ambao latter on wanaqualify kuitwa senators kama vile tumeona kwa nchi zingine. Katika hio region kama kuna number ya wabunge, instead wote waende kule, wanakutania kama ni headquarter Mombasa nao wanaongea mambo yao ya region. Halafu within them, I am suggesting kuwe na wale wana-qualify, wanachaguana wenyewe wana-qualify kwenda ku-present their development agendas kwa National Parliament. Call it Upper House – kwa Kimombo.

Mwisho ningeingilia kidogo powers za President. Nafikiri hio ndio mjadala mkubwa sana watu wengi wameguzia guzia. The government is the head of government, yeye tena ndiye Mkuu wa Majeshi, yeye pia ndiye mkuu wa vitu vingine viote hakuna kitu kinafanyika mpaka yeye aseme kitu kifanyike.

**Com. Abubakar:** Pendekeso lako ni nini?

**Jackson:** Pendekezo langu ni kuwa tupunguze sehemu fulani za kama Judges, to appoint Judges, kuwe kuna Commission ya Judges, Judicial Commission in a court na inarudisha kwa Parliament, Parliament wana-approve ndio inakaa gazetted. Hio naona Kenya itakuwa kidogo tumepunguza mtito wa huyo. Nashukuru.

**Com. Abubarkar:** Asante sana. Alfonse Mwangima.

**Alfonse Mwangima:** Commissioners mimi ni Mwangima, kwa Katiba ninayotaka ni kwamba katika wakati uliopita tumekuwa na hali ngumu ya kimaisha kwa sababu masingara ya babu zetu na baba zetu na jamii zetu yalitatizwa na serikali zilizokuwako hapo mbeleni. Ningeomba jambo hili liandikwe katika Katiba. Mnyama anapoua raiya, mraiya yule alipwe ridhaa ya million moja kwa sababu amepoteza uhai wake na jamii yake imepoteza mtu wanayemhitaji.

Mambo ya elimu. Mwalimu anapohusika katika mambo ya uasherati ama uzinzi na wanafunzi afutwe kazi. Mwalimu katika shule yake inahuzika na migomo mwalimu yule aondolewe mahali pale. Mambo ya kulipa tuition fee yaondolewe katika mashule kwa sababu yanalete mzigo kwa wazazi.

Police – Police anaposhika mwananchi na apatikane amechukua rushwa afutwe kazi. Police anapompeleka mshitakiwa ahakikishe mshitakiwa ameandika OB na kama mstakiwa yule hajaandika OB awe na haki ya kupeleka hoja mahakamani na

askari achukuliwe hatua na ashtakiwe kama inavyopata kwa sababu wanafunja sheria kwa njia hio. Mwananchi wa kawaida naomba Commission hii, anapokuwa na utetesi fulani kwa shamba lake, kwa nyumba lake, kwa jamii yake apewe kwa jamii yake apewe nafasi ya kutetewa kisheria. Awe na wakari ambaye atapewa na serikali ili haki zake zitimizwe. Judge anapopatikana na makosa ya hongo afutwe kazi na hiyo iwe kama vile bank wanafanya kwamba usipewe kazi ingine tena ya kuendeza kazi ya uakili. DC, DO, chief, sub-chief na wazee wa mitaa utaratibu huu umetatiza watu wengi. Tunaomba hivi, DC akipola ardhi ya wananchi, apokonywe na alipe ridhaa. DO akifanya hivyo hivyo, afanywe hivyo hivyo, chief hivyo hivyo, sub-chief hivyo hivyo kwa sababu hii itakomesha upolaji wa ardhi ya wananchi na kutoa kelele mingi ama vita kwa wananchi. Pia naomba jambo hili unapotaka kuchagua mbunge, naomba Commissioners, mimi nisiende Kilifi ama ukambani kwenda kutatisa watu wa pale kuchagua mbunge wao nampenda. Naomba iwe mtu wa pale mwenyeji mkabila wa pale achague mbunge anayehitaji kwa sababu hii itaondoa ungomvi na chuki na majirani.

Mambo ya uchimbaji wa madini, naomba Commissioners, hii mwenyeji anayekuwa mahali pale, mzaliwa wa pale, mkabila wa pale, ichunguzwe madini hayo yana madhara gani kwa mtu wa pale, inapoidhinishwa kuchibwa.. Pia mwananchi wa pale asaidike na madini yale kwa kulipa karo kama bursaries, kusaidia ujenzi wa mahospitali, na mashule na barabara. Na ikiwa atakaepewa nafasi hio ya uchimbaji wa madini na hatimizi mambo hayo wananchi wa pale wawe na haki ya kumkataa.

Maji – Sehemu zote katika nchi iwe ni haki ya uridhi wa pale. Maji haya itakayokuwa inauzwa wilaya ingine na ile, ile wiraya ipewe percentage ya kuwaridhisha ambayo itaamuliwa na wenyeji wa pale. Wakati wa uwajili uajiri jeshini, ama serikalini ama kwa wizara yote ile kuwe na video ambayo itachukuliwa wakati watu wanapoajiriwa kama hapa hivi kuwe na video itayoendezwa ambayo baadaye itapelekwa Bunge kuonyesha ukweli uliotendeka mahali pale. Na waulizwe wale walioajiriwa kama kweli wako kazini au ni mdarizi au ni danganyivu. Na inapopitishwa na Bunge kwamba mtu yule hakuandikwa alikuwa ni mdanganyivu, basi yule alikuwa muandikizaji achukuliwe hatua na asifungwe chini ya miaka 10, ili haki itekelezwe. Tunaona kunao wengine wanaoenda kuleta chuki na masengenyo na madhalau kwa jamii zingine kwa sababu tuna waganga wengine, na wachawi wanaoruhusiwa kuishi katika na kutatiza jamii zingine. Naomba Commissioners hii, iwapo utatoka hapa na kwenda wilaya ingine na kutatiza jamii ya pale kwa kuwaletea miungu yako migeni, naomba jambo hili kwa sababu yaliruhusiwi hata katika biblia, naomba mambo haya, huyu mganga apewe uhamizo kutoka kwa ile jamii na kwenda jamii yake. Kama ni mchawi arudishwe kwao. Kumekuwa na tatizo kwa jamii ambao kumewakaribisha kwetu, na wanapokuwa na uhalifu inakubalika wao kufanya uhalifu kama wana pesa kila kitu. Naomba jambo hili kwa Commission hii, mtu anapopatikana na uhalifu na sio mwenyeji wa pale apewe migrant. Hio itakomesha uhalifu, mambo yale yameshuka ya kuua na kuuana. Ikiwa utapatikana, wewe umekuja na wewe tajiri na umekuja mahali pale katika town ile na utajiri wako unanyanyaza wengine, pia sheria iseme kwamba ulipe ridhaa kwa wale wafanyi biashara wandogo urihalibia mali zao kwa sababu walipoteza biashara kwa sababu yako. Jambo hilo litatekelesza uwajibikaji katika kila kazi.

Kwa hivyo langu la mwisho ni hili. Kuna watu ambao kawaida hutunda wasichana mimba na kuharibu nyumba za watu naomba Commission hii watu kama hao wachukuliwe sheria watangazwe mtaani pale wamefanya mambo hayo, atangazwe hadhalani, na

afungwe miaka mitano mtu ameacha kuwa mtoto. Pia akipatikana jambo hilo amelitenda kwa mda mrevu maishani mwake, afungwe miaka 30. Mtu atakayeharibu nyumba ya mtu mwingine kwa kwenda na mke wa mtu, mtu huyo apigwe faini 50,000 kwa kwenda na mke wa mwenzake. Hio itakomesha uasherati na kueneza mambo ya kuabukizana ukimwi. Kwa haya machache asanteni Macommissioners. Ninaomba jambo hili kwamba kwenu muniwie radhi. Naomba jambo hili nimeandika hapa hizi karatasi nikpeana naomba Bwana ziwe zimeandikwa kwa sababu zitasaidia sana kutatua hayo. Kwa haya machache asanteni.

**Com. Abubakar:** Agustin Maganga. Mwameko, E. Mwangi, Churchil Njanji, amezaa maliza, Justus Mwandawilo, Mwaisaka Noah.

**Mwaisaka Noah:** Asante sana sina mengi ya kuzungumza bali niko na machache tu. Yangu ni kuuliza Commission hii, ilikuwa tuko na mambo madogo madogo. Tangu mwanzo tumekuwa kwamba serikali imekuwa ikibadilisha Katiba. Katiba hizi zilikuwa zinabadilizwa Bungeni. Siku hizi tumeletewa Katiba tunabadilisha sisi wananchi. Ningelipenda kujua Katiba hizi wakati wa mwanzo wakati wa ukoloni zilikuwa ni zipi zimeandikwa na ni zipi tunazo. Wananchi wanajua ni Katiba ipi, sheria ipi, ingelikuwa inatakikana haswa ibadilishwe. Maanake tunajua kwamba mtu anaabiwa yeye ako juu ya sheria. Aliyeko juu ya sheria labda anaweza kuwa Mungu, lakini sasa tunaabiwa sheria iko kwa mwanadamu. Mwanadamu huyu tunataka kumjua, kwa nini apewe awe above the law? Na tukipewa hivi, ningelipenda kujua, ziku hizi tulikuwa na mila. Okey, jambo la kwanza langu la Kitaita ama la kienyeji ningelipenda kuuliza, tulikuwa na mila za Kitaita, tulikuwa na pombe ya kienyeji, tulikuwa tunaenda kwa milimi ile tulikuwa tunaweza kutoa sadaka kwa Mwenyezi Mungu.

**Com. Abubakar:** Mwaisaka, ni swali unauliza ama ni pendekezo (inaudible)

**Mwaisaka:** Tunaenda pole pole. Zikiza kwa makini.

**Com. Abubakar:** Mimi nataka sana unipatie pendekezo Bwana.

**Mwaisaka:** Nataka hivi tunataka sheria ya above the law iende chini, kila mtu ni mwanadamu. Tumekubaliana hapo? Nataka hivi, tulikuwa na Local Government ilikuwa inatengeneza pombe ya kienyeji. Tulikuwa tunapewa hata ruhusa. Tunafanya harusi za kienyeji, tunaambiwa, "Harusi yako ya kienyeji tengeza kapombe kako, mtahili mwanawe." Siku hizi imeambiwa ni mtu mmoja aliamua kwamba akina mama amsheni mikono, hamtaki pombe ya kienyeji hapa Taita? Huko upande wa juu iko. Hapa Coast Province twaka je?. Twataka hio pombe na mila zetu zirudi. Sawa? Twaelewana? Niendelee? Police wamekuwa, harassment, tulikuwa tunasema police kwamba wao ni peace makers, watu wa kuweka 'utumishi kwa wote,' peace makers. Siku hizi wamewachiliwa huru na serikali. Wanaenda kushika watu wa pombe ya kienyeji. Hawa watu je sheria mngeliweza kutuambia ilikuwa namna gani? Hapo sijui. Tulikuwa tunafikiria nauliza swali na utaniabia kwa sababu mimi nilikuwa sijui.

Ofisi ya DC ilikuwa inasemekana kwamba maaskari wa DC ndio wao walikuwa wanatakikana kushika mwenye makosa. Police ni peace makers. Niambieni, uhongo imeharibika, wananchi wameharibika, uchumi umeharibika, je tutafanya namna gani Taita hii? Hapa Taita. Sawa? Tunakubaliana? Usinywe maji kwanza nitakulipa peni.

**Com. Abubakar:** Sasa sikiza kwa heshima yako, na kama wewe huna pendekezo wapatie wale ambao wanaweza kuwa na maoni.

**Mwaisaka:** Nauliza hivi, pendekezo langu. Hii National Park, kwa nini bado iko under Royal family badala ya kuwekwa kwa Wataita? Asanteni sana, kwa nini bado iko under Royal family badala ya kuwa kwa Wataita ,kile kitu kidogo Wataita wapate, ama watu wa Pwani wapate. Madini inatolewa hapa inaenda bado, twahangaika. Watoto wanasoma tuko na watoto university wangapi? Watoto bado na wangapi form four? Kwa nini sisi tunapata taabu? Sisi tukiwa wazee tunapata taabu. Madini inatoka hapa. Tufanye namna gani? Fanya hivi uchumi kidogo unatoka hapa kwa National Park utoke kidogo uingie kwa either kama ni council, ama kwa wananchi direct.

**Com. Abubakar:** Sawa sawa. Asante. Jiandikishe pale. Lazalo Mcheki, Wilson Mwakina.

**Wilson Mwakina:** Jina langu Wilson Mwakina. Bwana Commissioner mimi naomba hivi. Kitu tungependelea kwendelea nacho ni majimbo. Neno la pili lina-cover na kitu kimoja. Kitu kimoja ndicho hiki, wana commission: leo unapeleka mtoto hospitali Voi. Ukimpeleka hospitali Voi, ugonjwa unazidi atapelekwa hospitali Mombasa. Yule yule mtu mgojwa. Anapelekwa hospitali Mombasa, yule yule mtu ulimpeleka hospitali Voi. Akipelekwa hospitali Mombasa, akienda ugojwa unazidi. Ugojwa ukizidi maisha inamalizikia Mombasa au Nairobi. Unaabiwa mgojwa wako alipelekwa Nairobi. Sasa wewe uko hapa Voi tu hukupeleka mgojwa wako kule. Unasikia simu mgojwa wako amekufa kule Nairobi. Sasa mtu huyo mliompeleka hatuna tena. Hebu hilo swali wananchi mnisaidie, au Bwana Commissioner swali hilo kama ni wewe ungelichukua aje? Apana kutingiza kichwa wewe niambie swali kama hili wewe mwenyewe ungelichukua kwa upande gani?

**Com. Abubakar:** Mimi nilikuja kuchukua maoni yako mzee. Kama huna maoni wapee watu wengine nafasi.

**Wilson:** Unajua Bwana Commissioner kuna maneno mengine mtu anazungumza hata wewe ukikaa uone ala, je?

**Com. Abubakar:** Uko na swala lingine ama umemaliza.

**Wilson:** Bado sijamaliza Bwana. Neno lingine ni hili Bwana, hapa tumekaa hapa, kuna watu wanatoka bara wanakuja Voi. Wakija Voi wanakuja wanaomba mahali pa kufanyia biashara. Badala ya biashara kesho, anaomba mahali pa kujenga. Na hilo ndilo linatatiza leo Bwana commissioner na ndugu zangu tuna watoto tunazaa. Leo wewe uliotoka bara ukawacha kujenga

kwenu, huyu mjukuu wangu atajenga wapi leo? Huyu mtoto ninayezaa, au anayezaliwa na ndugu yangu leo hebu niambieni mliosimama hapa, nitampeleka wapi huyu mzee?

**Com. Abubakar:** Maoni yako ni gani? Ulikuwa unataka aje?

**Wilson:** Nataka mtu wote ametoka bara, hatumuulizi biashara. Akondeshe nyumba kama hili afanyie biashara yake.Akifanyia biashara yake akichoka nyumba aiache.

**Com. Abubakar:** Umemaliza? Jiandikize pale. Mwalinda Mwandoyi. Mwachela.

**Joseph Mwatela:** Tume ya Katiba na wananchi wenzangu hamjambo? Mimi nasema hivi katika nchi ya Kenya tunayo makabila karibu 42, na vile tujuavyo vile ni lazima tupate kiongozi kutoka kabila yoyote. Lakini kitu ambacho mimi naomba ni kwamba kiongozi yoyote atakayechaguliwa iwe kutoka kabila yoyote ile, awe ni kiongozi ambaye hana umbaguzi, ambaye anastahili na ana hali za uongozi. Na hatumchagui kwa sababu ya ukabila wake, ama ya upwani ama ya uwapi, lakini tunamchagua kwa sababu ana hali za uongozi na atakuwa na haki kwa wote. Hio ndilo pendekezo langu.

Pili katika serikali yetu ni lazima kuwe na ile mikono mitatu ambaye ni Judicially, Executive na Legislature. Kila mkono upewe mamlaka yake na uachiliwe kutumia mamlaka yake kwa ajili ya watu wa Kenya mpya kwa jumla. Bila hivyo kama lingine tutaingilia nyingine nafikiri hapo tutakuwa tunakosea haki kwa nchi ya Kenya na kwa mwananchi kwa jumla. Kiongozi ambaye amechaguliwa na wananchi ni lazima ajue kwamba Katibani sheria kuu ya nchi, na ana haki awe na wajibu kuitunza, na atuambie hivyo kuwa ataitunza, na ajue kule anapokwenda mahali patakatifu, awe tayari kulinda corruption isiingie na watu wake na marafiki wake na ndugu zake wajue hivyo kwamba, kama yeye Rais, si Rais wa ndugu yake, si Rais wa mke wake, si Rais wa rafiki yake lakini Rais wa nchi ya Kenya kwa hivyo atunze corruption isiingie pale. Manake inapoingia utakuta kwamba serikali hio inakuwa ya watu wachache, na wale raiya wanafuatwa bio, na kuhangaishwa. Kwa hivyo tunataka atunze Katiba ya nchi na pia alinde aone kwamba corruption haiingi, kwa sababu inapoingia ndio chanzo cha maovu na ummaskini wa nchi na kwa wananchi kwa jumla. Kwa hivyo tunaomba kwamba atunze Katiba na pia alinde corruption isiingie katika nchi. Asanteni.

**Com. Abubakar:** Joseph Mwamburi.

**Joseph Mwamburi:** Asante sana Bwana commissioner na waliokuja kusikiliza na kutoa maoni. Maoni yangu kuhusu elimu. Elimu ilioko sasa ibandilishwe iwe elimu ya zamani. Kwa mfano zamani kulikuwa na elimu ile ya standard 7 na form 4 na university. Isiwe kama ilivyo sasa. Kuhusu hawa walimu wanaofundisha shule kwa wakati ulioko sasa, walimu wasiwe wanachukua mamlaka kuliko committee ya shule kwa sababu mwalimu mwingine akija mwalimu mkuu basi amekuwa yeye ndiye anachukua mamlaka kuliko wenye shule ambao ni committee ya shule.

Halafu kuhusu watoto – Haki za watoto ziangaliwe kwa mfano sasa kuna watoto wengi ambayo wanaoranda mtaani ambao ni mayatima hawangaliwi na pia ni viongozi wa kesho. Kuhusu mayatima hao hao katika waetima kuna walemavu. Walemavu shule zenyewe za walemavu haziko hapa, ningelipenda katika mikoa ama katika district shule ziwekwe za walemavu ili wapate kuangaliwa. Kuhusu walemavu hawa hawa ambao pia ni watu wazima, majengo ambayo yanajengwa yanastahili kujengwa katika hali ile ambayo itastahili ili ulemavu kuna stairs kwa mfano hapa mlemavu hawezi kupanda. Kwa hivyo mlemavu pia aangaliwe.

Nikiangalia kuhusu hali ambayo tulikuwa tunazungumzia, raslimali – Raslimali zilizoko katika district kwa mfano ya Taita Taveta kuna madini. Madini, wanaostahili kufaidi ni mwenyeji. Ikiwa kuna mkuja ambaye amekuja asipewe kibali cha kuchimba madini katika eneo ile. Mwenye madini ni mwenyeji, mwenyeji apewe kibali ndio wakitaka kuelewana, waelewane. Halafu usawa wa kutoa hiki kibali tunaona kwamba viongozi wengine ambao wana ndugu zao kutoka huku sehemu hizo zingine, akitoka hapa kupata kibali ni rahisi lakini mwenyeji wa eneo lile kupata kibali si halisi. Kwa hivyo kuwe usawa.

Halafu kuhusu hii raslimali, kuna raslimali kwa mfano kama maji. Maji yayotoka Mzima springs inaleta sector mingi. Inayoleta faida nyingi katika serikali yetu ya Kenya lakini mwenyeji ama wale ambao wanaishi katika jiji ile hawafaidi. Kwa hivyo ikiwa kwamba kuna mkoa wa Nairobi wanafaidi watoa raslimali zao kwa hivyo na sisi tufaidi. Kwa hivyo tufaidi kwa maji, ikiwa idara la maji ikitoa malipo yale tunalipa seventy 70% iende kwa serikali, 30% itumike hapa hapa. For example tuko na tunatoa kodi lakini yale hayatumiki hapa. Tukiangalia nchi tunasema kwa mfano tunaitwa na hili jambo nazungumza ki-group kuna mchanga ambao uko katika mto, ni raslimali. Unakuta ya kwamba mchanga ule badala ya mwananchi afaidi, mwananchi anatoshwa kodi ama cees. Mwananchi yule anastahili kufaidi bila kulipa chochote kwa sababu ajimudu kimaisha. Kuna mawe pia halikadhalika, tukiangalia kwamba kuna hizi tuseme kwa mfano forest, kuna hizi forests ambazo serikali imeweka ambazoo zinaangaliwa na serikali kwa jumla. Lakini unakuta kwamba katika kuaminiwa ile inambiwa iziingie katika msitu ule na isikate msitu. Misitu ile irudi kwa wananchi yaani irudi kwa wazee ili wawe wakiangalia ile misitu. Na ikiwezekana kama eneo lile yale maeneo ambayo ni ya msitu kubwa kubwa. Mayatima ama akina mama ambayo hawana ardhi ya kutosha, ni heli wapatiwe ardhi ile wapati kusaidikia.

Halafu tukiangalia kuhusu uchaguzi ama mamlaka – Mamlaka President asiwe na mamlaka zaidi akiwa na makosa ashtakiwe. Halafu kuhusu uchaguzi – tukiangalia kwamba katika hizi serikali za mtaa – serikali za mtaa kiongozi anaestahili kuchaguliwa awe na elimu minimum education provided hata kama amefika kiwango gani ajue kuandika na ajue kusoma kwa sababu ndiye ataishi na wananchi vizuri. Tumeona wale ambao wamesoma kupitia elimu ile zaidi hawezi kuishi na mwananchi yule ambae hajafika kiwango cha chief.

Halafu katika huo huo uchaguzi, tukiangalia ni hawa wabunge. Hawa wabunge wasiwe wakienda Bunge bila kutoa maoni kwa wananchi kwa sababu kuna mbunge anaweza toka anaenda kuripoka kule lakini yale maoni atatoa ya wananchi. Halafu

mbunge huyo huyo, awe akizungumza mambo ya eneo lake kwa sababu kuna mbunge anazungumza eneo lake hawezi kuzungumza ile inatakikana kuzungumzwa katika eneo lake anazungumza eneo lingine.

Halafu kuhusu pension – Kuna akina mama ambao wameachwa na Bwana zao na baada ya kuachwa na maBwana zao badala ya kupewa hio pension, wanahangaizwa mpaka ule mda wa pension unaisha. Unaelewa ya kwamba baada ya miaka mitano yule anastahili kupewa pension kwa miaka mitano. Baada ya kule kuhaingaishwa ile miaka mitano ikiisha zile pesa zinaingia humu humu. Twaomba hiki kipengele kirekebishwe.

Halafu kuhusu habari ya mashamba – Habari ya mashamba irudiswe kwa wazee. Na wale wazee, ikirudiswa kwa wazee wajulikane wale wazee kweli ni wa kijiji kile ili watekeleze haki katika hizi landboards ambazo ziko katika kila mkoa ama district hazitekelezwi. Unakuta kwamba mtu si mwenyeji amefika pale halafu anateuliwa kuwa katika land board ile. Basi uhaki hautatendeka hapo.

Halafu kuhusu ugawanyaji wa plot – Ugawanyaji wa plot urudishwe katika municipals zetu hizi council. Kwa sababu unakuta kwamba diwani anasema kwamba plot fulani imenyakuliwa na yeye hajui. Kwa hivyo zikirudishwa kwa council watakuwa wanaelewa kila kitu kitaendelea. Halafu kuhusu hawa land registrer, hawa ambao wanagawanya hizi maplot. Tungeliomba ikiwezekana atakapokuwa huyu land registrer asipewe mamlaka, mamlaka yake yapunguzwe, mamlaka yawe ni ya wananchi kwa sababu akipewa madaraka ndio unaona maovu yanatendeka. Tukiangalia kuhusu hizi pombe ambazo zinaendelea, tunaangalia kwamba kuna miti dawa. Ukiangalia hapo miti dawa inaendelea na pombe ya kienyeji inafanya nini? Kwa hivyo maoni yangu pombe ya kienyeji irudishwe na ikirudishwa itumiwe kimila si ati kutumiwe hivi hivi ati kunararishe, lakini itumiwe kimila kwa sababu imesimamishwa.

Halafu kuhusu hawa chiefs – civil servants tungekuwa tunaomba chief, tuwe tunamchagua sisi wananchi. Kwa sababu chief tukimchagua sisi hatakuwa na mapendeleo kwa sababu kuna akina mama kupeleka pale kushtakiwa kwa vile chief mmekataa kuelewana naye ikiwa mwingine wewe unaelewa. Inaleta shida kwa hivyo chief tumchague sisi pamoja na assistant chief.

Mayor – Mayor tumchague sisi wananchi. Mayor na deputy mayor sisi wananchi pia tumchague. Macouncillor wao wasichague mayor. Mayor ni sisi tunachagua. Halafu kuhusu, ninapoendelea kummaliza, serikali ya majimbo. Nilikuwa ninaomba ikiwa kutakuwa serikali ya majimbo serikali ya majimbo iwe na haja ya kufanya nini? Ikiwa mtu ametoka sehemu ya huko, sehemu hizo zingine ambazo actually tuseme kwamba kwa mfano Taita Taveta district ama mkoa wa Pwani awe na kibali kwamba ametoka kule watu wengine wanasema kwamba kuna maovu huwa yanatendeka. Akija hapa awe na kibali na nilikuwa nataka kutekeleza yale yalioko katika mkoa ule ajiandikishe katika mkoa ule awe ni wa pale na kila kitu kiwe kinafaidika pale. Na ikiwa pia yeye amejenga nyumba hapa, akijenga nyumba hapa kwa kuwa yeye ana kibali mambo yake ni ya hapa tunakumbaliana na yeye, lakini naye akubaliane na yale yetu vile tunavyoishi.

Katika hiyo hiyo, serikali isiwe na serikali ya amri maana mnaona kawaida wakati mwingine chief huwa anatutisha sijui what, unaitwa kwa chief. Hio ni amri, ama si hivyo? Kwa hivyo pia hio isiwe serikali ya amri.

**Com. Abubakar:** Asante sana mzee enda ujiandikishe pale. Rev. Ronald Nzai. Daniel Mwasi. Austine O. Omiau. David M. Jonathan. Said Mwangala. Stephen Musinga. David Mwandime. Adam Kamata. Noar Kisingo. Josephat Mwandime. Alex Mwathege. Japhieth Kigoma. Hamisi Makeo. Makeo James. Ronald Mwanyala. Rehema Mwandema. Musa shauli. Zaid Care. Ramadhani Mwangala. Albert M. Zete. Kuja basi.

**Albert Zete:** Macommissioner, wananchi mlio hapa. Kwa majina natwa Albert Mwalimo. Mimi haya yote nimesikia kwa wenzangu ni kwamba si sawa kabisa ninayaunga mkono na hawa wanataka majimbo la madini na hawataki kusema, mimi iandikwe hapa Albert mwalimu anataka kwanza majimbo. Na kama mningeruhusu nimueleze kidogo tu. Sababu ya kusema majimbo kwanza mipaka haiko sawa sawa ile ya ukoloni. Nataka mipaka irekebishwe. Ya pili ardhi na mali ya asili iwe ya wenyeji pale. Biashara vile vile watu wa pale kwanza wapate nafasi ya kwanza kwa jumla chochote kitakapofanyika katika district au katika jimbo iwe watu ambao wamepewa kwanza.

Nafikiri mimi sitakuwa na mengi isipokuwa ningeguzia utawala kwanzia kwa machinani. Maoni yangu ni kwamba tuwe na chief wa kuchaguliwa. Chief wa kuchaguliwa, atafanya kazi jema kwa maoni yangu. Awe na assistant chief mmoja katika kila location. Kwanzia wale wa vijiji wapewe nafasi zaidi kwa sababu wawe wanajua mambo ya huko chini zaidi kuliko hawa machiefs, maassistant chiefs. Jinzi ninavyojua ni kwamba assistant chiefs wanategemea wale wazee wa vijiji. Chief anategemea wazee wa vijiji, police anategemea wazee wa vijiji. Kwa nini tuwache mje tuseme tu Mungu awabariki na huo ndiye anajua watu vijijini. Ningejaribu kuonekana kufanya kwamba majimbo yanafaa na haya vita vyote katika dunia au katika Kenya yetu vinaletwa kwa sababu ya ardhi. Tukiweka ardhi katika majimbo, kwa wenyewe, kwa wenyeji wale watu wa pale, mali ya asili, shamba kila kitu, naanza mukumbuka kwa mfano hapa Kenya tulikuwa na Molo. Tulikuwa na vita Coast Province. Hii ukipelelesa ililetwa na mashamba. Kwa hivyo nazidi kusema zaidi majimbo yatatusaidia hata katika kurudisha amani. Hata ukienda Congo hawa watu wanapigana kila mara ni kwa sababu ya ardhi. Madini yako pale kila mtu anataka kuyamiliki. Ukienda Angola Waisrael sasa na Wapalestine wanapigania ardhi. Hii inaleta vita kila mahali ulimwenguni kote. Kwa hivyo hii ardhi ikirudiswa kwa wenyewe, hii mambo mengi itaisha. Unaweza kuona watu mtu amejenga nyumba yake, Commissioner, na amejenga nyumba na yuko na watoto, na yuko na kitu chochote kule kwa nyumba na amekaa zaidi ya miaka 20. Mtu anakuja asubuhi anamuonyesha barua. Hii barua yangu nimepata hapa ni kwangu, ondoka, na anakuja na askari. Huyo mtu hawezi tulia vile kutakuako. Mauaji yatatokea pale. Hio ndio nataka kusema majimbo yanafaa na hata hapa kwetu Wataita, our Coast Province tumenyanyazwa miaka mingi. Ndio sababu nasema hii ardhi ikirudiswa kwa wananchi mambo mengi yataisha.

**Com. Abubakar:** Mzee wangu tumekuelewa kabisa. Rudi pale mzee. Wilson M. Omar Ahmed.

**Wilson Omar:** Asanteni Macommissioner na wananchi kwa kunipatia hii fursa nitoe maoni yangu. Maoni yangu kwa ufupi,

pendekezo yangu ni kuwe na majimbo. Lakini majimbo yenyewe federalism iwe ni ya economic wise. Yaani ya kiuchumi. Halafu katika ile majimbo, ingefaa kuwe na Bunge la kila jimbo . Kila Bunge iwe ya kila jimbo. Katika hio Central Government ikuwe na Senate ambayo kila district itakuwa ina-represent mtu mmoja aende kwa Senate. Hio itakuwa ni Nairobi.

Na pia ningependekeza kuwe na mfumo wa Prime Minister, kuwe na President na Prime Minister. President apate kupunguzwa nguvu zaidi mambo mengi yawe yanafanywa na Prime Minister kama vile kuchagua mawazili, iwe ni Prime Minister lakini lazima wapitie kitu yaita vetting. Wapelekwe katika Bunge iwe yaangaliwa record yao yafaa kweli wapatizwe.

Ingine nitaingilia ni mambo ya ardhi. Ardhi imekuwa jambo moja limetatiza watu wengi na ingefaa ardhi yote imilikiwe na wawe wenyeji wa pahali hapo. Ikija transfer iwe transferred kupitia wale wenyeji.

Pendekezo langu lingine ya kua siku kama hapa Voi tunakuwa twatoshwa land rent. Inatoshwa na Central Government na hio ni ya Nairobi na hapa municipal tuna land rates. Kama mimi kwa mfano nalipa land rates to the municipal ya voi 40,000 kila muaka na land rent ya hio hio ardhi ni 8,000. Kwa hivyo hatuelewi hii ardhi kwani twalipia mara ngapi? Ingefaa iwe kama ni municiple, municiple peke yake ndio wanalipiwa because katika ile mfumo wa majimbo wawe wakipokea 75% ingefaa kila raslimali inayepatikana katika kila jimbo lile linaweza likabaki pale. 25% ndio itoke iende kwa Central Government ndio isaindie kule.

Nitaingilia sasa mambo ya ID - imekuwa na shida sana kama hapa Voi nafikiria hapa district yetu tunaitwa Border District kwa hivyo kupata ID ni shida sana. Inaweza pata ID ukapata ile barua ya kungojea ID usipate pia miaka miwili, miaka mitatu. Kwa hivyo hii ID mambo yake yawe yanaharakishwa. Kila mtu ana birth certificate aweze kupata ID. Basi na yule alizaliwa pahali hapo hapo lazima apate ID hapo hapo. Na kusiwe tena mambo mengine kama saa hizi tuna ID, tuna passport, tuna voting card hizi vitu lazima ziwe consolidated iwe ni kitu kimoja, si mtu anabeba vitu 20. Na pia tusiruhusu vitu kama dual citizenship yaani mtu anaishi yeye ni Mkenya ni Mtanzania ni nani yuko nchi zote ana vipande vya hizo nchi zote, haitawezekana.

Jambo lingine ningependa kuguzia ni juu ya hawa police, tuna police, tuna AP, tuna stock theft, tuna GSU yaani tuna kila aina na nchi ni ile ile ndogo, watu ni wale wale. Kwa hivyo pendekezo langu lilikuwapo ni kuwa kama anti stock theft hawana kazi waondolewe. GSU, police pia wafanye hio hio kazi. Kwa hivyo tupunguze hizi forces kabisa kwa sababu forces zenyewe tunaabiwa kila siku hawa ndio wanachangiwa pesa nyingi. Pesa nyingi inaenda department of defence. Hio haitafaa kwa sababu sasa walimu saa hii wapiga kelele wataka pesa hawawezi wakaongezewa.

Nyingine ningetaka kuguzia ni juu ya Chief Kadhi – Chief Kadhi mimi nikiwa muislam nataka tuchague sisi asichaguliwe na President na awe na wadugu wake na Chief Kadhi awe na koti yake, yeye awe ni kama Chief Justice na akiwa na wale Kadhi wake wao pia wawe kama wako judge. Na wao wao wanaweza wakafanya lolote lile katika Muislam kila kitu chamhusu

Muislam. Ningependelea yeye awe anaweza akafanya kazi yote kama Judge mwingine. Yaani anaweza akawa na appeal court, unaweza kupeleka appeal kwake, unaweza kupeleka case si kila siku ati serikali kazi yake nikufungiza ndoa, kufungia watu, uridhi kwani tutashida hapo? Kwa sababu mwanzo wa dakika hii Constitution ile inaweza ina-recognize kuna kitu kinaitwa Uislam. It should recognize Islam as a religion. It should respect its rights and practice of religious activities. Si mimi naenda kufanya fasting wakati wa kuswali nakatazwa. Na mimi kwangu dini yangu yaniruhusu niende nikafanye ni lazima. Ningeachiliwa nikaswali dakika tano. The Constitution should protect Muslim's right and implementation of those right by Muslims at all times.

Kwa upande wa elimu – Elimu kuna college yetu hapa yaitwa Mitindani. Mitindani mwalimu akifaulu pale hawezi akaandikwa na TSC kwa sababu anafundisha na I.R.E. Sasa tunakuwa na walimu wachache wa kufunza dini. Lazima na wale wawe wanaruhusiwa nakatika agizo la teachers colleges lazima kuwe na Islamic education, just like any other one. So that ukichukua IRE nataka kufanya Islamic religion na pia naweza ukafunza Geograhy. Hio pia ningependa ifanyike katika Bank. Waislamu haturuhusiwi kitu chaitwa labour. Kwa hivyo lazima katika hii Constitution turuhusiwe tuwe na mabenki zetu na mavazi yetu yakubalike. Mtu akifaa ijabu siku zitafuata.

Kitu cha mwisho ningetaka Parliamentary powers to be limited, kwa sababu tunakaa hapa leo hii MP anajiongeza mshahara yeye anaongeza leo laki moja kesho laki mbili, kesho kutwa laki tatu vile anavyotaka. Lazima kuwe na kipengere Fulani kiwe kinawazuia kwa sababu sisi, we are the tax payers. Lazima kuwe kuna kitu ambacho kinawazuia wao wasiwe wanaweza kujiongezea kwa sababu MP akizajiongezea, judge naye na mimi pia na tunapata mara mbili yake huyu. Kwa hivyo hatuwezi tukaishi katika mfumo wa aina hio. Asanteni.

**Com. Abubakar:** Asanteni sana. Julius Masela. Wilson Mwangombe, Grace Kiseu.

**Grace Kiseu:** Macommissioners na wote waliohudhuria kikao hii, nashukuru kwa nafasi hii. Nami singetaka nitumie mda mrefu isipokuwa nataka tu nitaje machache. La kwanza jina langu ni Grace Kiseu kama mlivyoambiwa. Ningetaka kutaja kuwa Voi ni municiple council lakini hatuna ile faida ambayo wenzetu walipata wakati zile municiple council za kwanza kama vile Thika, Mombasa, Nairobi. Wao wakifanywa municipal council kulikuwa kuna hospitali, kuna mashule, kuna mpaka MPO, municipal education officer, nakadhalika. Hapa Voi tuko tu na hili nyumba peke yake sijui kama tuna shule yetu. Kwa hivyo ningependa kukifanywa machanges tafadhali mabadiliko kama hayo, kama kwa mfano municipal council iwekwe pia serikali iwe imetengeneza hali ya kuwa kuna hizo hospitali za municipal ambazo zina manurses na watoto wa Voi wanapata kazi. Kwa mfano sana sana nasema upande wa Voi manake wanakuwa wanajengewa kimunicipal walimu pia kimunicipal, nakadhalika ndio tusikie ile uzuri wa municipal lakini hapa tumendanywa.

La pili, pia sewage iwe haiko katika hali ambayo niya ki-muncipal. Kwa hivyo tuseme ya kuwa katika changes zozote yaani kwa changes ambazo serikali itafanya iweke hali ambalo ni ya standard, kusiwe na sub-standard.

La pili kuna hii elimu ya bure ambayo tumeambiwa – Elimu ya bure kwa kweli wakati shule wakati shule zilifunguliwa walimu walikuwa na shida sana, maanake kuna elimu ya bure lakini haieleweki ni elimu ya bure kivipi. Kwa hivyo hapa ningesema pendekezo langu ni kuwa kukifanyika mambo kama hayo elimu sasa ni ya bure ieleze kabisa kinaga uBwana ni ya bure to which extent. Ni uniform watoto watapewa na vitabu na nini na nini, ama tu ni elimu ya bure, halafu kesho activity fee kesho sijui hili na lile basi kuwe na maelezo kama hayo. Free education to what extent iedezwe vizuri na serikali katika hio Katiba.

Bursary –Wengi ambao wanapata bursary ni watoto matajiri na hao matajiri pendekezo langu ni kuwa ikijulikana wewe ulikuwa ni tajiri hata miaka 20 iliopita na watoto wako wamesoma wamepata madegree na nini, ni maprofessor na nini, ulipe pesa hizo kwa sababu ulikuwa ni tajiri ama hawa watoto wako watajiwe walipe ili yule maskini pale chini ingawa maskini atakuwa wasi wasi hawakusoma lakini wale watakuwa bado wanasoma wasomeswe na zile pesa ambazo zime-deductiwa pengine kutoka kwa mshahara wa huyo tajiri ama hawa watoto wa matajiri kwa sababu ya ambao unasoma na wewe ni tajiri wewe wajua babako ni tajiri ukisoma si unajua tunasoma kwa pesa za wawili? Kwa hivyo tafadhali iandikwe kwenye Constitution yetu ambaye atajulikana ametumia pesa za bursary kwa undanganyivu itafikia miaka fulani ambayo itajulikana na ikijulikana hizo pesa zirudizwe katika huo mkoa hio bursary committee isomeshe mtu ambaye ni maskini.

Lingine land grabbing – Waliogunduliwa wamegrab land tafadhali wakijulikana hiyo land ichukuliwe tena ilipewe kiharari na wewe upokonywe hio title deed na usiwe na mamlaka tena ya land hio.

La tano ni kuwa Presidential term ifike miaka 10. Sio kwenda na kwenda na kwenda wakati mwingine vijana wanasema ina-bore.

Haya lingine, kuajiliwa – Wameoajiriwa kama kwa mfano kwazia tarehe mbili na kwendelea walimu watakuwa wakiangaliwa kwa kila mkoa kufanyiwa interview. Kwa kweli watu wengine wamezungumza lakini kuna jambo la kusikitishe kuwa hapa katika mashule yetu kuna kila kabila ya mwalimu hadi kuna watoto wetu wenyewe Wataita ambao hawana kazi. Wamesomea huo walimu lakini hawana kazi. Sasa wanaitwa katika interview wale ambao wanachukuliwa ni wachache labda katika TTC, hizi mateachers colleges, ni wachache wa Taita. Na ni watoto wengi wako na C and above. Hilo likijulikana ambao walifanya hio interview basi nao pia wachukulie hatua, ambao walifanya interview na hawakuchukua wale ambao wanahitajika.

Na pia hapo pia ningesema ile quota system itumiwe kwa hali nzuri. Kuwe 85% ya wale wananchi wa hapo hapo wachukuliwe watoto wa hapo hapo Taita, wa hapo hapo sijui ni wapi wa nchi gani ya Kenya wachukulie waende TTC wajisomee warudi waje wafundishe mashule yao.

Lingine ni kwa upande wa Constitution – Constitution review iwe inafanywa kwa wakati fulani fulani. Sio tukae miaka 39 ndio tufanye nyingine. Isipokuwa tuwe tuna ile constant review ambayo sasa haikwambatani pengine na uchaguzi au na hali ingine

yeyote ile. Na katika education syllabus kwanzia kule chini, Watanzania husema shule ya vidude zile nursery school waanzizwe vile abavyo tuna HIV syllabus iko juu juu kwa mashule. Kwanzia kule chini watoto waanze kufundishwa kwa njia fulani pengine ya kiutoto hivi kama ni kwa nyimbo zao na nini na nini waendelee hivyo hivyo mpaka kitambo wamalize chuo kikuu hata hakuna mambo ya kuuliza hii Katiba ni kitu gani. Washaijua ijua wao wenyeye.

Lingine ni mishahara – Serikali ikitangazwa walimu wapate mishahara pia mtu mwingine serikali asiongezwe kwa sababu kama hakuna mishahara iwe ni equal kwa kila mtu hakuna mishahara mpaka serikali itakapopata pesa sio wengine wanaongezwa wengine hawaongezwi. Unashindwa sasa hii ni serikali hio hio moja ama serikali ya wale wengine ni tofauti na ya hawa wengine.

Lingine nalo ni hili – Tabia ya wanawake kuridhiwa, kuna msemaji mmoja alisema mtaniwia radhi lakini ya wanawake kuridhiwa hio nimeweka X, hakuna. Tusikubali kwa sababu siku hizi kuna ugonjwa wa ukimwi kuna mambo mengi, haya mambo ya wanawake kuridhiwa katika Constitution yetu tusikubali. Kila mtu awe na haki yake, mwanamke mwenyewe akijiamulia sawa lakini sio iwekwe hapo kwenye Katiba wewe ikifia unalidhiwa na X. X akifiwa anaridhiwa na Y, hakuna. Isiwe yenyewe imewekwa kwenye Constitution, hio ni very serious.

NGOs – NGOs ambazo zinakuja katika tarafa zetu ama katika Taita Taveta district ama district zozote zile, ziwe zinaendelea kufanyiwa constant review pia hizo. In case hio NGO imemaliza miaka 5 haijafanya lolote la maana, ni kazi gani? Mwaileta hapa ya nini? Iondolewe. Isiwe tena yaendelea kukaa hapa yaendelee kutundanganya watu na nini miaka nenda miaka rudi. Ifanyiwe review na hao kwa serikali na hawa leaders wa nyajani pia waseme kwamba sisi haturidhishwi na hii NGO. Five years ni sawa hatujaridhishwa tuachane nayo.

Lingine ni kwa huyu Rais wetu – yaani kwa kila kitu, ni kwa vyuo vikuu, ni kwa kila mahali, tafadhali ningesema kwanza kwa upande wa vio vikuu asiwe chancellor. Sisemi ati Rais huyu present lakini hata in future tusiwe ati huyo huyo President ndiye chancellor wa all universities, no. Tuwe na professor fulani ambaye amesoma amehitimu awe ndiye mkuu wa chuo kikuu. Sio mtu wa standard 8 ndiye mkuu wa chuo kikuu. It cant happen. Hio haiwezekani.

Lingine ni katika hizi macommission tunafanya matume mengi. Kulikuwa mpaka hii ya 8-4-4 ilikuwa ilifanywa juzi hapa hivi. Ikafanywa lakini baada ya hapo hizo Commission zote zinakuwa dumped, kuna dust bin yake yakuwekwa. Hivi msishangae macommissioners wenzetu hapa. Sorry, si wenzangu, macommissioners msishangae baada ya kufanya hii kazi yote mkaongezewa miezi 8 ikawa dust bin bado iko, lakini serikali ya Kenya tafadhali ilete katika Constitution hii mwandike hata kama ikiwa kwa dust bin bado hio inasema hivyo hivyo tusiwe dumped hata kama itakuwa dumped.

Lingine – Nikuwa kuna hii tabia ya ministers wanachaguliwa ambao hawajahitimu katika upande huo. Kwa mfano mmoja alisema hapa wewe pengine ni mtu alikuwa mkuu wa majeshi wawekwa upande wa health, jamani do you have anything

yafanana na pengine kulenga bunduki, lakini ni kitu tofauti kabisa. Kama wewe pia wawekwa minister wa education uwe ulisomea elimu at least to some extent even at least kwa masters level, ndio u-become minister of education, ndio elimu yetu nayo itapanda.

Lingine tena ambalo mimi nafikiri ni la maana sana ni kuwa kuna, hii polio injection watu walikuwa wakipewa hapa Pwani. Hakuna education yote watu walifanyiwa. Hizo mapolio kweli twapewa tena only Coast Province kwa nini? Kwa nini isipewe watu wote? Na tena kama ni kuangalia hio sio polio lakini tetanus. Tetenus nani yuko katika side ya tetenus? Mwenye atahitaji ya tetanus nafikiri ni yule pengine mchungaji pale, hawa pastoral communities Wamasai, wanaume kwa wanawake, wanini wale. Lakini sasa wewe una kaa pale sokoni tetanus itakuguza saa ngapi? Kazi yako ni kupanguza panguza nyumba yako chini hapa tu, nini hapa wakaaji wa Pwani. Upanguze upange mandazi yako tetanus saa ngapi? Sasa bona hiyo kila undundwe sijui mara ngapi? Mimi kusema kweli sikubaliani na mambo mengine. Nafikiri katika hio Constitution mwandike kuwa kama watu watafanyiwa chochote especially cha kuhusu mwili, basi wapewe elimu kwa mda fulani na wakubali, halafu watakapokubali basi wafanyiwe hivyo.

Haya, lingine ambalo nafikiri litakuwa ni la mwisho ni kuzungumzia juu ya wasichana ambao wanaolewa kwa umri mdogo. Kwa mfano utakuta mzee fulani ataka bibi wake wa sita ama wa saba wa 10 years old. Huyo akienda akitolewa, hapa hakuna kitu ya kuficha lakini mimi nimeshuhudia kabisa. Msichana hapa aitwa Malungu mdogo kabisa ambaye ameolewa akatolewa na alipotolewa sasa ni kama watu wanafichaficha hata hakuna neno, hakuna neno, lakini haya mambo yanaendelea. In our district may be kwa percentage kidogo lakini ina affect huyo msichana may be angekuwa ni President in ten years to come. Sasa umemuacha huko, kwa hivyo nasema wasichana kama hao wakitolewa yule mtu kado pengine na kuwekwa korokoroni, yeye pia ahihakikishiwe kuwa ni lazima by court order atatoa pesa ya kumsomesha huo mtoto mpaka amalize, na hana mamlaka ya kumuoa. Huyo mtoto amsomeshe na ikiwa hapo katika Katiba yetu nina uhakika kuwa kina mama, watoto na hata watu wengine wote especially la mwisho kabisa ni education. Chochote ambacho kitafanyiwa tuwe tunakuwa educated in advance. Nashukuru sana.

**Com. Abubakar:** Asante sana Grace. Geoggrey Njenga.

**Geoggrey Njenga:** Bwana Commissioner, na wananchi wenzangu hamjambo? Mimi yangu ni mambo matatu peke yake na moja imezungumziwa na watu watano na mimi ni wa sita. Kwa hivyo mtanisikishe tu halafu imeandikwa kwenye record.

Kwanza ni mila na utamaduni – Mila na utamaduni ni wetu sisi Wafrika popote ulipo na kuna sababu hii unapotaka uolewe wewe ama unaoa kuna mambo hufanywa kwenye arusi ya kienyeji. Mambo hio kwanza hapo kuna kitu inaitwa pombe na bila pombe hio arusi ya kienyeji haiendi mpaka yule msichana atapewa ile pombe apewe namkono wake ashike ambiwe shike hii baba yako wa Kikuyu. Baba shika hii pombe hata kama ni ya kitamaduni haikudhuru hapa. Hio ni kuonyesha ya kwamba ameruhusu ile arusi iendelee kimila. Pombe hiyo hiyo tukiondoa hiyo hapo mila na utamaduni kuna wakati wa kunyua pombe

watu waki-chargiwa kimila mpaka sasa tunapinga upande mwingine, upande wa wanaume hatujapinga. Tuna mila na pombe mpaka iwepo mila hio haitakuwa sahihi kabisa. Hii ina maana kwamba pombe ya kienyeji irudishwe kwa Katiba hii.

Mimi mzee hapa, na huyu ni mzee anataka tuzungumze mambo fulani kwake nyumbani. Anapika pombe vibunyu viake viwili vitatu, anamtuma mtoto wake wakiume nenda kwa mzee fulani mwambie namuita.

**Com. Abubakar:** Tumeshaa andika hio chini mzee wangu. Tumeandika hio. Enda ingine, point ingine.

**Njenga:** Okey. Kuna ingine ya pili ni Katiba – Katiba hii tunaenda kuandika hapa ina maana kubwa sana. Ina maana kubwa kwa sababu pasipo hii Katiba hatuwezi kuishi vizuri. Mimi napendekeza hii Katiba ifanyike mpaka ifike mwisho isiwe nusu nusu ati marekebisho madogo ati tufanye uchaguzi na Katiba ya zamani. Hio andika, tumekataa sababu zamani Katiba hii hakuna kitu tumefanya. Above the law haitakuwa chini wakati huo lakini Katiba ikija above the law itakuwa chini. Mimi nasema hivi na uandike hapo. Masaa inakwisha sana tufanye masaa 24 lakini Katiba ifike mahali Prof. Ghai alisema isifike hapo na uchaguzi ujao ufanywe na Katiba mpya. Hio ni ya pili.

Ya tatu, kiwango ya vyama – tulisema kwamba tunataka vyama sita. Mimi napendekeza vyama viine. Vyama viine vipi? Ichaguliwe, KANU, Ngilu, Kijana Wamalwa na DP. Yangu ni hayo.

**Com. Abubakar:** Simon Katembo. Francis Onyango.

**Francis Onyango:** Macommissioner na wenzangu wale wamekuja pia kushiliki katika hii mambo ya kuandikisha Katiba, mimi nina matatu. Haya matatu nilikuja hapa saa nane kuna mwingine alikuwa ashaazungumza nyumma. Kwa hivyo kama nitakuwa pamoja na wao nimeshukulu kwa kuwa tumeungana. Jambo langu la kwanza ni hili – kuna kitu ambacho kinaitwa ushilika au mashirika. Haya mashirika macommissioner yanatutisha kwa sababu haya mashirika yanachaguliwa mtu. Kama mimi ni Francis Onyango napenda kusimamia hio ushirika natafuna mpaka niangushe halafu hio shirika inauzwa. Mimi Onyango hakuna pahali yoyote natolewa ninapelekwa kwa shirika lingine. Hio kitu kwa sheria kwa ukweli macommissioners iondolewe. Mtu yeyote ambaye amechaguliwa kwa ushirika na ameanguza ashtakiwe. Na mali yake pia ile amepora kwa hio ushirika ichukuliwe, irudishiwe hilo shirika sababu tuna watoto wansoma na wale pia wanataka kazi na kesho unaskia serikali inasema serikali haina pesa, serikali haina kazi na hio ndio kitu ambacho inazidi kupunguza maidara ya kazi.

Pili nafikiri mnanielewa. Pili kuna watu mtu mmoja amezungumza kitu kama hicho tunawachagua wanaitwa maMPS. Hawa maMPs wanaandikwa na wananchi hawa ambao wako hapa, wao si matajiri na ni ajabu wameandikwa na wananchi na kwenda kule kupigania wananchi, wanakwenda kupandisha mshahara yao. Kitu ambacho kwa Kenya nafikiri upande wa MPs wanapata mshahara mkubwa sana kushida wengine hata hawa majilani yetu. Na huku tunalia Kenya imefilisika, Kenya hakuna pesa, Kenya hakuna nini na unakuta MP anakura mshahara ambao sehemu ametokea hata usulu ambaye anatoka pale hailingani

na yule mshahara anatumia. MP akitaka kuongezwa mshahara arudi kwa hawa ambao walimuandika wakubaliane waongeshe mshahara kule Bungeni au si hivyo. Si mtu apate mshahara shilingi 40 na wananchi wamemuandika yeye ni shilingi 5,000 na ndio matajiri.

Ya mwisho – Uchaguzi. Ikifika uchaguzi iwe na watu wamesimama pale kabisa sio wale wanachaguliwa na Rais halafu wengine wanatumwa wanambiwa Onyango ukienda pale fulani akipita wewe usirudi hapa. Hio kitu inafanyika. Kwa hivyo uchaguzi usiwekwe ati President, sio President huyu, President yeyote tupewe nafasi ya kuchagua au ya kusimamia mambo ya uchaguzi. Asanteni wenzangu.

**Com. Abubakar:** Asante sana mzee wangu. Julius Mwakina. Jiandikishe pale mzee wangu. Julius Mwakina, ame-present. Yussuf, Leah Jumma. Yuko.

**Leah Jumma:** Nashukuru sana kwa nafasi hii Commissioner wa Tume hii nashukuru sana kwa nafasi hii na wananchi pia nawasalimia. Mimi maoni yangu ni kwamba nimeshukuru sana kwa sababu serikali imetutabua kuweza kujitetea sisi wenyewe na mimi ni Mkristo na wakati ambapo biblia imeandikwa haichagui yaani ni nani ameiandika. Basi twasoma hivyo, kwa hivyo tukitetea shida zetu twangalie zile shida tuko nazo katika eneo zetu, tuweze kujitetea sisi wenyewe. Shida moja inaniudhi katika moyo wangu ni shida ya ardhi. Ardhi tuko nazo lakini hatujui tutumie namna gani na tuna watoto ambao ni machokora ama wengine ambao wamezaliwa nje ya ndoa. Labda mzee yuko na msichana wake amezalia pale na mvua itanyesha lakini hakuna mahali pa kuweza kulima. Kwa hivyo tunataka hii ardhi irudishwe kwa wananchi wenyewe mahali ambapo hakuna watu ambapo wananchi wa Pwani. Watoto kama wale wapatiwe mahali wakaweze kulima ili wasiendelee kuuza vitu ama wasiendelee kuomba omba, ama hizi pombe za kienyeji sikae katika mtaa maanake zimeharibu watoto na hata ugonjwa wa ukimwi unaendelea kupanuka maanake hawana kazi wanatafuta njia ya kupata pesa ili wajisaidie maishani. Kwa hivyo naomba team hii ikaweza kuangalia jambo kama hili naomba. Hivi sasa hata mashule imejengwa saa ingine na harambee na unakuta shule zile watu wanastahidi wale watu wanajitahidi ni wale wadogo sana ama saa zingine halls zingine zimejengwa kuweza kusaidia wananchi ati unakuta zile hall zinajisaidia na watu fulani. Kwa hivyo mambo kama yale yaweze kuangaliwa ili mambo kama haya yarudi kwa wananchi ambao walikuwa katika mambo yale na pesa hizo ziweze kusaidia watu wenyewe.

Jambo lingine kama mahospitalini, iwe na kamati ambapo ni ya pale pale, ambapo wananchi wa pale pale, waweze kuangalia zile pesa zinaingia na inaweza kujulikana ni ngapi. Na hata magari kama imeingia tujue magari ambaye inaingia inalipwa ni watu wangapi, ni pesa ngapi tunakopa katika nchi yetu. Na katika wanyama tujue ushuru wetu tunapata, ni hizo hizo zinasaidia katika mahali pale tuweze kusaidikia katika kupitia kwa wanyama, kupitia kwa mashule yetu, labda tujengee katika harambee na mambo mengine yale.

Na jambo lingine pia, ningetaka kuzungumzia, mtanisamehea, kuna makanisa ya imekuwa mengi, na makanisa yale yamekuwa kama biashara. Kuna watu wengine wanafanya makanisa haya kuwa biashara. Na makanisa yale haihudumii watu kulingana na

vile Mungu ameandalia. Kuna wengine ambao ni nabii, kuna wengine ni mitume, lakini unakuta nafasi ile yule mtume, ama yule nabii haiwezi kuitumia. Anafinyiliwa na kisha anapata kuajibika. Kwa hivyo ningeomba serikali yetu ipate kuangalia ama ikaangalie wale manabii wanaomba kwa kupitia kwa Roho Mtakatifu ili kuomba kwa roho na kweli manake kuna watu wengine wanaomba na ili miujiza unatokea. Kama vile Yesu Kristo alikuwa akienda akifanya pia dakika iko nao wanaombea ukimwi, ukimwi unaisha lakini unakuta watu wengine wanasema hawa ni manabii lakini hatuoni miujiza kama hayo. Kwa hivyo wafikiriwe watu kama wale wawe wakilipwa pesa na pia kuchunguzwa kama kweli kazi zao au kipawa chao kinafanya kazi maanake wanaona ukiwa unaisha wanaomba miujiza inatokea. Lakini kwa sababu ya ule ummaskini, kwa sababu Mungu anamtumma anaenda mbali anawacha watoto wake na njaa akili zake zinafikiria watoto nyumma. Haendi kufanya ile kazi Mungu amemujalia nayo. Kwa hivyo naomba Tume hii ikapate kuangalia.

Jambo lingine naomba pia Wataita wenzangu maanake hapa tuko Taita, tunapozungumza jambo tusitaje makabila bali tutaje yale matatizo tuko. Kwa sababu tukitaja ukabila tunasema tunagawanya gawanya kwa hivyo naomba kwa hurumma zenu tuzungumze shida zile tukonaye ile shida ya chini sana. Sasa tuangalie na tuwapatie matatizo yetu. Kwa hivyo tunaomba ardhi yetu turudishiwe sisi wenyewe tukaweza kuigawanya, tuweze kuangalia kupiga darubini, ni nani atapata na ni nani asiye pata. Kwa hivyo kila mtu ajue yeye ni mkaaji wa pale ana uhuru wake wakufanya kile ambalo kiko. Asanteeni sana, jina langu naitwa Leah Ndulo Jumma Box yangu ni 48.

**Com. Abubakar:** Asante sana, jiandikishe pale. Joyce Kaleb. Otieno ambaye amejiandikisha kama Otieno peke yake. Said Mohammed.

**Mohammed:** Macommissioner na wakazi pamoja na ndugu kutoka Ukunda tunahudhulia hapa zote, ili sina mengi sana lakini nitazungumza kwa lugha ya Kiingeresa.

Since the Constitution

**Com. Abubakar:** Ndugu yangu fanya namna hii, usitusomee just highlight the content because we will read it at our own time. Just highlight.

**Said Mohammed:** Since the Constitution is the supreme lawof state and the Constitution came about through acquisation, agreement and compromise of all people therefore 1. There shall be no person who should be above this law. 2. All leaders including the President should recognize the fact that they are selected and are working for the people therefore they should respect the power of these people. 3. All rules shall be for all people including the administrators. This means all people shall be below the law. 4. The system of governance should be based on the peoples consent which the citizens shall seriously take part and share the work of governing the state. And 5. The Constitution of Kenya should totally respect the democratic principles in which to bring up freedom. Therefore it must effectively provide the citizens with the power and enjoy from the government a

total freedom, socially, economically and politically. This means that citizens should have the ability to make lawful choices and to do lawful without being worried or stopped others. b) there should be fair opportunities and treatment of all citizens towards government resources and responsibility. c) There should be total justice, fairness and equality in all areas. No form of discrimation among people in the country eg. all registered political parties should be equal before the supreme law. This way a coalition government to be formed and every citizen to presented in the government. e) For the respect of freedom of worship one should not be forced to do something in which faith does not allow him or her to do unless otherwise.

Hapa nimetoa mfano; kwa mashule kuna dini zingine mfano, kama dini ya Kiislam watoto wa kike wanataka kuvaa jinzi sheria za Kiislam inahusika halafu wanakatazwa. Therefore that one should not be that way. Halafu subjects pia, if I am not willing to take any subject tafadhali hio isiwe ni lazima, because I will be going against my faith.

As to respect the freedom of worship also they should be total peace in worhiping places so as to avoid interference and disturbances. Hii ni mfano wa manyumba ya starehe yawe mbali kabisa na sehemu za kufanyia ibada.

Number 2 – Due to different types of worship in different faiths, of is possible the worshiping places should be at least far from other faiths, at least at an estimated circumfrence yaani kwa sababu ibada zinaenda tofauti tofauti, huenda pale pengine Wakristo wakiwa wanapiga ngoma pale vile inafanya inafanya.. kwa hivyo Katiba iwe inaeleza kwamba at least kuwe na circumfrence hizi ibada mbili ziwe mbali mbali.

There should be a difference between a Kadhi and, I am now talking about Kadhi. Kuwe na tofauti baina ya Kadhi na Muslim because, this means Kadhi should only deal with cases related to Islamic faith. I am not to serve an Islamic leader. That one it belongs to Muslims. Kadhi shall remain as other judges in court.

For a person to be a Kadhi he must I say a must kwa sababu katika sheria ya Kislam mwanamke hawezi kuwa Kadhi. He must be a Muslim, aged at lest 5 years and above, a well educated person from okne of the recognized Islamic universities in the world. Must have good personality. Okey. In Kadhi's court there should a well defined Islamic book which will help to guide the Kadhi in dealing with cases kwa sababu hii hakuna saa hii. Kwa hivyo katika Katiba tunapendelea hiyo iweko ambayo a book should be compiled and written Islamic scholars through the law as in holy Koran and Hadith his prophet. In order to avoid interference an inconvenience in the Kadhis court should at least in three levels.

First class, at district level, huyo atakuwa Kadhi and then we should also have senior Kadhi who will serve High Court, halafu we have the Chief Kadhi ambaye the Chief Kadhi score will listen to cases which has been heard by the High Court and where the parties justifies into the judgement. Yaani ni kama Court of Appeal. The Chief Kadhi should be the last person to decide the fate of any Islamic faith cases through the right laws. This means Muslims cases should not be taken to other courts apart from those dealing with Islamic faith unless otherwise.

There should be an Islamic leader, whose word will deal with all other Islamic matters. For a person to be a monk he shall have the same qualifications of those laid by Chief Kadhi. In the Court of the Kadhi, there shall be a woman representative who will deal and forward matters concerning Muslim women. She has to be well educated and also have good personality towards the faith.

Nikimalizia nitaongea kuhusu powers – the state powers – the principle organs of the government that is the legislature, executive and the Judicially should seriously have equal powers in terms of their work. There shall be no part of government arm in which shall have too much powers or goes beyond its function. Two the Judicially arm of the government should seriously enjoy the security of tenure so as to work efficiently and create a justice atmosphere within the government. In order for this system to work well, the President should not have powers to appoint the Chief Justice. The Chief Justice shall be appointed by the Parliament. The powers of the President to exercise the right of mercy should be fairly done and not either on favouring ground.

The Attorney General should not have powers to end a criminal case before judgement is delivered. This work shall be done by the Chief Justice and the reason for doing so to be known by the people. The President should not have powers to create and do away with jobs and departments. Likewise appointing persons to such offices and to end such office without the consent of the Parliament. The President should not have powers in controlling the work of the house, eg suspending and dissolving Parliament. This responsibility should be done by the house speaker through agreement from the house members.

And the last, powers of all administrators shall be of a certain limit in which shall not interfer the freedom of work in other offices nor of other citizens. The use of powers should always be regulated.

**Com. Abubakar:** Thank you so much. Can you hand in your memo and sign. Can we have Peter Mwandawiro.

**Peter Mwandawiro:** Bwana Commissioner nafikiria nimeandika kwa hivyo nitaenda mbio mbio. Huu si chama cha kisiasa pendekezo langu hapa ilikuwa ni kwamba at least angalau kuwe na vyama vitano vya kisiasa na pasiwe na chama chochote ambacho kitaghalamiwa na fedha za umma. Kwa mfumo wa serikali pendekezo langu ni kwamba tuwe na mfumo wa majimbo. Mamlaka ya Rais yapunguzwe.

Kwa upande wa wabunge ni kwamba, wabunge wawe na mamlaka ya kuchagua Mkuu wa Sheria na viongozi wa mashirika ya serikali, na mkuu wa police. Hii isiwachiwe mtu mmoja manake inamfanya aliyechaguliwa kuhudumia mtu mmoja. Na angalau mbunge awe na kiwango kingine zaidi, manake hii saa ingine. Unapata wengine hawaelewi mjadala unaendelea vipi. Kwa hivyo pendekezo langu ni kwamba angalau hata akina na shahada ya diploma, ya degree kuendelea hivyo ubora tuelewane katika Bunge.

Serikali ya mitaa pendekezo langu ni kwamba tuwe na uwezo wa kuchagua mamayor wetu wenyewe hapa. Ama wenye viti wa mabarasa na wawe wakihudhumu kwa kipindi cha miaka miwili vile vile manake mamayor akiwa ameleta matatizo kidogo tunakuwa na nafasi ya kumuodoa.

Kwa upande wa wabunge, nilikuwa nasema, wa Rais sorry, ahudumu mda wa miaka 10 kwa vipindi viwili vya miaka mitano, mitano ikiwezekana isizidi hapo.

Kwa raslimali, nilikuwa napendekeza hivi. Huu umaskini saa ingine unaletwa kwa vile serikali yenyewe haizaidii wananchi kutambua zile raslimali ndogo na zitumie ni kikamilifu. Kwa hivyo panapo uwezekano uzaidiwe tutabue raslimali kama mfano hizi buga za wanyama wa porini. Tujue hivi kwamba ni zetu na sitahifadhiwa vipi ili waweze kuchangia kikamilifu kwa manufaa yao. Na kama maji ya chemi chemi, vitu kama hizo zisaidie maskini. Kuna eneo la ardhi hapa, lakini tunaweza kuondoa ummaskini. Serikali itusaidie kutumia zile raslimali zetu kikamilivu.

Pili yale mapato yatakuwa yamepatikana kutoka kwa raslimali angalau sehemu kubwa ibaki katika eneo ile ili kudumiza zile raslimali ambazo zilizoko na kutia mutisa wale ambao wanahudumia pale.

Haki za kimsingi – Hapa nilikuwa nafikiria sana elimu ikiwezekana pendekezo langu elimu iwe ya bure kuanzia shule ya msingi mpaka ya shule ya upili angalau kidato cha nne. Afya, hii iweze kuwa ya bure angalau hata yule ambae hana namna aweze kupata matibabu manake ni haki ya kila mtu na nchi kama itatoshwa basi itoshwe kulingana na hali ya kiuchumi kwa wakati huo.

Haki za ardhi na mali – Pendekezo langu ni kuhusu kwamba mali ni tuna haki ya kumiliki pale lakini kuna watu wengine kwao, si vizuri lakini na mimi niwe ninajua mamlaka yale ya kuridhi pale kwangu kwamba mimi sipatiwi yale makaratasi ya kuridhi watu wengine wakamkia kwangu. Ikiwa kama nitashirikizwa ama kumkabidhi mtu mwingine, then iwekwe Katiba kwamba mpaka nihusishe watu wangu, awe wa kiume, awe wa kike. Na pana matatizo penye watoto wa kike siku hizi wengine hawaolewi. Wale ambao hawana makao wawe na haki ya angalau kuridhi sehemu ingawaje nilikuwa napendekeza wao wapewe sehemu kidogo wale wa kiume iwe kikubwa.

Na kwa uongozi wa matumizi ya mali ya asili, pendekezo langu ni kwamba kile tutakuwa tumechuna katika eneo letu, sehemu kubwa itumiwe hapa kwetu. Nafikiria ni hayo, asanteni.

**Com. Abubakar:** Cose Mwakio, J.M. Ngatia.

**J.M. Ngatia:** Mimi hapa niko na mapendekezo kutoka vikundi bili tofauti. Hapa niko na maoni ya akina mama na niko na maoni ya ofisi yangu ya NGO. Na yangu ni marefu sana sijui nitasoma ama nitafanya je.

**Com. Abubakar:** Just hight light. Jaribu ku-hightlight the most important.

**Ngatia:** Nitaguzia mengi haijaguzwa lakini kuna machache ambayo nitatilia mkazo. Imependekezwa kwamba hazwa na akina baba kwamba kulegezwe pombe ya kienyeji. Mimi nafikiri kama mama, kama mwanamke na kama mzazi nitapinga, na zipingi peke yangu, napinga kwa niamba ya akina mama, nikipinga nafikiria kwamba Kenya itaharibika baada ya kuwa ni baya itazidi kuwa ni baya zaidi. Nasitikika kwamba watoto hawatasoma itakuwa ni bangala na ni bangala kweli. Sisi tutasukulu serikali kwa sababu ili-burn kwa hivyo hiyo burn iendelee isiwe lifted.

Pili nitazungumzia juu ya kunajiziwa – Hii tabia imekuwa imezidi lakini kitu nitapendekeza ni kwamba wakati mtu amenajizi, siku hizi wanangizi hata wa kuume pia. Mtu akipatikana na kosa hilo awe dealt with accordingly na apelekwe kotini na ashtakiwe kulingana na zile damages zimesababika. Na ikiwa atahukumiwa kama kunyongwa, kama atahukumiwa kufungwa wala si kunyogwa si chini ya miaka 10.

Nitazungumzia juu ya watoto wa kina mama walemavu. Hawa ndio watu wamekatwa katika serikali na wamesahaulika kabisa ni kama hawako. Kwa hivyo ni jukumu la serikali kuhakikisha hawa watoto wa akina mama walemavu wameangaliwa wamepata basic needs kwanzia mwanzo mpaka mwisho free of charge.

Nitazungumzia pia afya ya akina mama. Kila siku twaambiwa ukijenga mama umejenga taifa. Sisi tunapendekeza kwamba kuna hii cost sharing, hatujakataa ni kwa sababu uchumi ni mbaya lakini mimi nazungumza kwa niaba ya akina mama. Kwa akina mama naomba access ya hospital ama health facility iwe free. Kumekuwa na ummaskini kwa upande wa akina mama na hapa nikiangalia nitazungumzia Voi kwa uchache. Akina mama ndio walezi wa jamii. Kwa hivyo mimi napendekeza serikali ipeane mikopo kwa akina mama na terms zake ziwe soft sana. Wapewe mda wa kutosha kulipa bila matatizo na kama kutakuwa na faida iwe ni faida ya chini sana ambayo yule mama wa chini kabisa anaweza ku-afford kulipa huo mkopo without matatizo. Hayo ndiyo machache nimepitia kwa upande wa akina mama.

Hapa nilikuwa na presentation ya Tsavo wardens na human relations to promotion ambazo nimetengeneza mimi kama councillor and my director. Nimesema hapa tumependekeza serikali, wakati Rais anaingia kuwa President awe na kiapo atakula. Nafikiri nitapitizia kwa kifupi sana. The President shall make the following formal declaration. I solemnly undertake to perform my duties according to the general interest of Kenya. In carrying out my duties as the head of state, neither to seek nor take instruction from foreign government or body. To refrain from any action in compatible to my duties I formally know that attention of the members of the family whether immediate or distant to respect this principle and not to seek influence from members of my government in their performance of the task. Hii ni kujikinga na kwamba kwa sababu mimi mtoto wa Rais, nachukua makokaa, nachukua kila kitu duty free. Kwa hivyo iwe ni mtoto wa Rais iwe ni nani ajue sheria ni msumeno hukata mbele na nyumma.

I further undertake respect both during and after my tenure of the office obligation arising there from and in particular a duty to behave with integrity. Hayo ni kiaoo cha Rais vile mimi nimependekeza. Tumependekeza kuwe na ministry 8 peke yake. Zimekuwa mingi, tunasema uchumi ni mbaya, ministries zimekuwa mingi, uchumi ni mbaya watu hawalipi, malipo yamekuwa ni matatizo, tumependekeza kuwe na ministries 8 peke yake. Iwe ministry ya agriculture, Consumer Affairs, Defense, Education, Workers Right Energy, Economic ana Finance, Environment and Public House, Foreign Affairs, Industry and Commerce, Regional Development, Travel and Communication Social ana Internal Affairs.

Tumependekeza vile vile, there should be one Supreme Court, and 11 High Courts. Tumechoka kila siku nikiwa referred to High Court. Kila province iwe na High Court yake. Vile vile inasemekana tutazikilizikiana the President is above the law, imerudiwa tena lakini sitaki kurudia he is above the law, haitawezekanahizi nguvu zipunguzwe na ikiwezekana zitolewe kabisa. Awe kama mwananchi mwingine akifanya makosa awe answerable, ajibu kotini na ile penalty mimi napewa kama councillor apewe yeye kama President. Zile nyingi napitia na-pick zile za muhimu.

Hapa tulitumwa na mapendekezo juu ya protection of humman rights. The same must govern the right of individuals and application to protect democratic institutions. It must not turn judges into legislature. When human rights are endangered no nation should be left to judge himself. First universal an individual freedom need to be defended at the E. African community level. The Constitution shall provide religious freedom, property rights, equality in commerce, the poor relief, the right to poor relief, the right to elementary education, freedom of press, freedom of association and freedom of assembly, the right to work, freedom of press and peace and all forms of rights improved.

Hapa pia kuna women environment nafikiri nishaseme sitarudia. Kuna political parties – There can be many political parties as possible. As a general rule political parties which are not represented in Parliament may only participate in a General Election if they can win a petition supported by voters who participated in the last general election. All Kenyan citizens including those Somali speaking are entitled to fundamental rights that are guaranteed in the Constitution. The Constitution must declare principle of non-discrimination regarding politics, religious, social and cultural rights. Nafikiri nitasoma kwa ufupi, nafikiri wakati nitaenda kusoma nitawachokesha lakini tunaomba mutuwakilishe.

**Com. Abubakar:** Asante sana, tutasoma. J.M. Ngatia, Nzome Ngala. Sabastian Salim.

**Sabastian Salim:** Bwana Commissioner na wananchi kwa ujumla, hamjambo? Mimi langu la kuanzia ningependa kuanzia na kutolewa hasa kwa maPC, maDC, utawala wa mkoa na utawala pia wa Wilaya. MaDC, maDO, machief hao wote ningeomba ni kama watolewe kabisa kwa sababu hawatusaidii kwa kazi yoyote. Mimi ningeomba hapo tungekuwa badala yake kuchukuliwe nafasi hio na macouncillors ambao wanaongoza miji yetu kama vile municipal, nataka kuwe na mabarasa kama haya. Lakini kama DC sioni kazi yake manake mambo ya kule nimalicence, nini, vitu kama hizo, na hizo zote ambazo zinatoka

kwa mabarasa yetu kwa sababu wale pia naona ni sera tu ile ambayo ilikuwa ni ya ukoloni.

Kitu kingine pia ni mambo ya resources ambayo imeongewa na hio pia ningependa kutia mkazo. Vitu vyote kama ni mambo ya hapa ambayo tuko nayo, kama ni buga ya wanyama, kama ni madini ambayo tuko nayo basi tunastahili pia watu wa hapa tuyafaidi. Ikiwezekana 75% na zaidi.

Kitu kingine cha tatu ni mambo ya majimbo – Majimbo tunaitaka. Kwa sababu bila majimbo naona hatutaendelea mzuri. Watu hawatakuwa na vile vipawa ama nguvu za kuweza kumiliki ardhi yao vile wanavyotaka.

Ugawanji wa mashamba pia – Hio ambayo imesemwa. Pia hapa tunastahili ugawaji wa mashamba urudishwe kwa wananchi, kwa sababu kuna wenzetu hapa hapa wako na mashamba zaidi ya ekari 100, tunaskia kwamba shamba lingine ni la sisal liko na ekali zaidi ya 5,000, na sijui kama hizo zitakuwa sinafanya nini. Kwa hivyo tunaomba zilegezewe wananchi na wagawane kwa sababu tayari 75% ya tarafa yetu imechukuliwa na buga za wanyama. Kwa hivyo hio ingine tumebaki ni kidogo, nayo pia hakuna hata cheti cha kumiliki hio ardhi.

Kitu kingine pia ni tax, ushuru – ushuru umekuwa juu zaidi. Tungeomba sana ushuru uangaliwe mambo yake, utelemzwe chini. Kitu kingine pia ambacho ni cha tano – Centralization of industry, power, water, vitu kama hivyo. Kwa kummanisha hapo, namaanisha kwamba tukiwa na industries, industries ziwe zimegawanywa, zigawanywe na zitawanywe kwa kila kama ni mkoa, huo mkoa fulani unakuwa na industries na ziwe katika town plan, ili tuweze kuendeleza miji yetu. Kwa mfano kama Mombasa, isiwe na Mombasa peke yake inakuwa na industries zote. Zigawanywe zingine zipelekwe Malindi, zingine zifunguliwe kama ni hapa Voi, at least tundeleze. Na hio pia inazuia uenezaji kama ni wa wizi, na nini, na mambo mengi ambayo watu hawaishi vizuli kama vile Nairobi.

Kitu kingine ni labour rights – Hizi pia wafanyi kazi tunaomba waangaliwe haki zao. Isiwe mfanyi kazi tu leo anaabiwa tumekufuta kazi. Leo leo anaenda zake na hakuna maswali mengi. Lazima hizo sheria ziangaliwe. Kutungwe sheria za kuangalia rights za wafanyi kazi. Vile vile wakati mfanyi kazi anapokwenda retire, asisubuliwe kwa miaka mitano ndio aje kupata pesa zake. Mwaka mmoja uwe mwisho, pamoja na insurance ile ambayo inatolewa sana sana kama pengine kumetokea ajali, ama nini. Hizo huwa zimesubua watu. Unakuta mtu anafujika mkono lakini pesa yake haipati bila kwenda vizuli akaenda akahongana pesa yake aipate. Kwa hivyo hiyo pia iangaliwe. Mambo kama hayo mwaka moja mwisho.

Kitu kingine pia wabunge wetu ambao tuko nao kama hawatatufanyia kazi ile ambayo tunataka basi kuwekwe kipengele fulani cha kuweza kuwatoa mamlakani kabla ya hio miaka mitano haijafika. Kama hatufanyii kazi within those five years, ama kabla kama amekuwa mlengevu ama amekuwa anaenda kule kwa ajili ya tumbo lake basi atolewe mara moja.

Kitu kingine pia ni habari ya freedom of worhip – Hii nitapata kuipinga kwa sababu freedom of worship ndio imetuletea mambo

mengi sana. Rais wakati aliidhinisha freedom of worship ndio kumetokea mambo ya devil worshiping halafu pia kumetokea makanisa mengi sana vile mtu mmoja alisema, kwa hivyo tungeomba sana makanisa yawe ni yale yamekuwa recognized na sana hata kwako kama nitasema tu hata upande wa kanisa ya wokofu. Wokofu tunajua ni wokofu mmoja. Basi tungeomba iwe na kanisa limoja la wokof. ,Isiwe makanisa mengi ya wokofu, kwa sababu hii lina sheria zake na sheria unaangalia hakuna. Kila mmoja anaclaim tu ameokoka, lakini hizo zote zimekuwa nyingi sana kwa sababu wameabiwa kuna freedom of worship. Mtu anaamua anapanda gari bus, anaanza kuhubiria watu ati ni freedom of worship kumbe ndani yake anafikiria biashara. Kwa hivyo tungeomba hizo zote zikuwe scrapped, zibakie zile zile zilikuwa kitambo, sijui mwaka gani, lakini zile zilikuwa kitambo, zile churches.

La mwisho ni hizi powers za President – Hizo hata mimi nachangia kabisa zikatwe kabisa, na katika ile hali ya zile arms za Executive, Judiciary, Legistlative naona zote zingekuwa independent. Kila mmoja kiviake, na wale wote wawe wakichaguliwa na Bunge. Sijui huyu anasema wacha nichague wangu, ama leo anafuta judge. Hio mambo basi itakuwa inaenda ovyo. Itakuwa hakuna kazi tutakuwa tumefanya. Asanteni kwa kunisikiliza.

**Com. Abubakar:** Asante sana mzee. Joseph Makio.

**Joseph Mwakio:** Asanteni macommissioner na wananchi kwa jumla. Mimi kwa upande wangu huko nataka kuingilia mambo ya tax kwanza. Sana tukiangalia hapa sana sana kwa kwetu Kenya boma, tax nyingi sana inachukuliwa lakini hatuoni ile manufaa yoyote hii hutufanyia kwa sababu tukiangalia mahospitali yetu ndiyo hayo. Wafanyi kazi wanadhulumiwa. Tukiangalia pia hizi barabara zetu, yaani kila kitu kinadhulimiwa. Sasa nilikuwa naona hata wale wanabiashara labda zile nini walikuwa wanatoa kidogo kidogo wasitoe kabisa. Kuna nini huwa wanatoa kwa kuuza wasitoe hata license huko naona hazina maana kwa sababu hazitufaidi. Na hata pia kwa tax ningependa pendekeza labda kuwe na kipengere kinazungumzia mambo ya tax, na kiangalie hizo tax zinatumika kwa manufaa gani. Kwa sababu zingine nyingi zinaingia kwa mfuko wa watu. Halafu kuzungumzia mabahari, labda niseme mambo hapa Voi, tukiangalia tujadilie tumechukua nafasi nyingi sana. Tukiingilia wengine hatuna mashamba kabisa, hatuna pahali pa kupata kuweza kutengeneza hata kibada. Hata huku naomba kama ingewezekana hio land ipunguzwe at least kuwe na mashamba yagawanyiwe wale wa eneo lile, na pia kwa hayo hayo mashamba wale ambao wamemiliki labda huko tunasema yachukuliwe zile title deed zitolewe zote halafu tugawanyiwe sawa sawa, equally kwa wale ambao labda wamechukua karibu ekari 50 na si za halali. Labda kukiwa kipengele kiwe, achunguzwe kwa koti na anyang' anywe hio nini, na alipe kwa sababu itakuwa alidhulumu na achiachiwe.

Na pia nikiongea juu ya mambo ya municiple – Tukiangalia municiple ya kwetu ni kama si municiple, lakini iko rank ya county council. Kwa sababu yale mambo ya municiple hayaonekani. Tukiangalia sewage hazina maana. Tukiangalia tena kuna zile pesa nyingi huwa wanapata kwa land na kwa kila kitu. Lakini hata hazitufaidi kama watu wa Voi hata huko naomba iangalie sana hata katika zile rank za municiple, wangalie zile pesa zikuwe zinafaidi watu wa pale. Asanteni.

**Com. Abubakar:** Mwachengu Wasaa.

**Wachofi Wasaa:** Mimi kwanza macommissioner karibuni wenzangu. Mimi nimetayarisha mapendekezo, lakini ningependa kueleza kwa ufupi. Naitwa Ngorio Matengu Wachao Wachofi. Ukweli ni furaha kubwa kwamba tunapata nafasi ya kuweza kutoa mapendekezo. Mimi hata kile kilinifanya nije kutoa mapendekezo ya Katiba ni ule ummaskini ulioko katika nchi yetu, ni ile hali ambayo watu wanaishi. Ukitoka mpakani Busia mpaka Lamu, kutoka Taveta mpaka Marsabit kwote katikati. Ukitazama ni ummaskini. Tena sio ummaskini wa kawaida, ni ummaskini ambao unaedelea kuongezeka. Ummaskini umekili, unaongezeka na unaendelea kutapakaa kila mahali. Wakenya wanaishi kama wakimbizi katika nchi yao, na mjadala ambao tumefanya na watu katika sehemu nyingi katika miezi michache iliyopita hapa katika Pwani tumeona wazi kabisa kwamba ummaskini huu umesababishwa na utawala usiofaa. Utawala ulioko, utawala amri, au dictator ukitaka. Utawala ambao tulirlidhi kutokana na ukoloni. Utawala ambao badala ya kuwa kiwezezi cha maendeleo ya mwananchi, unakuwa ni kipingamizi cha maedeleo ya wananchi. Ndio maana inakuwa lazima tutoe mapendekezo kwa sababu huu utawala mbaya ambao ndio unasambabisha hali baya ambayo watu wetu wanaishi dani yake, unaangaliwa na unahimiliwa na Katiba. Katiba baya, Katiba ambayo inaweka uhuru maskini uendelee kuwa pale.

Hii ndio maana ndio sababu tumekuja kutoa mapendekezo, ni kwa sababu ingawa 1963 tuliambiwa kwamba tumepata uhuru, nami nilikuwa kijana na mimi ni mmoja wa wale ambao tulienda kuwasha moto kule Nguria ati Pwani mzima waone kama ukoloni umeenda, ingawa tuliambiwa uhuru ulipatikana siku hio kwa kweli kama kuna uhuru ulipatikana siku hio basi ulikuwa ni uhuru wa nchi. Lakini uhuru wa wananchi bado hujafika. Nafikiri mnanielewa kwamba kuna tofauti ya uhuru wa nchi kwamba hii nchi ni huru, haizimamiwi na wengine ingawa tunajua, kwa njia zingine inasimamiwa, kwa sababu ukiwa maskini unaomba omba. Wale wenye kukupa ndio wanakutawala. Lakini hii ni tofauti na uhuru wa wananchi, yaani wananchi wenyewe kuweza kujitawala na kupanga mambo yao. Sasa huu uhuru hauko. Katiba ya 63 ilijaribu kidogo ikasema majimbo, na kujaribu kufungua kazi zingine ili wananchi waweze kushiriki utawala, lakini tunajua kwamba kipindi cha 63 hadi leo hata yale machache mageuzi ambayo yaliokuja sasa hayako tena, yamebadilishwa. Ndio maana, kuomba au kutoa mapendekezo ya Katiba ni kutoa mapendekezo ya mfumo mpya. Ni kutoa mapendekezo ya kutoa hali ilioko sasa na kuleta hali mpya. Nikuleta Katiba ambayo itawezeza utawala, utawala ambao ni wa kushirikisha wenyeji, ili wananchi waweze kutumia raslimali zilizoko na wazitumie ili kuondoa ummaskini. Waondoe ummaskini wao binafsi na waondoe ummaskini wa nchi.

Katika mapendekezo ambayo nimetoa, nimejaribu kueleza kwa nini ninakuja kutoa mapendekezo haya, na natoa mapendekezo haya sio kwa niamba yangu peke yangu peke yangu lakini pia kwa niamba ya wale wengi wasio na sauti, wanaogandamizwa na udictator ulioko sasa. Mambo haya tunatoa kwa sababu tuna imani, kwa sababu tunajua ni imani za Wakenya na imani ya kwanza ni kwamba nikuhusu umiliki wa uraslimali Wakenya wote wenye nia nzuri walio wengi wanaamini kwamba raslimali zilizoko tulipewa na Muumba ili tuweze kuzitumia kutoa mapato ambayo yatatuwezeza katika maisha kila siku.

Kuhusu jambo la vipi watu wahusiane, ni wajibu wa kila mtu kuhusiana na raslimali. Ni kweli tunaamini kila mwananchi ana

wajibu wa kufanya kazi, juu ya hizi raslimali ili kuweza kuongeza uwezo wetu na kuondoa ummaskini ambao unatusumbua. Kuhusu ugawaji wa raslimali na utajiri na mapato yaliopo. Mfumo wa utawala tulio nao sasa unapendelea wachache, wale walio wengi hawapati chochote. Na vile nilisema ni kwa sababu utawala tulio nao ni wa mpokeo wa mkoloni. Katika mfumo wa ukoloni utawala uliwekwa kwa sababu moja tu, kuhakikisha kwamba raslimali zetu zinatumika kufaidi wageni wachache na sisi walio wengi tuendelee kuwa maskini. Baada ya uhuru, hari ni ile ile sasa, kwamba utawala ulioko ni kuwezeza wachache waendelee kufaidi raslimali ikiwezeza wachache walio na mamlaka waendelee kujipatia raslimali, ni kuwezeza wachache wenye uwezo waendelee kufaidi mapato, na wale walio wengi wasipate. Kumbe kwa kufanya hivyo tunajenga ummaskini wa nchi, tunawacha wakenya wanaishi kama watumwa.

**Com. Abubakar:** Mwana Mwachofi, unajua ulikuwa na dakika tano nasasa umemaliza nne kwa point moja tu. Tafadhali ujaribu kwenda kwa point zingine.

**Mwachofi:** Okey. Nashukuru niku-highlight lakini tuseme katika ama pendekezo tumeeleza mwenye Katiba ni nani, na tunasema Katiba ni ya Wakenya. Kwa hivyo pale mwanzo iseme sisi Wakenya, Katiba hii ni yetu na tunaitunza na tutoe sababu zake. Kwanza ni imani, zingine kama zile nilikuwa nataja. Pia katika Katiba ambayo napendekeza kuna jambo la haki. Tunasema kila binadamu ana haki kadhaa. Moja ni kupata na kusherehekea haki zote za msingi, kuwa na uhai: tuweze kupata chakula, malazi, mavazi, hewa na maji safi. Kupata na kufurahia haki zote za kujamii, kufaidi kutokana na mazao yake, kudai na kupata haki, na thamani halisi ya jambo na juhudi zake. Pia katika Katiba tunapendekeza ni kwamba kuna uhuru, vipengele kadhau vya uhuru ambao kila mtu anapaswa kuwa nao. Kwa sababu tunazijua sitaweza kuzitaja. Tunasema pia kila mwananchi anawajibu wa kufanya kazi kwa bidii kwa mfano kwa kuhesimu haki, kwa kudumiza usawa wa wote, kwa kutenda haki kulipa watu waliofanyia kazi haki yao kamili. Kila mtu ana haki ya kuzaa na kulea watoto na mapato, bila kuingiliwa kila upande mpaka bedroom unaambiwa fanya family planning kwa mfano. Uhuru wa kutetea haki ushiriki katika ukataji kauli, kukozoa utawala. Mambo ambayo wengine tumejaribu kutoa utawala makosa na tumekiona na mpaka sasa. Uhuru wa kulinda Katiba ambayo tunaitunza, uhuru wa kukataa kabisa hongo na kufichua na kuangamiza ufisadi.

Pia katika Katiba tunapendekeza tuna jambo mamlaka ya nchi na tunasema mamlaka ni ya wananchi. Kuna maelezo zaidi kwamba wale ambao watakuwa mamlakani ni watumizi, ni chombo cha wananchi. Tunataja pia vile jamhuri itaundwa, tuwe na jamhuri ya muungano wa watu wa Kenya. Aina ya utawala watu wengi wametaja na hapo tuna mapendekezo marefu. Tunapendekeza utawala katika ngazi za sita. Katiba itabue kwamba kuna utawala katika familia, kwa hivyo hawezi kuingiliwa. Katiba utabue kwamba kuna utawala katika kijiji, vijiji vyote. Katiba itabue kuna utawala katika location. Tunamaanisha utawala ambao unachaguliwa na watu wenyewe, utawala ambao ni serikali, una mahakama, na una Bunge. Kijijini kwa mfano Bunge la kujiji ni wana kijiji wote katika sasa, Bunge la sasa ni wakilishi wawili mme na mke katika kila kijiji. Ukienda kwenye wilaya badala ya councillor mmoja, kila council inatoa watu wawili, mme na mke, waende kwenye ile serikali ya wilaya na mambo kama hayo.

Kwa hivyo hizi ngazi sita ambazo tumependekeza ni familia, kijiji, kata, wilaya, mkoa na taifa. Katika mambo haya tunasema katika kila kiwango tutakuwa na Bunge, kwa hivyo sizungumzi juu ya Bunge moja ya Kenya tunazungumza juu Bunge la taifa, mambunge ya mkoa na Bunge katika wilaya, maBunge vijijini. Tutakuwa na wabunge vijijini, mwana kujiji ni mbunge. Mambo ya kuwa mtu anaogopewa ati yeye ni Rais, kuwe na Rais katika kila kiwango, Rais wa nchi, Rais wa mkoa, Rais wa wilaya, Rais wa Kata, ndivyo hii tendo liondoke. Unajua mwaka siku zile baada ya uhuru, wakati Kenya imepata jamhuri mwaka 64, hata vocaburary imegeuzwa tukaambiwa neno President katika Kenya, dictionary ya Kenya imegeuka neno President ni mtu mmoja anaitwa hivyo. Kube siku zile tukisoma shule mimi nilikuwa President wa debating society, wengine walikuwa President wa farmers club. Kwani President ni nini? Si ni Rais tu, sasa tukiondoa kwenye mmoja tuweke kila mahali kuna Rais, hio tabalaa itakwisha. Na hivyo napendekeza tena katika utawala kila ngazi, ziwe na tofauti ya mkuu wa ile jumuia.

**Com. Abubakar:** Sasa summarize. Saa yako imeisha. Take the most important points.

**Mwachofi:** Nimechukua mda mrefu kueleza kwa sababu nikiwa utawala na ninaona ndio hasa Katiba lakini kuna uchaguzi wa viongozi, tunaeleza vile uchaguzi utafanywa. Tumeeleza juu ya kuteuliwa kwa watumizi wa umma, vile inapaswa ufanywe. Kila wakati kuwe na kile kiwango. Tumezungumza juu ya mfuko wa umma, hii serikali zinazosema ati sisi hatutapata pesa, tumeeleza, kwa kila ngazi. Tumejaribu kueleza juu ya usalama wa nchi na tunasema kuwe na jeshi la wananchi, yaani jeshi ya wanachi wa jamhuri ya muungano ya Wakenya. Jambo la usalama wa ndani, tumependekeza kwamba ni aibu na ni makosa kuendelea kuwa na kikozi cha police cha nchi nzima. Nduniani kote kwenye democrasia, vikozi vya police vinakuwa katika district. Kwa hivyo tunapendekeza kwamba badala ya kuwa na Kenya Police, kila wilaya wawe na kikozi chao cha police ambacho kinakuwa accountable kwa wenyeji. Kwa hivyo tukiona huyo hafai tunamtoa. Pia tuna kipengele tunazungumza juu ya raslimali za nchi, kueleza ni za nani, zitumiwe vipi? Mambo ya ardhi tumetaja lakini labda jambo moja naomba mnisamehe ingawa wakati umekwisha, nitaje juu ya ardhi. Ni kwamba ule wizi, upolaji wa ardhi na unyakuzi ambao umefanyika enzi ya ukoloni ya wazungu naule ambao umefanyika, umefanyika chini ya ukoloni wa Kenyatta na Moi. Hiyo ardhi yote zilinyakuliwa irudishwe kwa wenyewe. Kuna maelezo zaidi lakini wakati vile unasema uko kuna pia kipengele cha haki za wanyonge. Tumependekeza njia fulani ya kupendelea wale waliolemewa kama vile wanawake, makabila madogo, watoto na walemavu, kuwe na provision katika Katiba ya kusema hawa watawezezwa vipi kuwa sawa na wale wengine na ndio maana kwa mfano katika yale maBunge tumesema mme na mke kutoka kila kiwango waende wakae pale.

Ya mwisho kabisa tumezungumza juu ya uhusiano na majilani, na umoja wa Africa. Tunasema muungano wa jamhuri ya Wanakenya itajitabua kama shehemu hai ya jamhuri ya mguungano wa Africa mashariki. Kwamba wakati wowote tunapofikiria juu ya umoja wa Waafrika wote, basi jukumu la kukata kauli, kuamua kama haya mambo yatafanyika vipi, irudishwe kwa mwananchi, na sio kwa viongozi wachache. Poleni kwa kuchukua mda mrefu.

**Com. Abubakar:** Asante sana mzee. Oginga Ladin, ametoka. Mwambuli Swalleh.

**Mwambuli Swalleh:** Hamjambo wana Katiba. Yangu mimi ni kidogo tu, nimesikia watu wameongea Moi si mtu mzuri. Kwa kusema ukweli mimi maoni yangu ni kwamba powers zote zake zikatwe kabisa. Kwa kusema ukweli kitu kitakikana ni one man one job at least nasema hivi tuwe na kazi kidogo sio yeye kila mahali, yeye akuwa ni conquer kwa hivyo hiyo kitu hatutaki.

Halafu jambo lingine ni kuhusu mambo ya ardhi. Ardhi inatakikana at least wenyeji wawe wanashiriki mambo yao, kuwe na kamati ya wazee wa pale pale ndio hao wanashiriki ile kiti. Manaake Moi anaimba kuwa kamati ni yako lakini unakuta imebadilishwa siku ingine, watu wengine ndio wanaingia na matitle deeds zao. Kwa hivyo hio kitu inatakikana iangaliwe sana.

Halafu jambo lingine ni kulingana na mambo ya uchaguzi wa machief, mamayor, maPC kitu kama hicho. Hio kitu inatakikana Moi asishughulikie kabisa iwe inachaguliwa na watu wengine. Naona yangu ni hayo tu.

**Com. Abubakar:** Asante sana. Joseph M. Mbela.

**Joseph Mbela:** Wanakamati ya Katiba na wananchi, hamjambo? Mimi nimekuja kutoa maoni yangu kibinafsi na sina mambo mengi sana, lakini nilikuwa nasema kwamba Katiba ambayo itaundwa sasa iwe na utangulizi. Na utangulizi mwenyewe uwe unalinda wananchi.

Halafu jambo langu la pili nilikuwa naomba kwamba serikali ambayo itaundwa iwe serikali ya majimbo. Katika Kenya kuwe na majimbo manane, na katika kila jimbo kuwe na governor mmoja na huyo governor asiwe anachaguliwa na kiongozi wa nchi. Awe anachaguliwa na Bunge.

Halafu kuna jambo lingine juu ya mamlaka ya Rais. Mamlaka ya Rais nikuwa naomba kwamba yaondolewe awe kama mwananchi wa kawaida anaweza kama anafanya kosa ashtakiwe na awe kama ni kuhukumiwa ahukumiwe kama mwananchi wa kawaida. Jambo lingine ni kwamba wakati serikali imeundwa ya majimbo kama ni raslimali za jimbo lile 75% ibaki katika jimbo lile na 25% iende katika ofisi ya Rais ambayo inaweza kufanya hayo mambo mengine.

Jambo lingine ni kwamba, ile ardhi ilikuwa imechukuliwa na watu wengine katika njia isio ya halali. Unaweza kuta mtu mmoja ako na ekari kama 10 na zaidi na mwingine hana ardhi, ako na pengine robo ekari. Hiyo ekari irudishiwe kwa wananchi halafu wananchi wagawanywe ardhi wao wenyewe, ili kwamba kuwe na usawa kusiwe na mtu mwingine anaonewa hana ardhi na ako katika nchi yake.

Jambo lingine nilikuwa nataka kutoa pendekezo ni kwamba katika nchi kuondolewe jambo la kusema kwamba huyu ni squatter. Kwa sababu huwezi kuwa squatter katika nchi yako wewe mwenyewe. Mtu squatter ni yule anakuja ametoka nchi nyingine anakuja kukaa kwa mda, lakini mwananchi mwenyewe asije akaitwa squatter wakati wowote. Hilo jambo liondolewe. Halafu katika hali, pengine kuna zile tax ama cees zinatolewa, ziwe zinalindwa vizuri kwa sababu mali wakati mwingine pesa

zinachukuliwa nyingi katika tax, lakini twaona kwamba zinaingia katika mifuko ya watu. Haziingii katika serikali. Hio nayo iangaliwe sana kama kuna hali ya ufisadi inapatikana katika hali hio, basi hao wachukuliwe na washtakiwe katika mahakama.

Halafu Rais asiwe na nguvu ya kumchagua Mkuu wa Sheria. Kwa sababu kama Rais anachagua Mkuu wa Sheria inaonekana kwamba kama mwananchi wa kawaida amefanya makosa halafu aende pale kotini, hata akisimama aseme hakufanya kosa, kwa sababu yuko pale judge, ametokana na uwezo wa Mkuu wa Sheria, basi yule mwananchi ataonewa na atafungwa. Kwa hivyo Mkuu wa Sheria asichaguliwe na Rais, achaguliwe na Bunge. Yangu ni hayo machache sitaki kuendelea sana, Mungu awabariki.

**Com. Abubakar:** Asate sana. Mathias Mwabingu.

**Mwabingu:** Bwana Chairman na macommissioners na wananchi wenzangu, mimi niko na machache tu. Mimi kulinganisha na ugeuzi wa Katiba, ninaongea kwanza juu ya mila zetu sisi Wataita hapa. Sisi tumegandamizwa kwa sababu hata hatuwezi fanya sherehe yoyote. Tukitaka kuyahiri watoto wetu tunatengeneza ile pombe ya kienyeji kidogo halafu tunatelemsha na nyama kidogo, halafu sasa, tunakuja tunashikwa sasa na ni mila zetu sisi kufanya namna hio. Hatutaki mambo hayo sisi. Tunataka tukuwe huru kabisa na tusiwe tunasubuliwa Bwana.

Kitu kingine kinahusu hospitali – Hospitali imekuwa kwamba mtu anakuwa mgojwa anakufia nyumbani, na hali sisi kodi zetu sisi ndio tunazotoa na tukifika hospitali tunaenda tunalipizwa madawa. Hii cost-sharing ya huko hospitali iondolewe. Waona Bwana, iondolewe kabisa, andika hio,

Kitu kingine ni juu ya elimu – Watoto wetu sasa wako nje. Hii mvumo wa 8-4-4 umeharibu kila kitu sasa. Unaona sasa imekuwa sasa watoto hawasomi, watoto wengi. Sisi tunataka hii mpango wa elimu sisi wenyewe tunaviotoa kodi kama zamani, ile kodi yetu tunaitoa hii, tunataka elimu ikuwe bure kutoka nursery mpaka chuo kikuu. Unasikia Bwana, maanake ile kodi yetu tunayotoa ndio itaghalamia hiyo.

Kitu kingine tena nasema, ni kuhusiana na mandaraka ya Rais – Rais amepatiwa madaraka makubwa sana kiasi kwamba hata mwananchi hapumui. Sisi tunataka kwamba Rais kwanza apunguziwe yale madaraka yake. Sisi tunataka kama ni administration, sisi mambo ya DC, DO hatutaki, na machief. Sisi tunataka kama ni mayor ama chairman wa county council apewe madaraka ya DC, halafu councillor apewe mandaraka ya DO, manaake yeye amechaguliwa na wananchi. DO hachaguliwi na mtu, anatolewa huko analetwa hapa hatumjui, hajui mambo ya Wataita hapa. Kitu namna hiyo hatutaki. Nangea juu ya policy kabisa. Kama ni mambo ya DC sisi tuende kwa mayor, mwenyewe tulimchagua na anajua unyonge wetu na shida zetu.

Kitu kingine kinahusiana na upande wa mabenki – Mabenki yameweka sheria kwamba hata mwananchi hawezi pata mkopo

watu wadogo kama sisi, yaani imewekewa watu wakubwa ndio wanapewa maloans makubwa kubwa kutoka na mabenki, halafu mwananchi mdogo hawezi hata akafanya chochote. Nataka mfanye hivi, unaona hapa, hii National Park hapa nchi yetu hii, unaona Bwana. Wanyama hawezi kuzidi binadamu. Sisi tunataka tusukume hii National Park kilometer kama 20, unaona na hiyo igawanyiwe wananchi halafu tupatiwe title deed ambazo tunaweza kwenda nazo kwa benki na tukapata mkopo na sisi tujaribu kuinuka kidogo. Andika hio.

Kitu kingine ni kuhusiana na uajibika: wa wabunge na macouncillors. Sisi wanatundanganya hapa wakati wa campaign, ati watatufanyia hii, watatufanyia ile, wakishaa ingia kule, wanaweka end. Hio maneno hatutaki. Tutafanya hivi. Wakati tunamchagua, ni lazima andike contract na wananchi katika mwaka wa kwanza atafanya abc. Katika mwaka wa pili namna hio, namna hio mpaka miaka mitano. Ikifikia miaka miwili hajafanya vile ambavyo alikuwa anasema sisi wananchi wenyewe tupatiwe sheria ya kumtoa kwa vote of no confidence. Wasikia bwana, andika hio.

Kitu kingine kinahusiana na majudge – Judiciary. Judiciary haiko huru. Sisi wananchi tunahangaishwa sana. Tunasukumma sukumwa na kama huna pesa ya kuhongana, wewe unasukumwa tu kila wakati. Sasa hii madaraka ya kwamba judge achaguliwe na Rais hatutaki. Sisi judge tunataka achaguliwe na Bunge bwana, maanake mbunge ndiye tutamtumma na atachagua judge wale ambao tunawataka. Na pia tena kuhusiana na kustaafu kwake, asifanye kazi mpaka miaka 74 vile ilivyo kwa sheria. Huyu mtu atakuwa akili zake zimelala. Afanye kazi, astaafu katika ule mda wa kawaida 55 ama 50.

Kitu kingine ni kuhusiana na, nilikuwa nimeandika point lakini nimesahau rafiki yangu.

**Com. Abubakar:** Makofi kidogo kwa huyu jamaa. Wananchi watukufu huyu ndiye alikuwa mtu aliyekuwa akitaka kutoa maoni ya mwisho kwenye list niliyopewa. Tungependa kuwashukuru kwa dhati yetu kubwa kwamba mmejitokesha kwa wingi kutoa maoni yenu ili kunjenga Katiba mpya kwa nchi yetu tukufu. Ningetaka kuwakubusha tu kwamba kesho tutakuwa na kikao cha mwisho cha kukusanya maoni katika sehemu ya uakilishaji wa Bungeni wa Voi, Tausa ACK church, na tutanza kama tulivyoanza leo asubuhi saa mbili asubuhi mpaka tutakapomaliza saa kumi na mbili, au ikiwa saa kumi na mbili imefika bado wananchi wako, tutaendelea mpaka tutakapomaliza. Kwa hivyo ikiwa kuna watu ambao hawakufika leo na wako katika sehemu hii ya wakilishaji Bungeni, mnaweza kuwambia waje huko Tausa ACK church hapo kesho. Halafu Alhamisi na Ijummaa, Alhamisi tutakuwa huku Mwatate kwa Kinyungu ACK, halafu Ijummaa tutakuwa Mwatate, Kenyatta High School. Pia tungetaka kuwashukuru sana mwenyekiti wa kamati, mwalimu wangu, pamoja na wanakamati wake na watu wote waliofanya sisi tukafanya kazi yetu kwa urahisi.

Jambo la mwisho ningependa kumuomba katibu aje atufungie mkutano kwa kawaida tunavyofanya sisi kwa kumuomba mmoja wetu atuongoze kwenye maombi. Karibu.

**Katibu:** Kwanza kabisa kabla hatujafunga kwa maombi, kwa niamba ya Kamati hii ya Voi ningelipenda kutoa shukrani zetu

kwa ajili ya kufumilia hali zetu zile tulizo nazo wengine hatuwezi kunena kwa ufasaha, wengine labda hatuwezi kusimama, imebidi tuketi, wengine tuna mambo marefu kuliko vile mda ulivyopangwa lakini mtusamehe na mtuwie radhi na tumeshukuru zaidi kwa yote ambao mmetufanyia kuchukua maoni yetu. Imani yetu ni kwamba yale yote ambayo tumeyatoa yatafika pale ambapo kunahitajika katika referendum, ama kura ya maoni na tena baada ya hivyo najua yatarudishwa hapa ili kuhakikisha ya kwamba je, yale yote ambayo tumetoa yamenekiliwa, au bado. Na kama yamenakoliwa, kuna lingine ambalo tulisahau? Tutapata fursa ingine kwa imani ya Mwenyezi Mungu ya kwamba wakati huo utafika. Kwa hivyo ningependa bila kupoteza wakati tusimame tumbakishie Mungu shukrani na Mungu awabariki mahali popote mtakapoenda. Wale ambao hawajapata fursa, wameingia saa hii, kesho tuko Tausa vile mlivyotangaziwa na Commissioner wetu ikiwa utaweza kufika, uko uhuru. Tuombe.

Mungu wetu tunakushukuru kwa sababu tulikuomba ya kwamba tukaanze kuchukuliwa maoni yetu pamoja na wewe, pamoja na macommissioners wetu, na Bwana tulianza na tukaomba ya kwamba tutakapomaliza tummalize na wewe. Na sasa tumemaliza kwa njia ya amani na kwa njia ya uvumilifu na kwa njia ya upendo, nakwa njia zote zile ambazo umetuwezeza. Umetupatia usalama mpaka tukafika mwisho. Sasa tunatawanyika kila mmoja akirudi mahali pake, wengine watalala manyumba ambayo hawajazoea kwa ajili ya kukondisha, wengine watarudi manyumbani, Bwana tutakaposafiri either kwa miguu, ama kwa magari Bwana wewe mwenyewe tunaomba utulinde mpaka tutakapokutana tena. Tunaliinua jina lako takatifu ili Bwana tutakuwa na shukrani zaidi wakati Katiba hii itaandikika na itaanza kutekelezwa. Tunashukuru kwa haya machache kwa jina la Jesu Kristo Mwokozi wetu. Amen.

Neema ya Bwana wetu Yesu Kristo, na mapenzi ya Mwenyezi Mungu baba, na ushirika wa Roho Mtakatifu uwe pamoja nazi zote mpaka hata milele. Amen.

Wanakamati tafadhali tukutane halafu tummalize.

Meeting ended at 5.30 p.m.

**&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&**